JAMUHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

RIPOTI YA JUMLA YA KUHUSU UKAGUZI WA UFANISI NA UKAGUZI MAALUM KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 MACHI, 2014

RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI TANZANIA

Machi 2014

JAMUHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Dira

Kuwa kituo cha ufanisi katika ukaguzi wa hesabu za Serikali na taasisi za umma

Dhamiri

Kutoa huduma ya ukaguzi wa hesabu yenye tija ili kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma. Katika kutoa huduma zenye ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:

Uadilifu

Sisi ni asasi adilifu inayotoa huduma kwa namna isiyo na upendeleo.

Ubora

Sisi ni wanataaluma wanaotoa huduma zenye ubora kwa kuzingatia viwango kubalifu vya ukaguzi

Uaminifu

Tunahakikisha kuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala wa sheria.

Mtazamo wa watu

Tunatazama na kukazia zaidi katika matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha wa kazi.

Uvumbuzi

Sisi ni asasi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya asasi.

Matumizi bora ya rasilimali

sisi ni asasi inayothamini na kutumia rasilimali za umma ilizokabidhiwa kwa umakini mkubwa.

JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Mtaa wa Samora, S.L.P 9080, Dar es SalaamSimu ya Upepo: "Ukaguzi", Simu: 255(022)2115157/8, Nukushi: 255(022)2117527, Barua Pepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

Kwa majibu tafadhali taja
Kumb. Na. FA. 27/249/01 **28 Machi, 2014**

Mheshimiwa Dr. Jakaya M. Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 9120,
Dar es Salaam.

Yah: Kuwasilisha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi inayojumuisha Taarifa tatu (3) za Ukaguzi wa Ufanisi na tatu (3) za Ukaguzi maalum kwa mwaka wa fedha 2012/2013

Kwa mujibu wa ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ninawasilisha kwako ripoti yangu ya tano ya ukaguzi wa ufanisi na ukaguzi maalum zilizofanyika katika mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Taarifa hii inajumuisha taarifa tatu (3) za ukaguzi wa ufanisi na tatu za ukaguzi maalum katika Serikali kuu na Serikali za Mitaa ambazo zinatarajiwa kuwasilishwa mbele ya Bunge letu Tukufu katika kikao cha Mei 2014.

Nawasilisha.

Ludovick S. L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

YALIYOMO

Orodha ya vifupisho....................vii
Dibaji....................viii
Shukrani....................xi
Muhtasari xiii

SURA YA KWANZA
UTANGULIZI

1.1 Usuli 1
1.2 Mamlaka....................1
1.3 Madhumuni ya ripoti ya jumla 2
1.4 Mchakato wa kuthibitisha takwimu 3
1.5 Muundo wa ripoti....................3

SURA YA PILI
USIMAMIZI WA UTAMBUZI NA UTOAJI WA HUDUMA KWA WATOTO WAISHIO KATIKA MAZINGIRA HATARISHI TANZANIA

2.1 Utangulizi....................4
2.2Tulichochunguza katika utoaji wa huduma kwa WWKMH 5
2.3Sababu za kuchunguza WWKMH 6
2.4Tulichokiona....................7
2.5Hitimisho la ukaguzi....................12
2.6Mapendekezo ya ukaguzi....................15

SURA YA TATU
USIMAMIZI WA UKAGUZI WA BIDHAA ZINAZOINGIZWA KUTOKA NJE YA TANZANIA

3.1 Utangulizi....................18
3.2Tulichoangalia katika uingizaji wa bidhaa kutoka nje....................18
3.3Sababu za kuchunguza uingizaji wa bidhaa kutoka nje 20
3.4Matokeo ya ukaguzi....................20
3.5Hitimisho la ukaguzi....................31
3.6Mapendekezo ya ukaguzi....................32

SURA YA NNE
USIMAMIZI WA UKAGUZI WA CHAKULA

4.1 Utangulizi....................34
4.2Tulichokiangalia katika ukaguzi wa chakula....................34
4.3Sababu za kuchunguza ukaguzi wa chakula....................35
4.4Matokeo ya ukaguzi....................36
4.5Hitimisho la ukaguzi....................48

4.6Mapendekezo ya ukaguzi……………………………………………………50

SURA YA TANO
USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA

5.1 Utangulizi……………………………………………………………………52
5.2 Tulichokiangalia katika uwindaji wa wanyamapori……………………53
5.3 Sababu za kuchunguza uweindaji wa wanyamapori……………………53
5.4 Matokeo ya ukaguzi…………………………………………………………55
5.5 Hitimisho la ukaguzi………………………………………………………63
5.6 Mapendekezo ya ukaguzi…………………………………………………64

SURA YA SITA
USIMAMIZI WA TAKA ZA HUDUMA YA AFYA TANZANIA

6.1 Utangulizi……………………………………………………………………66
6.2 Tulichokiangalia katika taka za huduma ya afya………………………66
6.3 Sababu za kuangalia taka za huduma ya afya……………………………67
6.4 Matokeo ya ukaguzi…………………………………………………………68
6.5 Hitimisho la ukaguzi………………………………………………………73
6.6 Mapendekezo ya ukaguzi…………………………………………………73

SURA YA SABA
USIMAMIZI WA UDHIBITI WA GHARAMA KATIKA MANUNUZI YA UMMA

7.1 Utangulizi……………………………………………………………………77
7.2 Tulichokiangalia katika manunuzi ya umma………………………………77
7.3 Sababu ya kuangalia manunuzi ya umma…………………………………78
7.4 Matokeo ya ukaguzi…………………………………………………………79
7.5 Hitimisho la ukaguzi………………………………………………………90
7.6 Mapendekezo ya ukaguzi…………………………………………………91

SURA YA NANE
MADHAIFU YALIYOTAMBULIWA KUJIRUDIA KATIKA SHUGHULI ZA SERKALI

8.1 Utangulizi……………………………………………………………………94
8.2 Madhaifu ya kawaida yaliyobainishwa……………………………………94
8.3 Hitimisho la jumla…………………………………………………………108
8.4 Mapendekezo kwa Ofisi ya Waziri Mkuu…………………………………109

Kiambatanisho I 112

ORODHA YA VIFUPISHO

INTOSAI	-	Umoja wa Kimataifa wa Taasisi Kuu za Ukaguzi
OWM-TAMISEMI	-	Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali Mitaa
SNAO	-	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Swedeni
WWKMH	-	Watoto Wanaoishi Katika Mazingira Hatarishi
TBS	-	Shirika la Viwango Tanzania
TRA	-	Mamlaka ya Mapato Tanzania
GPSA	-	Wakala wa Huduma za Manunuzi Serikalini
WMU	-	Wizara ya Maliasili na Utalii
TFDA	-	Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania
WHO	-	Shirika la Afya Duniani
CITES	-	Mkataba wa Biashara ya Kimataifa katika Mimea na Wanyama Hatarini Kutoweka
MSD	-	Bohari ya Madawa
ISO	-	Shirika la Kimataifa la Viwango

Dibaji

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti yangu ya tano ya jumla ya ukaguzi ufanisi na ukaguzi wa maalum. Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi inahusisha ripoti tatu za ukaguzi uliofanyika kwenye Serikali Kuu (Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa). Ripoti ya ukaguzi Maalum, kwa upande mwingine, inahusisha ripoti tatu za ukaguzi uliofanyika kwenye Serikali Kuu (Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Fedha).

Taarifa hii inalenga kutoa kwa wadau wetu (Wabunge, Maafisa wa Serikali Kuu na za Mitaa, vyombo vya habari, wafadhili, Asasi zisizo za kiserikali, Asasi za Kiraia n.k) muhtasari wa mambo yaliyoonekana kwenye kaguzi mojamoja sita (6) za ufanisi na Maalum zilizotolewa hadi kufikia mwezi Machi 2014. Maelezo zaidi ya muhtasari huu yanaweza kusomwa kutoka kwenye ripoti kamili zilizotolewa kwa Afisa Masuuli husika.

Taarifa hii inawasilishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kulingana na Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 34(1) na (2) ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma namba 11 ya mwaka 2008.

Chini ya Ibara 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama inavyorekebishwa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha kwa Rais kila taarifa aliyotoa kufuatana na Ibara ndogo (2) ya Ibara iliyotajwa. Mara taarifa hiyo inapopokelewa, Rais anamwelekeza mtu husika anayetakiwa kuwasilisha taarifa hiyo mbele ya kikao cha kwanza cha Bunge kabla ya kupita siku saba toka kikao cha kwanza cha Bunge kuanza. Ibara hiyohiyo inamruhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha ripoti yake kwa Spika wa Bunge iwapo Rais kwa sababu zozote zile atashindwa kuwasilisha ripoti hiyo kwa Spika kama inavyotakiwa kisheria.

Kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya Mwaka 2008 kumeimarisha uhuru wa utendaji kazi wa ofisi yangu katika kutimiza jukumu lake kikatiba. Haya ni matokeo ya juhudi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge letu Tukufu.

Uhuru wa kufanya kazi katika ofisi yangu utaniwezesha kudhibiti matumizi ya rasilimali za ofisi ikiwa ni pamoja na rasilimali watu na fedha ambavyo vitaniwezesha kufanya kazi yangu bila kuingiliwa na mamlaka yoyote.

Sheria hii imepanua mawanda ya ukaguzi kwa kunipa mamlaka kufanya kaguzi za ufanisi (utendaji), utambuzi, mazingira na ukaguzi maalumu mbali ya ukaguzi wa kawaida wa taarifa za fedha.

Kimsingi, taarifa hii imeniwezesha kutoa maoni huru kwa Bunge kuhusiana na matumizi sahihi na uwajibikaji, uwazi na uadilifu katika matumizi ya rasilimali za umma kwenye maeneo ya usimamizi wautambuzinautoaji wa huduma kwawatoto walio katika mazingira hatarishi, usimamizi wa ukaguzi wabidhaa kutoka nje ya nchi, usimamizi wa ukaguzichakula, usimamizi wa uwindajiwanyamapori, usimamizi wa takazitokanazo na huduma ya afya naUsimamizi wakudhibiti gharamakatikamanunuzi ya umma.Zaidi ya hayo, nia ya ukaguzi ilikuwa kuangalia kama rasilimali zimetumika vizuri ili kuleta matokeo yaliyotarajiwa kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi kama ilivyotarajiwa na kupitishwa na Bunge kwenye maeneo yaliyotajwa.

Ni vizuri kufahamu kwamba wakati ofisi yangu inafanya ukaguzi na kutoa taarifa ya utendaji wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Programu na Mashirika ya Umma na shughuli mbalimbali kulingana na sheria na taratibu zilizopo, mwisho kabisa wajibu wa kuhakikisha utekelezaji wa mapendekezo niliyoyatoa upo kwa Maafisa Masuuli.

Ni matarajio ya Bunge kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi watahakikisha kuwa zipo taarifa za fedha kuhusu usimamizi wa rasilimali za umma katika Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya umma kuhusiana na tija na ufanisi kwenye utekelezaji wa programu. Ofisi yangu inachangia kwa kutoa mapendekezo ili kuboresha utendaji katika sekta ya umma. Kwa jinsi hiyo, Serikali kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na ofisi yangu zina mchango mkubwa wa kutoa kwa Bunge katika kujenga imani kwa Umma katika usimamizi wa rasilimali za Umma. Ingawa majukumu yanatofautiana, matarajio ya usimamizi bora ya rasilimali yanafanana.

Ili kukidhi matarajio ya Wabunge na Umma kwa ujumla Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya mapitio ya njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji wa uwajibikaji katika sekta ya Umma. Aidha, tunahakikisha ukaguzi wetu unalenga na kuyapa kipaumbele maeneo

muhimu ili kuchangia katika maendeleo ya sekta ya umma. Kwa kuwa kazi ya ukaguzi ni chachu katika usimamizi wa fedha, tunaendelea kujadili masuala yanayoathiri utawala/uongozi katika sekta ya umma, hasa katika utoaji wa taarifa za usimamizi wa fedha na masuala ya utawala bora.
Napenda kutambua mchango wa wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa juhudi kubwa walizofanya katika kutimiza malengo tuliyojipangia licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo ni pamoja na kukosa fedha za kutosha, kukosa vitendea kazi na mishaharaduni na wakati mwingine kufanyakazi kwenye maeneo yasiyopitikakiurahisi.

Natarajia kuwa Bunge litaona taarifa hii kuwa ni muhimu katika kuiwajibisha Serikali kutokana na jukumu lake la usimamizi wa fedha za Umma na utoaji wa huduma kwa Watanzania. Hivyo nitafurahi kupata mapendekezo ya jinsi gani nitaweza kuboresha taarifa yangu hii kwa siku zijazo.



Ludovick S. L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

____

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
S.L.P. 9080,
Dar es Salaam,
28 Machi, 2014

SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioniwezesha kutimiza wajibu wangu wa Kikatiba wa kutoa taarifa hii ya ukaguzi wa ufanisi na upembuzi. Napenda kumshukuru kila mfanyakazi katika ofisi yangu kwa jitihada zao kuniwezesha kutimiza matakwa ya katiba ya kutoa ripoti ya ukaguzi wa thamani ya fedha. Nalazimika kuishukuru familia yangu na za wafanyakazi katika ofisi yangu kwa uvumilivu wao wakati wa uandaaji wa taarifa hii.

Napenda kuishukuru Serikali na Bunge letu Tukufu kwa kuendelea kuisaidia Ofisi yangu katika kutekeleza majukumu yake.

Vile vile, shukrani za pekee ziende kwa wafadhili hasa Ofisi yaTaifa ya Ukaguzi ya Sweden (SNAO), Serikali ya Sweden kupitia Wakala wa Kimataifa wa Maendeleo wa Sweden (SIDA), Serikali ya Ujerumani kupitia GIZ, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa la Marekani (USAID),Idara yaMaendeleo ya Kimataifa (DFID), Benki ya Dunia kupitia mradi wa "the Public Financial Management Reform Programme funding" na wote waliotutakia mema ambao walichangia kwa njia moja au nyingine kwa nia ya kuleta mabadiliko katika ofisi yangu. Mchango wao katika kuendeleza uwezo wa wafanyakazi kiakili, kimfumo wa teknologia ya mawasiliano na nyenzo mbalimbali vimechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio yetu.

Hali kadhalika, ninawiwa kuwashukuru wadau wengine wote ikiwa ni pamoja na Afisa Masuuli wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Fedha, Shirika la Viwango la Tanzania na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania kwa ushirikiano na kutupatia taarifa muhimu zilizohitajika wakati wa uandaaji wa ripoti mojamoja ambazo ni chanzo cha ripoti hii ya ujumla.

Shukrani za kipekee ziende kwa jamii ya wanataaluma na wataalamu wa kada mbalimbali kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili,Chuo kikuu cha Kilimo Sokoine, Chuo Kikuu cha Ardhi, wataalamu wa kujitegemea na maafisa wastaafu kwa michango yao ambayo iliboresha ripoti za ukaguzi wa ufanisi kupitia ukosoaji na uhakiki walioufanya wa rasimu ya ripoti

Napenda kuishukuru Kamati ya Hesabu za serikali (PAC) ambayo itapitia ripoti hii na tunatazamia Maelekezo yake itakayoyatoa.

Napenda piakuishukuruKamati yaHesabu za Serikali Kuu (PAC) ambayo ripoti hiipamoja na ripoti binafsizitafanyiwakwa ajili ya uchunguzinamajadiliano.Tunatarajia michango ya kamati ya Hesabu ya Serikali kuunamaelekezovikiwemomajadiliano yaripoti hizo.

Mwisho, napenda kuwashukuru Maafisa Masuuli wote na watumishi wote wa ummaTanzania nzima, bila kusahau mchango wa walipa kodi ambao ripoti hii tunaitoa kwao. Mwenyezi Mungu awabariki wote kama mnavyojitoa katika kusimamia uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma nchini.

Muhtasari

Ukaguzi wa ufanisi unatoa tathmini ya kiwango ambacho taasisi inayokaguliwa inatumia rasilimali zake katika kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi. Ukaguzi wa ufanisi unaangalia kama malengoya awaliyaliyowekwa yamefanikiwa. Matokeo ya utekelezaji yanaangalia kama yamezingatia uwekevu, tija na ufanisi. Mapendekezokwa ajili ya kuboreshayanatolewa katikamaeneo yenye mapungufu.

Mdhibiti na MkaguziMkuu waHesabu za Serikali Tanzaniaamepewamamlaka yakufanya ukaguzi wa ufanisikutokakwenye Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008. Ukaguzi wa ufanisihufanyika kwa mujibu wa viwango vya umoja wa kimataifa wa Taasisi Kuu za Ukaguzi(INTOSAI) vinavyohusu Ukaguziwa ufanisi kwani Ofisi ya Taifa yaUkaguzini mwanachama wa INTOSAI na kwa hiyo ina wajibu wakuzingatia viwango hivi.

Uwasilishaji wa ripoti hii unalenga kusaidia Wabunge, Serikali, vyombo vya habari, umma na wadau wengine kuchukua maamuzi ili kutekeleza mapendekezo kwa ajili ya kuongeza uwekevu, tija na ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za serikali.

Ripoti hii inatoa muhtasari wa matokeo makuu, hitimisho na mapendekezo ya utendaji katika ripoti za ukaguzi wa ufanisi na maalumu uliofanyika hadi kufikia Machi 31, 2014. Pia inatoa uchambuzi wa matokeo ya kawaida katika kaguzi zilizofanyika, hitimisho kwa ujumla na mapendekezo ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya kuboresha.

Ukaguzi wa ufanisi unaohusu utambuzi na utoaji huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ulichunguza kama

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wana mchakato wa kiufanisi na uwazi katika kutambua na kutoa huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Ukaguzi umetokana na tatizo la ongezeko la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi licha ya jitihada zilizokwishafanyika.

Ukaguzi umebaini udhaifu katika mifumo yautambuzi wa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, utoaji wa huduma kwa watoto hao, utoaji taarifa ya mafanikio ya ufuatiliajinatathmini ya utendajiwa shughuli zawatoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Ilihitimishwa kuwaWizara ya AfyanaUstawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI hawajaweza kusimamia vya kutoshaili kuhakikisha kwambautambuzinautoaji wa huduma kwawatoto waishio katika mazingira hatarishi una tija na unafanyika kiufanisi.

Vile vile, ukaguzi wa usimamizi wa ukaguzi wa bidhaa kutoka nje ya Tanzania ulichunguza kama Shirika la Viwango linalenga kupunguza uingizwaji wa bidhaa zilizo chini ya kiwango kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na wa kutosheleza wa bidhaa zinazoingizwa. Ukaguzi umefanyika kutokana na kuongezeka kwa malalamiko ya wananchi ya ongezeko la kuwepo kwa bidhaa zisizokidhi viwango nchi . Ukaguzi ulibaini kuwa Shirika la Viwango Tanzania halikujipanga vya kutosha kukagua bidhaa zinazoingizwa nchini katika maeneo ya kuingizia bidhaa. Vihatarishi havizingatiwi vya kutosha wakati wa kuandaa mpango na utekelezaji wa ukaguzi. Kulikuwa na tofauti kubwa kati ya malengo na ukaguzi halisi.

Udhaifu pia ulibainishwa katika mgawanyo wa rasilimali, ufuatiliaji wa utendaji, tathmini na utoaji taarifa. ilihitimishwa kuwa ukaguzi uliofanyika haukuwa na uwekevu, tija na ufanisi kutokana na mbinu iliyotumika awali wakati wa kuweka mipango na kutekeleza kutozingatia vihatarishi, kutokuwepo kwa malengo ya wazi,

mikakati ya ukaguzi kutoelezwa ipasavyo na lengo kwa ujumla la kupunguza bidhaa zisizokidhi viwango na ukaguzi wa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje kutofikiwa.

Vile vile, katika ukaguzi wa usimamizi wa ukaguzi wa chakula, ukaguzi ulichunguza kama Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania inatimiza dhamira yake ya kulinda ubora wa chakula katika nchi. Sababu ya kufanya ukaguzi huu ulitokana na kilio kutoka kwa wananchi juu ya kuwepo kwa bidhaa za chakula zisizo salama kwa matumizi ya binadamu. Ukaguzi umegundua kwamba ukaguzi wa chakula haupangwi ipasavyo. Hii pia ni inatokana na kutozingatia vihatarishi katika hatua ya kupanga.

Pia utekelezaji wa ukaguzi ulibainika kuwa na madhaifu kwani haukufanyika katika viwanda hatari vya kusindika chakula ikiwa ni pamoja na bidhaa hatari za chakula katika maeneo ya kuingizia bidhaa toka nje ya nchi. Adhabu havikutumika ipasavyo kwa waliokiuka kanuni. Uratibu kati ya Mamlaka ya Chakula na Dawa na idara nyingine za serikali haukusimamiwa vya kutosha. Pia kulikuwa na udhaifu katika usimamizi, tathmini na utoaji taarifa za shughuli ya ukaguzi wa chakula. Hii imesababisha kuhitimisha kwamba ukaguzi wa bidhaa za chakula katika viwanda vya uzalishaji na maeneo ya kuingizia bidhaa hizo toka nje ya nchi haukuwa na tija na haukufanyika kiufanisi. Mamlaka ya Chakula na Dawa haijaweza kutekeleza dhamana iliyopewa. Vile vile, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kama wizara mama haijaweza kuchukua hatua za kutosha ili kuhakikisha kwamba uwepo wa bidhaa za chakula ambazo si salama unapunguzwa.

Ukaguzi wa Ufanisi wa usimamizi wa wanyama pori ulichunguza kama Wizara ya Maliasili na Utalii inasimamia na kufuatilia ipasavyo shughuli za uwindaji wa wanyamapori, ukusanyaji wa mapato yatokanayo na wanyamapori katika mapori ya akiba na mapori tengefu. Uchunguzi huu ulisababishwa na malalamiko ya umma juu ya kuongezeka kwa matukio ya ujangili nchini. Ukaguzi umebaini kwamba vifo vya tembo vilivyosababishwa na ujangili vimeongezeka katika kipindi cha mwaka 2009 hadi 2012.

Hii ni kwa sababu ya udhaifu uliopo katika doria kwani hazipangwi na kufanyika ipasavyo. Pia, doria hazifuatiliwi na kutathminiwa ipasavyo. Ufinyu wa bajeti nao pia umechangia kwa kiasi kikubwa.

Wizara ya Maliasili na Utalii haikuhusisha ipasavyo Mamlaka ya Bandari Tanzania na Mamlaka ya Kodi ya Mapato Tanzania katika udhibiti wa ujangili na usafirishwaji wa nyara haramu nje ya nchi. Pia mfumo wa kuwazawadia watoa taarifa hauna ufanisi. Ilikuwa ni vigumu kujua mgawanyo wa mapato yatokanayo na rasilimali ya wanyamapori hasakiasi cha fedhakinachopelekwaHazina, Idara ya Wanyamapori na kiasi kinachobakia katika Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori Tanzania. Ukaguzi ulihitimisha kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii haijatekeleza wajibu wake wa kuhakikisha kuwa sheria ya wanyamapori inatekelezwa ipasavyokwa lengo kupunguza matumizi haramu yawanyamapori.Hii imechangiwa na: kugawanya rasilimali zake bilakulengamaeneo korofi kwa ajili yakupambana naujangili; pia siwadau wote waliohusika kikamilifu katika utekelezaji wa sheria ya uhifadhi wanyamapori; kutofuatilia kwa ukaribu shughuli zauwindaji;naugumukatikakugawamapato yatokanayo na maliasili kwa wadau husika kwa kuzingatia uwiano.

Halikadhalika, umefanyika ukaguzi wa ufanisi juu ya usimamizi wa taka za hatarishi zinazotokana na tiba.ukaguzi huu ulilenga kuchunguza kama Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI) zinahakikisha kwamba taka hatarishi zinazotokana na tiba zinasimamiwa vizuri ili kulinda afya ya jamii na mazingira. Msukumo wa kufanya ukaguzi huu ulitokana na kuongezeka kwa kiwango cha taka zinazotokana huduma ya afya dhidi ya athari zake kwa afya ya binadamu na mazingira. Matokeo ya ukaguzi yanaonyesha kukosekana kwa takwimu za taka zinanazotokana na huduma ya afya hii inatokanana na udhaifu wa mfumo wa utoaji wa taarifa za huduma ya afya uratibu usio ridhisha kati ya Wizara, Sekretareti za Mikoa, Serikali za Mitaa na Vituo vya Tiba; na udhaifu wa mipango juu ya usimamizi wa taka hatarishi zinazotokana na tiba katika ngazi zote za utendaji.Kwa ujumla, udhibiti wa taka hatarishi haufuatiliwi kwa ukaribu, haufanyiwi tathmini na kupewa rasilimali ipasavyo..

Matokeo haya yapelekea kuhitimisha kwamba,pamoja na uwepo wa miongozo na kanuni mbalimbali zinazohusu usimamizi wa taka hatarishi zinazotokana na huduma ya afya hapa nchini, udhibitwa taka hatarishi kutoka kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati bado si mzuri. Hii ni kwa sababu Wizara ya Afya na Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI hawajaweka udhibiti katika usimamizi wa taka hizo.

Usimamizi na udhibiti wa gharama katika manunuzi ya umma pia ulichunguza ili kubaini endapowizara, taasisi za serikali pamoja na Serikali za Mitaa zina njia sahihi na makini ambazo zinafanya kazi kwa lengo la kudhibiti gharama katika manunuzi ya umma. Ukaguzi huu umetokana na malalamiko yaliyotolewa na wadau mbalimbali kuhusu mfumo wa sasa wa ununuzi katika sekta ya umma pamoja na utekelezaji wake kama unaleta manufaa yanayokusudiwa kupitia bidhaa zinazonunuliwa pamoja na huduma zinazotolewa.

Kwa mujibu wa utafiti katika eneo la manunuzi ya tiketi ya kusafiri kwa usafiri wa ndege, ukaguzi ulibaini ya kuwa bei elekezi hazikutumika kiusahihi ili kulinda maslahi ya umma wakati wa manunuzi hayo. Bei zilizolipwa zilitofautiana na bei zilizokuwepo katika mikataba; hapakuwa na taarifa muhimu kwenye tiketi ambazo zingesaidia katika kuthibitisha uhalali wa gharama za tiketi zilizodaiwa na mawakala; mashirika ya ndege na njia za kupita zilichaguliwa bila kuzingatia gharama zake; malipo yalifanyika bila ya kuhakiki ankara zilizotolewa na mawakala kwa kulinganisha na tiketi zilizotolewa; manunuzi ya tiketi yalifanyika kwa dharura kipindi kifupi kabla ya safari; hakukuwa na ushindani wakati wa manunuzi ya tiketi; kulikuwa na udhaifu wa uratibu wa Tasisi na mamlaka kama Wizara ya fedha, GPSA na Mamlaka ya Usafiri wa Anga katika kusimamia na kutathmini manunuzi ya tiketi za ndege.

Kwa upande wa manunuzi katika ujenzi wa majengo ya umma, ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa makadirio na makisio ya gharama za miradi; kulikuwa na tofauti kubwa kati ya gharama zilizotolewa na wazabuni dhidi ya makadirio ya wahandisi; ilibainika pia kuwa makadirio ya gharama (BOQ) hayakuandaliwa kwa usahihi na hivyo kusababisha marekebisho mengi ya

kimahesabu ambayo ama yalizingatiwa au kupuuzwa kabisa wakati wa mchakato wa mwisho wa kimahesabu katika zabuni zilizofanyiwa tathimini.

Mipango ya manunuzi haikuendana na hali halisi kwani aslimia 58 ya miradi iliyotekelezwa haikujumuishwa katika Mpango wa Manunuzi wa mwaka *wa* aasisi husika. Kulikuwa na udhaifu wa taasisi zinazohusika kama Wizara ya Fedha na GPSA katika kusimamia na kutathimini mwenendo wa shughuli za manunuzi.

Ukaguzi ulihitimisha kwamba taasisi zinazofanya manunuzi hazikutekeleza kwa usahihi sheria za manunuzi ya umma kwa lengo la kulinda maslahi ya umma. Hakukuwa na uangalifu katika kudhibiti gharama wakati wa mchakato wote wa manunuzi ingawa sheria ya manunuzi imetoa mwanya wa kulinda rasilimali za umma dhidi ya matumizi makubwa na yasiyo ya lazima. Manunuzi ya umma hayakusimamiwavema wala kufanyiwa tahimini na taasisi za udhibiti (kwa mfano GPSA) ili kubaini endapo maslahi ya umma yanalindwa ipasavyo.

Kulingana namalengo ya ukaguzinamatokeoya masuala yalioonekana katika kaguzi sitazilizofanywakamailivyoelezwa kwa kifupi katika ripoti hii, kuna masuala ambayo yanahitaji kutahadharishaSerikaliili kuhakikisha serikaliinaendesha na kusimamia shughulizake kitija na kiufanisi.Haya ni madhaifu katika Mipango, Bajeti, Uratibu, Utekelezaji washeria, Usimamizi wa Takwimu, Ufuatiliaji, TathmininaTaarifa yaUtendaji. Na kusababisha mapungufu katika ubora wa utoaji wa huduma kwa wananchi.

Uchambuzi uliofanywa unamaanisha kuwepo kwa madhaifu katika zoezi la usimamizi. Tija na ufanisi katika shughuli za serikali ni vigumu kufikiwa kutokana na madhaifu yanayoonekana kujirudiarudia katika kaguzi nyingi zilizofanyika. Maeneo yote

Yaliyotambuliwa na madhaifu yana mahusiano na matokeo yake huathirikila mmoja.Mipango duni dhahiri huathiri utendaji mzima wa shughuli katika suala labajeti,ufuatiliaji, tathmini na ripoti ya

utendaji .Tathmini duni hutoa nafasi ndogo kwa ajili ya kuboresha kwani watoa maamuzi hawana taarifa sahihi. Usimamiaji duni watakwimu, ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa unaathiri upatikanaji wa taarifa sahihi ambazo zingeweza kutumika kwa ajili ya kuboreshahapo baadaye.

Uchambuzi wa hapo juu na hitimisho vinatusababisha kutoamapendekezoili kuboreshautekelezaji wa shughuli za serikali hapo baadayekamaifuatavyo:

Ofisi ya Waziri Mkuuinapaswa kuhakikisha kuwavyombovyote vya serikali(Serikali kuu na Serikali za Mitaa):

- **zinaweka mipango ya utekelezaji ya kina itakayoshughulikia shughuli muhimu zilizotambuliwa;uchambuziwa vihatarishi ufanyike katikahatua ya awali ya mipangoilikutenga rasilimali kiufanisi;Ugawaji wa rasilimali ufanyike kwa misingi yamahitaji ya kipaumbele na hatari ya iliyopo;**
- **Zina mfumo madhubuti kwa ajili ya kutathminiutendaji wawadaukatika programu inayoratibiwa ya serikali;**
- **Znatumia kiusahihi adhabu kwataasisi za serikali na/ auwanaokiuka sheria ili kuepukakupoteza auutendaji mbovu;**
- **Zinapitia ipasavyo adhabu zilizowekwa ilikuhakikisha kuwa zinasaidia kufikia lengo lakuzuia matukio ya uvunjaji wa sheria; na**
- **Znatengeneza seti ya viashiria muhimu vyautendaji nahatuaya kutathmini utendajiwao**

Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishea:

- **Mara kwa mara inafuatilia na kutathmini utendaji wa vyombo vyote vya serikali nchini ili kuhakikisha kuwa mipango ya ufuatiliaji na tathmini kwa vyombo vya serikali inatekelezwa kiusahihi na ripoti za utekelezaji zinawasilishwa mara kwa mara; na**
- **Kuweka mfumo na utaratibu wa kina kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini shughuli za serikali / programu katika ngazi ya taifa.**

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli

Ukaguziufanisinimuhimukwa sababu unalenga kuboresha uwajibikaji na utendaji wa serikali ili wananchi wapate thamani ya fedha kutoka katika huduma za serikali. Vigezo mbalimbali vinatumika katika kuchagua mwelekeo wa ukaguzi wa ufanisi na maalumu. Miongoni mwa mengini pamoja nakilio cha wananchi na umuhimu wa eneo hilo ukilinganisha na sababu za kijamii na kiuchumi.

Ukaguzi wa ufanisi hutoa lengo na kufanya tathmini ya kujenga ya kiwango ambacho mkaguliwa ametumia rasilimali zake katika kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi. Ukaguzi wa ufanisi una tathmini kama shughuli, mipango au miradi inayohusisha fedha za umma katika Wizara, Idara, Serikali za Mitaana Mashirika yote ya umma imesimamiwa kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi. Uwekevu, tija na ufanisi unaweza kuelezwa kama ifuatavyo:

- **Uwekevu** – kupunguza gharama ya rasilimali zinazotumika katika shughuli kwa kuzingatia na ubora sahihi.
- **Tija** – uhusiano kati ya matokeo, katika suala la bidhaa, huduma, na rasilimali zilizotumika kuzalishia.
- **Ufanisi** – kiwango ambacho malengo yamefikiwa na uhusiano kati ya athari iliyokusudiwa na athari halisi katika shughuli husika.

1.2 Mamlaka ya kukagua

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Tanzania ana mamlaka ya kisheria ya kufanya ukaguzi wa Ufanisi kupitia Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

Kifungu cha 28 cha Sheria hii kinasema “Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwalengo la kuthibitisha **uwekevu, tija na ufanisi** katika matumizi yafedha au rasilimali za taasisi ya umma,

anaweza kukagua,kuchunguza na kutoa ripoti, kadiri atakavyoona inafaa, juu ya:

(a) Matumizi ya fedha na rasilimali za umma katikawizara, idara, mamlaka za mitaa na mamlakanyingine za serikali;
(b) Utekelezaji wa majukumu ya maafisa masuuli, wakuu wa idara na wakuu wa taasisi mbalimbali za umma;

(c) Utekelezaji wa matakwa ya sheria ya mazingira, kanuninasera ya ndaniya mazingiranaviwango".

Ukaguzi wa ufanisi unalenga kuangalia kamamalengoya awali yaliyowekwa mwanzo wa shughuli yamefanikiwa. Kisha unaangalia kama uwekevu, tija na ufanisi vimezingatiwa. Mapendekezokwa ajili ya kuboresha yanatolewa katika maeneo yaliyoonekana kuwa na mapungufu.

Ukaguziu nafanyika kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa ufanisi. Viwango hivyo vinahitajitimu ya ukaguzi kupanga na kutekeleza ukaguzi ili kupata ushahidi wa kutosha ambao utakuwa kigezo cha mapungufu yaliyoonekana na hitimisho kwa kuzingatia lengo la ukaguzi. Timu ya ukaguzi inaamini ushahidi uliopatikana unatoa msingi sahihi wa mapungufu yaliyoonekana na hitimisho kwa kuzingatia lengo la ukaguzi.

1.3 Madhumuni ya ripoti

Utoaji wa ripoti hii ya jumla unalenga kuwapa taarifa muhimu Waheshimiwa Wabunge, vyombo vya habari, umma pamoja na wadau wengine kufanya maamuzi yatakayoongeza uwekevu, tija na ufanisi katika shughuli za serikali. Hadi mwisho wa ripoti hii, muhtasari wa kila ripoti umehitimishwa kwa masuala ya kuulizwa na Kamati ya Bunge ya Usimamizi kwa Maafisa Masuuli.

Ripoti hii haikusudii kuwa mbadala wa ripoti sita ambazo zimeelezwa kwa muhtasari katika sura zinazofuata. Ili kuweza kupata uelewa zaidi juu ya matokeo ya ukaguzi kwa ajili ya kuwahoji maafisa masuuli katika maeneo husika, msomaji anashauriwa kusoma ripoti kamili. Hizi ni ripoti za ukaguzi wa ufanisi na maalumu zinazohusu maeneo yafuatayo:

- Usimamizi wa Utambuzi na utoaji wa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi;
- Usimamizi wa ukaguzi wabidhaa kutoka njeyaTanzania;
- Usimamizi wa ukaguzi wa chakula;
- Usimamizi wa uwindaji wanyamapori;
- Usimamizi wa taka zitokanazo na huduma za afya; na
- Usimamizi wa kudhibiti gharama katika manunuzi ya umma.

1.4 Mchakato wa uthibitisho wa takwimu

Wizara zilizokaguliwa, Idara na Wakala walipewa fursa yakujadili na kutoa maoni yao juu yamatokeo ya ukaguzinakusahihisha makosa ya usahihi wa taarifa.

1.5 Muundo wa ripoti

Ripoti hii ya jumla imeundwa katika sura nane. Sura ya Kwanza inatoa utangulizi sehemu ya ukaguzi wa ufanisi, mamlaka, madhumuni ya ripoti ya jumla, viwango vinavyotumika na mchakato wa uthibitisho wa takwimu;

Sura ya Pili hadi ya Saba ina muhtasari wa ripoti sita za maeneo yaliyokaguliwa. Muhtasari unalenga kile kilicho chunguzwa, sababu kwa ajili ya uchunguzi, nini kilichoonekana, hitimisho na mapendekezo yaliyotolewa kwa Afisa Masuuli . Maeneo haya ni kama ifuatavyo: Sura ya Pili imelenga usimamizi wa utambuzi na utoaji wa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi; Sura ya Tatu inazungumzia ukaguzi wa ufanisi juu ya usimamizi wa ukaguzi wa bidhaa kutoka nje; Sura ya Nne ni juu ya usimamizi wa ukaguzi wa chakula ya nchi; Sura ya Tano inalenga usimamizi wa uwindaji wa wanyamapori; Sura ya Sita inashughulikia usimamizi wa taka zitokanazo na huduma za afya; Sura ya Saba inalenga usimamizi wa kudhibiti gharama katika manunuzi ya umma; wakati

Sura ya Nane inaelezea madhaifu ya kawaida yaliyoonekana katika shughuli za serikali katika kaguzi za ufanisi zilizofanyika.

SURA YA PILI

USIMAMIZI WA UTAMBUZI NA UTOAJI WA HUDUMA KWA WATOTO WANAOISHI KATIKA MAZINGIRA HATARISHI TANZANIA

2.1 Utangulizi

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii imepewa mamlaka ya kuhakikisha ya kwamba kuna mfumo imara wa kutoa huduma kwa makundi ya watu wanaoishi katika mazingira hatarishi nchini. Makundi hayo ni pamoja na: Watoto, Watu wenye ulemavu na Wazee. Vilevile,Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia Serikali za Mitaa inajukumu la kuratibu na kuwezesha utoaji wa huduma za msingi kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi (WWKMH) nchini.

Kazi ya Utoaji huduma kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi (WWKMH) inasimamiwa na Sheria kuu mbili, ambazo ni Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 na ile ya Serikali za Mitaa Na.7 ya mwaka 1982.

Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ndio sheria mama inayotoa mwongozo wa usimamizi na utoaji huduma kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi (WWKMH). Sheria hii inazitaka Serikali kuu na zile za Mitaa kuhakikisha ya kwamba kuna mfumo imara wa kutoa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi nchini.

Sheria Na. 7 ya Serikali za Mitaa inazitaka Serikali za Mitaa kuratibu utekelezaji wa utoaji wa huduma za msingi kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi katika maeneo yao.

Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 1996 imeainisha haki za msingi za mtoto ikiwa ni pamoja na ile ya kuishi, ulinzi na usalama na maendeleo.

2.2 Tulichokichunguza

Ukaguzi ulichuguza kama Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI) wanazo taratibu zenye ufanisi na uwazi katika kutambua na kutoa huduma kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi (WWKMH). Ukaguzi ulijikita zaidi katika Usimamizi wa Watoto Wanoishi Katika Mazingira Hatarishi katika eneo la utambuzi, utoaji wa huduma, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa utoaji huduma kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi nchini.

Malengo mahususi ya ukaguzi yalikuwa ni:

- Kubainisha kama Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI wanahakikisha ya kwamba kuna utambuzi yakinifu wa Watoto Walio katika Mazingara Hatarishi (WWKMH) katika Serikali za Mitaa;
- Kutathmini kama Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI) wamehakikisha kuwepo kwa ufanisi na tija katika utoaji wa huduma kwa WWKMH; na
- Kuangalia utoshelevu na ufanisi wa usimamizi, ufuatiliaji na utathmini wa shughuli za utoaji huduma kwa WWKMH zilizofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Serikali za Mitaa.

Ukaguzi ulijikita katika ngazi zote za utawala nchini yaani Taifa, Mkoa na Serikali za Mitaa ili kuweza kupata picha ya kina ya namna ambavyo maswala ya WWKMH husimamiwa nchini. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI) ndiyo waliokuwa wakaguliwa wakuu.

Mikoa 7 kati ya mikoa 25 inayotekeleza mipango ya utoaji huduma kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi (WWKMH) nchini ilitumika kama maeneo ya ukaguzi. Aidha, ukaguzi uliangalia utekelezaji wa utoaji wa huduma hizo kwa

watoto katika kipindi cha miaka minne ya fedha (kuanzia 2009/10 mpaka 2012/13). Kipindi hicho cha miaka minne kilichaguliwa kwa kutilia maanani ya kwamba utekelezaji wa Mpango Mkakati wa utoaji huduma kwa WWKMH kwa awamu ya kwanza ulianza mwaka 2008. Vile vile, kipindi cha miaka minne kilichaguliwa ili kuweza kuona mwelekeo wa utendaji wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM -TAMISEMI) toka utekelezaji wa Mpango Mkakati wa utoaji huduma kwa WWKMH ulipoanza mwaka 2008 mpaka Juni 2013.

2.3 Sababu Zilizopelekea Kukagua Utoaji Huduma kwa WWKMH

Serikali imefanya juhudi mbalimbali katika kutatua matatizo ya Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi kama vile utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa WWKMH wa 2007-2010 (Awamu ya Kwanza) na 2013-2017 (Awamu ya Pili), kutunga na kupitisha Sheria ya watu wenye Ulemavu (2010) na Sheria ya Mtoto (2009) na kanuni zake, utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Kuimarisha Ubora wa Huduma, Misaada, na Ulinzi kwa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi Tanzania.

Pamoja na juhudi zote madhubuti zilizochukuliwa na serikali kushughulikia masuala ya WWKMH, na ukweli kwamba mipango mbalimbali imeshatekelezwa na serikali, tatizo la kupunguza madhara ya WWKMH bado linaendelea kuwepo.

Mipango hiyo hapo juu ilikabiliwa na changamoto wakati wa utekelezaji wake. Mipango ya WWKMH imeripotiwa kuwa na ushahidi wa manufaa kidogo sana[1], ushiriki mdogo wa WWKMH katika michakato ya utambuzi, kutokuratibiwa kwa utoaji huduma kwa WWKMH[2], huduma zilitolewa kwa idadi ndogo ya watoto na kaya kwa njia ambazo kijamii zilikuwa si za kuridhisha na wakati mwingine zenye kunyanyapaa, ukosefu wa ufuatiliaji na tathmini ya huduma zilizotolewa kwenye mipango ya WWKMH haswa iliyolenga katika ulinzi wa kijamii na pia mipango michache tu ilishughulikia uhifadhi na uhamasishaji wa ulinzi wa kijamii.

[1] Evaluation Report of MVC National Costed Plan of Action (2007 – 2010) and Children and women in Tanzania report Volume I 2010

[2] Influencing Policy for Children in Tanzania (REPOA Report - 2009

Mipango ya umma ya WWKMH imefika maeneo machache tu ya Tanzania kwani hadi Disemba 2011 ni asilimia 63 tu ya kata zilikuwa zimekwisha fanya utambuzi na kati ya WWMH waliotambuliwa, asilimia 75 walikuwa wamepatiwa walau mojawapo ya mahitaji ya msingi.

Ili kuweza kutoa majibu katika swala hili, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu iliamua kufanya ukaguzi wa Usimamizi wa Utambuzi na Utoaji wa huduma kwa Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi nchini.

2.4 Matokeo ya Ukaguzi

Matokeo ya ukaguzi yameainishwa katika maeneo makuu manne, ambayo yanahusiana na mifumo ya utambuzi, utoaji wa huduma, utoaji wa taarifa za utekelezaji wa utoaji huduma za msingi, na ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa huduma zilizotolewa kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi (WWKMH).

2.4.1 Mifumo ya Utambuzi wa WWKMH ni dhaifu

Mfumo wa utambuzi wa WWKMH ni dhaifu na haufanyi kazi Vizuri. **Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa kamati za WWKMH zisizojitosheleza na zisizo fanyakazi/mfu. Katika halmashauri zote tisa (9) zilizotembelewa kamati hizi zilikuwa bado hazijaundwa. Katika Halmashauri sita[3] (6) kati ya tisa (9) zilizotembelewa, Kamati za Ukimwi za Halmashauri zilikuwa bado hazijajumuisha kazi za WWKMH, msukumo ulikuwa kwa WWKMH walioathiriwa na virusi vya ukimwi na wale waliohitaji msaada wa kielimu tu.**

Vilevile katika Halmashauri zote tisa (9) zilizotembelewa, kamati za Mitaa/vijiji za WWKMH zilikuwa bado hazijaundwa. Wastani wa asilimia 52 pekee ya mitaa/vijiji ndivyo zilizokuwa zimeunda kamati za WWKMH katika Halmashauri tisa zilizotembelewa. Vivyo hivyo, nusu ya Halmashauri ya wilaya zilizotembelewa zilikuwa zimeunda chini ya asilimia 50 ya kamati za vijiji/mitaa za WWKMH. Hata hivyo,

[3] Kinondoni MC, Liwale DC, Musoma MC, Makete DC, Sumbawanga MC, and Ilala MC

nusu ya 50% ya kamati za WWKMH zilizokuwa zimeundwa zilikuwa hazifanyi kazi.

Hali hii ilitokana na usambazaji na mafunzo ya utambuzi yasiyojitosheleza, kamati za WWKMH kufanya kazi kwa hiari, upangaji na utengaji wa mafungu ya fedha kwa shughuli za utambuzi usiotosheleza na pia uhaba wa zana kufanya utambuzi.

2.4.2 Madhaifu katika Utoaji wa Huduma kwa WWKMH

Huduma zilizotolewa kwa WWKMH zilibainika kuwa na mapungufu mbalimbali. Ukaguzi ulibaini kuwa huduma zilizotolewa kwa WWKMH zililenga zaidi aina moja ya huduma wakati huduma nyingine zilitolewa kwa nadra sana au hazikutolewa kabisa.

Msaada wa elimu ulitolewa kwa asilimia 80 ya Halmashauri za Wilaya saba zilizotembelewa na timu ya ukaguzi wa ufanisi, wakati theluthi moja tu ya Halmashauri hizo zilitoa misaada ya Kisaikolojia kwa watoto hao. Asilimia 40 pekee ya Halmashauri hizo Saba ilitoa msaada wa kuinua uchumi kwa WWKMH na zaidi ya asilimia 40 ya Halmashauri ilitoa msaada wa kimatibabu kwa WWKMH.

Kwa mujibu wa mapitio ya taarifa ya mwaka 2012/13 ya WWKMH ya Idara ya Ustawi wa Jamii na Taarifa ya tathmini ya programu za WWKMH ya mwaka 2012/13 ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ilibainika kwamba kati ya WWKMH 894,515 waliotambuliwa nchini, ni asilimia 44 pekee (sawa na WWKMH 394,425) walikwisha patiwa kiwango cha chini cha mahitaji (walau mahitaji ya msingi matatu). Kwa upande mwingine, waliobakia asilimia 56 (sawa na WWKMH 500,090) walipatiwa walau hitaji moja la msingi kati ya mahitaji mengi ya msingi waliyohitaji kupatiwa.

Hii ina maana ya kwamba matarajio ya WWKMH ya kupata walau kiwango cha chini cha mahitaji ya msingi hayakufikiwa. WWKMH waliohitaji kiwango cha chini cha mahitaji ya msingi (walau mahitaji matatu) walipata aidha mojawapo au mahitaji mawili ambayo hayakukidhi mahitaji yao yaliyotambuliwa, na kwa hiyo WWKMH iliwalazimu kutafuta njia mbadala ili kupata msaada uliohitajika. Njia hizo ni pamoja na kuombaomba barabarani, wizi wa mifukoni, kujiuza kimwili n.k.

Kwa upande mwingine WWKMH hawakuweza kuhakikishiwa upatikanaji wa huduma za msingi walizohitaji na hakukuwa na uhakika wa mwendelezo wa utoaji wa huduma za msingi kwa watoto hao kwa kuwa sehemu kubwa ya utoaji wa huduma hizo ulitegemea zaidi nia na uwezo wa wafadhili mbalimbali.

Hali hii ya kushindwa kutoa huduma za msingi kwa WWKMH imesababishwa na mambo mbalimbali kama vile upungufu katika utengaji wa rasilimali fedha na watu. Ilibainika ya kuwa baadhi ya Halmashauri zilikuwa hazijatenga fedha kwa ajili ya utoaji huduma kwa WWKMH na vile vile kutokuwa na Maafisa wa Ustawi wa Jamii). Sababu nyingine ni uratibu dhaifu katika utoaji wa huduma kwa WWKMH. Japokuwa mahitaji ya msingi ya WWKMH yalianishwa lakini huduma zilitolewa bila kuzingatia mahitaji hayo yaliyoanishwa na kunyumbulishwa.

Pia ukosefu wa takwimu za WWKMH zilizohuishwa na kutokuwepo kwa taarifa sahihi za utoaji huduma ilifanya kazi ya kutoa huduma kwa watoto WWKMH kutokufanyika kwa ufanisi.

2.4.3 Uwepo wa Mifumo Isiyoendelevu ya Utoaji wa Huduma kwa WWKMH

Ukaguzi ulibaini uwepo wa mifumo ya utoaji wa huduma kwa WWKMH isiyo endelevu kutokana na sababu zifuatazo:

- **Utegemezi wa wafadhili kwa kiasi kikubwa;**
- **Kuna mgawanyo duni wa rasilimali kwa ajili ya utoaji wa huduma kwa WWKMH usiotosheleza toka ngazi ya Taifa hadi Halmashauri;**
- **Ilibainika pia kulikuwa na upungufu wa maafisa wa Ustawi wa Jamii katika ngazi mbali mbali za utawala, kuanzia ngazi ya Mkoa mpaka ya kata; na**
- **Kulikuwa na utaratibu dhaifu wa utoaji wa huduma kwa WWKMH katika ngazi zote za utawala (kuanzia ngazi ya taifa mpaka Halmashauri).**

Kuwepo kwa Mgawanyo usiotosheleza wa rasilimali za WWKMH toka ngazi ya Taifa mpaka ngazi ya Wilaya: **Ilionekana ya kwamba kwa muda mrefu bajeti ya idara ya Ustawi wa Jamii imekuwa ni asilimia 1 ya bajeti yote ya MoHSW ambayo hujumuisha huduma za walemavu na wazee na huduma za marekebisho ya watoto, ustawi wa kifamilia, ustawi na ulinzi wa watoto na maendeleo ya watoto. Kiasi hichi kidogo kilikwaza utendaji na utekelezaji wa huduma za ustawi kwa WWKMH. Ingawa Idara ya Ustawi wa Jamii ilifanya juhudi nyingi ili kuhakikisha kiwango kinaongezeka, bado kiwango kiliendelea kuwa finyu. Hali hii ilionekana katika Halmashauri kwani ni asilimia 48 (yaani 63 kati 134) ya halmashauri zimekuwa zinatenga fedha kwa ajili ya shughuli za WWKMH nchini.**

Vilevile ilionekana kuwepo kwa upungufu wa maofisa wa ustawi wa jamii katika ngazi za Mikoa, Halmashauri na kata**: Kwa wastani tatizo hili la uhaba wa maofisa ustawi wa jamii lilionekana katika ngazi hizo za mikoa na Halmashauri. Uhaba katika ngazi ya mikoa ni asilimia 12 na upande wa Halmashauri ni asilimia 80.**

Vile vile, *kulikuwa na uratibu dhaifu/hafifu katika ngazi za kitaifa na halmashauri:* Japokuwa Kamati ya Taifa ilipaswa kuratibu wizara za serikali katika ngazi ya kitaifa kwa kutumia vikao, vikao havikuitishwa na hata katika ngazi ya halmashauri, idadi kubwa ya wadau hawakuratibiwa vizuri na Halmashauri.

2.4.4 Ufuatiliaji na Utathmini wa Shughuli za WWKMH Usiotosheleza

Mifumo ya Ufuatiliaji na tathmini za utendaji wa shughuli za utoaji huduma za msingi kwa WWKMH katika ngazi zote za kitaifa na serikali za mitaa ulibainika kuwa dhaifu. Kiasi kidogo cha ufuatiliaji na utathmini kilikuwa kimefanyika. Aidha, ofisi ya ukaguzi ilipofanya tathmini ya taarifa hizo ilibaini kuwa maafisa walitumia 50% ya vigezo/ viashiria vya utendaji (6 kati ya viashiria 15) na kati ya hivyo vingine havikuwa viashiria vizuri katika kupima utendaji wa mfumo wa WWKMH.

Vigezo ambavyo havikuangaliwa ni vile vilivyohusu mgawo/utengaji wa fedha, utoaji wa huduma za msingi kwa WWMH, utambuzi wa WWKMH, utoji wa huduma na taarifa za maswala ya WWKMH.

Hii ilihusiana na upungufu wa maarifa wa maafisa wa Ustawi wa Jamii na maafisa wengine katika usimamiaji, ufuatiliaji na utathmini wa utendaji wa shughuli za WWKMH. Matokeo yake, usimamizi, ufuatiliaji na utathmini wa utendaji wa shughuli za WWMH haukufanywa kwa kiasi cha kutosha.

2.4.5 Udhaifu katika Utoaji wa Taarifa za Kiutendaji zautoaji huduma kwa WWMH

Mojawapo ya kasoro zilizoonekana wakati wa ukaguzi ni pamoja na udhaifu katika utoaji wa taarifa za mafanikio yaliyofikiwa katika utoaji wa huduma kwa WWKMH. Ngazi mbalimbali za kiserikali (yaani Taifa, Mkoa na Halmashauri za Wilaya) zilikuwa na jukumu la kutoa taarifa za robo mwaka na ile ya majumuisho ya mwaka mzima, lakini ukaguzi ulibaini ya kwamba hili halikuwa likifanyika.

Ukaguzi ulibaini ya kwamba asilimia 67 ya ofisi za umma katika ngazi mbalimbali za kiserikali (yaani Taifa, Mkoa na Halmashauri za Wilaya) hawaandai na kuwasilisha ripoti kwa mamlaka husika kama ilivyotakiwa. Halmashauri za Wilaya zilibainika kutowasilisha ripoti za robo mwaka na ile ya jumla katika Ofisi za Katibu Tawala Mikoa. Vivyo hivyo, Ofisi ya Katibu Tawala Mikoa, zilishindwa kuwakilisha taarifa zao kwenda Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI. Ukaguzi ulibaini pia ya kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ilitegemea kupata taarifa kuhusiana na utoaji wa huduma kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi kutoka kwa watoa huduma binafsi badala ya kupata taarifa hizo kupitia muundo uliopo wa kiserikali.

Wakati huo huo, mfumo wa kudhibiti takwimu za Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi ulionekana kuwa ni dhaifu na haukidhi matakwa ya Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi. Hivyo, mfumo huo wa takwimu haukuwa unafanya kazi iliyokusudiwa kwa ufanisi na matokeo yake ni kukosekana kwa takwimu za uhakika na kupelekea serikali kutokuwa na uwezo wa kufanya maamuzi

sahihi na kufuatilia utekelezaji wa malengo iliyojiwekea juu ya utoaji wa huduma hizo kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi.

Dosari hizo zilizoainishwa hapo juu katika utendaji wa utoaji wa taarifa zinazohusiana na utoaji huduma kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi ulitokana na ukosefu wa ufuatiliaji madhubuti wa kuhakikisha wadau wote wanaandaa taarifa na kuziwasilisha kwa wakati. Vilevile, ilichangiwa na tofauti za mifumo ya uandaaji wa ripoti ya wadau wanaotekeleza shughuli za utoaji huduma kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi.

2.5 Hitimisho la Ukaguzi

Pamoja na ukweli kwamba kuna mfumo unaoeleweka wa kutambua na kutoa huduma kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia

Idara ya Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI) hawakusimamia vya kutosha kuhakikisha ya kwamba utambuzi na utoaji wa huduma kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi unafanyika kwa tija na ufanisi.

Vilevile, ukaguzi ulihitimisha ya kwamba:

2.5.1 Utambuzi wa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi haukufanyika kwa Ufanisi

Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na Wizara ya Afya hawa kuwa na mifumo ya uthibiti kwa upande wa utambuzi wa WWKMH na uchambuaji wa mahitaji yao. Matokeo yake, walitambuliwa watoto wahitaji wachache na waliobaki waliachwa wakijihangaikia wenyewe. Kwa upande mwingine, hata hao wachache waliotambuliwa, mahitaji yao halisi haya kubainishwa sawa sawa na hivyo huduma zilizotolewa hazikuwa na misaada tosha kwao.

Utambuzi wa WWKMH usiokidhi kiwango ulisababishwa na udhaifu katika upangaji wa utambuzi wa WWKMH na pia kutokuwa na

ufanisi katika usimamizi kwa upande wa watendaji katika ngazi ya kitaifa (Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI na Wizara ya Afya na Ustawi Jamii) na pia watekelezaji katika ngazi za jamii haswa halmashauri. Katika ngazi hizi mbili za serikali, suala la upangaji halikupewa uzito na shughuli za utambuzi zilichukuliwa kama kazi za kushtukiza. Sababu nyingine ilikuwa ni kutofanya kazi kwa kamati za WWKMH, uratibu mbovu wa masuala yanayohusiana na WWKMH na kushindwa kusambaza na kutumia kwa mapana miongozo ya utambuzi wa WWKMH.

2.5.2 Huduma Zitolewazo kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi Hazikidhi Mahitaji yao ya Msingi

Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Serikali za Mitaa hawakutimiza majukumu yao makuu ya utoaji wa huduma kama vile elimu, makazi, matibabu, misaada ya kisheria n.k kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi kwa ufanisi. Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi wanao hitaji msaada wa serikali hawakupatiwa huduma za msingi kulingana na mahitaji yao halisi.

Wakati Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi walihitaji huduma za msingi kama vile elimu, makazi, matibabu na msaada wa kisheria; serikali ilishindwa kutoa huduma zote hizo kwa wakati mmoja na hivyo kutoa sehemu tu ya mahitaji ya huduma hizo. Hivyo, Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi waliweza kupatiwa hitaji moja au mawili kati ya mahitaji yao matatu ya msingi.

Kushindwa huko kwa Serikali kuweza kuwapatia huduma hizo za msingi kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi kwa ujumla umepelekea watoto hao kuwa na mzigo mkubwa wa maisha na hivyo kujaribu kutafuta njia mbadala za kujisaidia wenyewe.

Sababu kubwa nne zilizochangia kuifanya Serikali ishindwe kutoa huduma za msingi kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi ni pamoja na:

Mosi, uwepo wa mifumo isiyo endelevu na isiyokidhi viwango vya utoaji wa huduma kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira

Hatarishi. Sehemu kubwa ya utoaji wa huduma za msingi kwa watoto hao ilitegemea zaidi misaada mingi iliyotolewa na wafadhili na pia asasi za kiraia na zisizo za serikali ziliachiwa jukumu la utoaji huduma za msingi kwa watoto hao bila usimamizi madhubuti.

Pili, kutokuwepo kwa Maafisa Ustawi wa Jamii wa kutosha waliopatiwa mafunzo ya kusimamia utoaji wa huduma za msingi kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi. Tatizo hili lilionekana katika ngazi ya Mkoa na ile ya Serikali za Mitaa.

Tatu, kutokuwa na uratibu katika ngazi zote za serikali kwa kuwa kila taasisi iwe ni katika Serikali (katika ngazi ya kitaifa au Serikali za Mitaa) au washirika wanaotekeleza utoaji wa huduma za msingi kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi wanatoa huduma hiyo bila kushirikiana. Hali hii imesababisha muingiliano wa utendaji kazi na hivyo kutokuwa na ufanisi katika matumizi ya rasilimali chache zilizotengwa kwa huduma hizo za msingi kwa watoto hao.

Nne, ni udhaifu wa utafutaji wa rasilimali kwa ajili ya utoaji huduma za msingi kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi. Ukaguzi ulibaini ya kwamba, watendaji na uongozi wa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, na Serikali za Mitaa hazijachukua jitihada za kutosha ili kuhakikisha ya kwamba rasilimali fedha na watu zinazohitajika katika kutoa huduma kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi zinapatikana.

2.5.3 Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa utoaji huduma kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi ni Dhaifu

Ukaguzi umebaini ya kuwa uwezekano wa taasisi za serikali zinazohusika na utoaji wa huduma hizi kuboresha utendaji wao ni mdogo. Hili linatokana na uwepo wa mifumo dhaifu ya ufuatiliaji na tathmini za utendaji wa taasisi za serikali katika shughuli zote zinazohusika na utoaji wa huduma za msingi wa Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi. Pamoja na ukweli ya kwamba kuna viashiria mbalimbali vya utendaji katika utoaji wa huduma hizo za msingi lakini viashiria hivyo havijafafanuliwa vizuri na kuonyesha

ni kwa kiasi gani vitatumika katika ngazi tofauti za usimamizi na utoaji wa huduma kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi nchini.

Vile vile, mfumo dhaifu wa usimamizi wa utoaji taarifa kuhusiana na huduma za msingi zinazotolewa kwa Watoto walio Katika Mazingira Hatarishi haulengi kuboresha uwajibikaji na ufanisi katika ufikishaji wa huduma hizo kwa walengwa.

2.6 Mapendekezo ya Ukaguzi

Ofisi ya Taifa ya ukaguzi imetoa mapendekezo katika maeneo makuu matatu, ambayo ni: utambuzi, utoji wa Huduma, na Ufuatiliaji na tathmini ya kazi za utoaji huduma kwa Watoto walio Katika Mazingira Hatarishi.

Mapendekezo hayo yametolewa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kama yalivyoainishwa hapo chini:

2.6.1 Mapendekezo kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii haina budi:

i. Kutengeneza utaratibu utakao hakikisha ya kwamba mahitaji ya Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi yana chambuliwa kwa kina na kushirikisha wadau wote katika Halmashauri. Vilervile, taarifa hizo zitumike katika uandaaji wa bajeti na rasilimali zingine zinazohitajika katika utoaji wa huduma kwa Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi;

ii. Kutengeneza taratibu na mikakati ya kuhakikisha ya kwamba utoaji wa huduma kwa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi unaendana na mahitaji ya msingi yaliyo ainishwa ya Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi;

iii. Kutengeneza Viashiria vinavyopimika vya muda mfupi na mrefu vya utekelezaji wa Mipango ya utoaji huduma kwa Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi;

iv. **Kutengeneza mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ambayo itawezesha ufuatiliaji wa mwelekeo wa utekelezaji wa malengo na mipango ya utoaji huduma kwa Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi; na**

v. **Kuorodhesha watoa huduma wote nchini na kutoa utaratibu unao eleweka wa utoaji wa taarifa za utendaji utakao hakikisha ya kwamba washirika wote wanatoa taarifa za utekelezaji wa huduma wanazozitoa kwa Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi katika maeneo yao.**

2.6.2 Mapendekezo kwa Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa haina budi:

i. **Kuandaa mipango ya utambuzi wa Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi na iainishe vijiji na mitaa yote nchini;**

ii. **Halmashauri zote zianzishe mipango kazi madhubuti ya utekelezaji wa utoaji wa huduma kwa Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi na kuhakikisha ya kwamba mipango hiyo itatekelezwa kwa wakati;**

iii. **Kuandaa taratibu na miongozo ya namna ambavyo huduma mbalimbali zitolewazo kwa Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi kama vile makazi, elimu, afya n.k zitakavyotolewa;**

iv. **Kuhakikisha ya kwamba kuna uwiano wa msingi wa mgawanyo wa rasilimali watu na bajeti zinazotengwa kwa ajili ya Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi; na**

v. **Halmashauri za Wilaya zinafuatiliaji na kutathmini utekelezaji wa utoaji wa huduma za msingi kwa Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi na matokeo yanatolewa / taarifa ziwasilishwe katika ngazi zote za utawala yaani Taifa, Mkoa na Halmashauri.**

SURA YA TATU

USIMAMIZI WA UKAGUZI WA BIDHAA ZA NJE TANZANIA

3.1 Utangulizi

Kwa maendeleo ya taifa lolote lile, ubora wa bidhaa ni muhimu sana ili kuweza kuhakikisha uwepo wa usalama wa kiafya kwa watumiaji na mazingira yanayo wazunguka. Jukumu hili la kuhakikisha bidhaa zote zinazotumika nchini Tanzania zina ubora uliokusudiwa linafanywa na Shirika la Viwango nchini (TBS). Shirika hili lipo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Shirika la Viwango nchini limepewa mamlaka ya kutengeneza viwango vya bidhaa na kuhakikisha viwango hivyo vinatekelezwa na kufuatwa kwa bidhaa zote zinazotengenezwa nchini na zinazoingizwa nchini.

Majukumu ya Shirika la Viwango nchini (TBS)

TBS ina majukumu makuu yafuatayo kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Viwango Na. 2 ya 2009:

- Kutengeneza/kuandaa na kusimamia viwango vyote vya kitaifa;
- Kutoa ushauri viwandani juu ya uzalishaji wa bidhaa bora;
- Kupima na kuhakikisha vipimo vinavyotumika viwandani;
- Kukagua bidhaa mbalimbali zile zinazozalishwa nchini na zinazoingizwa nchini kutoka nchi mbalimbali;
- Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa viwandani;
- Kuelimisha umma juu ya masuala yote yanayohusu uwekaji na usimamiaji wa viwango pamoja na udhibiti wa ubora wa bidhaa viwandani; na
- Utoaji wa leseni na vyeti vya ubora.

3.2 Tulichokichunguza

Ukaguzi ulichunguza kama Shirika la ViwangoTanzania (TBS) linafanya ukaguzi wakutoshana wa mara kwa mara wa bidhaa zinzaoingia nchini kwa ufanisi ili kupunguza uwepo wa bidhaa zenye ubora hafifu. Mkaguliwa mkuu ni Shirika la Viwango

Tanzania (TBS) ambalo lipo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Ukaguzi ulilenga katika kaguzi za ubora wa bidhaa zinazo ingizwa nchini kutoka nchi mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kuwa Shirika linatekeleza jukumu la kudhibiti na kupunguza bidhaa hafifu katika soko la Tanzania.

Malengo makuu matatu ya Ukaguzi huu wa Ufanisi yalikuwa ni:

- **kutathmini kama usimamizi wa ukaguzi wa ubora wa bidhaa zinazoingia nchini ulifanywa kwa kuzingatia viashiria vya uwezekano au hatari ya bidhaa kuwa na ubora hafifu;**
- **kutathmini kama Wizara ya Viwanda na Biashara inafanya ufuatiliaji na utathmini wa shughuli za ukaguzi wa ubora wa bidhaa zinazoingia nchini kutoka nje; na**
- **kufahamu kama kuna udhaifu na sababu za udhaifu huo wa ukaguzi wa ubora wa bidhaa zinazoingia nchini kutoka nje kupitia Bandari na mipaka ya Tanzania.**

Masuala yaliyo angaliwa katika ukaguzi huu ni pamoja na mipango, miongozo, utekelezaji wa ukaguzi, uratibu, vipaumbele na kutoa taarifa juu yamatokeo ya ukaguzi wa ubora wa bidhaa zinazoingia nchini, hatua za kuchukua kwa wanaokiuka sheria pamoja na utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa bidhaa kutoka nje.

Ukaguziulifanyika kwa kuangalia utendaji wa kazi wa TBS wa kipindi cha miaka mitatu (3) ya fedha yaani kutoka mwaka 2010/11 hadi 2012/13 ili kufahamu mwenendo wa utendaji kwa kipindi hicho.

Ukaguzi uliangalia masuala ya bidhaa zinazotoka nje kupitia bandari ya Dar es Salaam (pamoja na bandari kavu kumi); na wakaguzi wa walitembelea ofisi za TBS katika mipaka ya Holili, Namanga, na Sirari. Pia maafisa mbalimbali kutoka TBS, Wizara ya Viwanda na Biashara, na Mamlaka ya Mapato Tanzania(TRA) walihojiwa juu yamasuala yanayo husiana na ukaguzi wa ubora wa bidhaa kutoka nje unaofanywa na TBS.

3.3 Sababu zilizopelekea kuchunguza Ukaguzi wa Bidhaa Nje

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi juu ya kuwepo kwa bidhaa zenye ubora hafifu nchini. Inakadiriwa kuwa kati ya asilimia 30 na 40 ya bidhaa zinazoingizwa nchini kila mwaka ni hafifu (TCAs 2009). Aidha, Ripoti ya ukaguzi wa fedha ya TBS (2012) ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ilibainisha kuwepo bidhaa mbalimbali ambazo ziliingizwa nchini na ziligunduliwa ya kuwa hazikidhi viwango na hazikuharibiwa au kurudishwa kwenye nchi zilipotengenezwa.

Asilimia 30 ya bidhaa zinazouzwa nchini Tanzania ni hafifu. Hii ina athiri afya za walaji na kukosesha Serikali mapato. Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI); Utafiti uliofanywa na CTI, 2012)

Kwa kuzingatia haya, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) aliamua kufanya ukaguzi wa ufanisi ili kuhafamu sababu ya tatizo la ongezeko la bidhaa zenye ubora hafifu na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa.

3.4 Matokeo ya Ukaguzi

3.4.1 Mapungufu katika mipangilio ya mchakato wa ukaguzi wa ubora wa bidhaa

Ukaguzi ulibainisha kuwa TBS haikuwa na mipango madhubuti kwa ajili ya ukaguzi wa ubora wa bidhaa zinazoingia kutoka nje katika maeneo ya Bandarini na mipakani. Udhaifu huu ulionekana katika mambo yafuatayo:

- Nyaraka/Miongozo iliyotumika haikuonyesha jinsi ya kufanya ukaguzi wa kuzingatia viashiria/vihatarishi vya uwepo wa bidhaa hafifu;
- Hakukuwa na taratibu zinazozingatia viashiria/vihatarishi vya uwepo wa bidhaa hafifu wakati wa ukaguzi;
- Hakukuwa na vipaumbele vya ukaguzi kwa kuzingatia viashiria hivyo; na
- Wakaguzi hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya mipango inayozingatia viashiria hivyo wakati wa ukaguzi wa ubora wa bidhaa.

Zana (Nyaraka na miongozo) inayotoa miongozo ya kaguzi za ubora wa bidhaa haionyeshi jinsi ya kufanya ukaguzi wa ubora wa bidhaa kwa kuzingatia viashiria vya uwepo wa bidhaa zenye ubora usio kidhi viwango: TBS haijaboresha uwezo wake wakutambua vihatarishi vikubwa au jinsi ya kuzuia kuingia kwa bidhaa hafifu na kuhakikisha kuwa ukaguzi unapangwa kwa kuzingatia vihatarishi husika.

Udhaifu uliotambuliwakutokana na miongozo hiyo ni pamoja na:

- Kutokuwa na mwongozo wa jinsi yakupanga kwa ajili ya ukaguzi, hasa aina mbalimbali za kaguzi zinazofanywa na TBS juu yabidhaa zinazoingia nchini kutoka nje;
- Kutokuwa na maelekezo ya utaratibu wa utoaji/utambuzi wa sampuli kwa ukaguzi wa bidhaa zinazoingia nchini kutoka nje katika bandari au mipaka;
- Kutokuonyesha jinsi gani wakaguzi wanatakiwa kutoa kipaumbele katika ukaguzi kwa kuzingatia aina ya bidhaa zinazoingia nchini kutoka nje ya nchi;
- Kutokuonyesha taratibu za kufuata wakati wa ukaguzi wa bidhaa zinazoingia kutoka nje;
- Haionyeshi muundo waripoti ya ukaguzi wa ubora wa bidhaa utakuaje; na
- Kutokuwaongoza wakaguzi jinsi gani wanaweza kuratibu kazi ya ukaguzi na watendaji wengine wa serikali ambao wanahusika katika ukaguzi wa bidhaa zinazoingia nchini kutoka nje.

Hakukuwa na muongozo wa kufuata wakati wa ukaguzi, unaoonyesha viashiria/vihatarishi vya uwepo wa bidhaa hafifu. Muongozo uliopo “Import Inspection Manual” hauoneshi ni hatua zipi za kufanya katika mambo yafuatayo;

- mbinu nzuri inayotathmini viashiria hatari vya kufahamu ni bidhaa zipi na waagizaji wapi wanatakiwa kusimamiwa kwa uangalifu ili walengwe wakati wa ukaguzi pindi waingizapo bidhaa nchini;
- njia sanifu ya kufanya ukaguzi, ambayo inahusisha utunzaji wa kumbukumbu kwa ajili ya kuhifadhi matokeo ya ukaguzi;

- mpango wa kufuatilia waagizaji wanaovunja taratibu na kuhakikisha kwamba marekebisho yanafanyika, faini zinalipwa, na ikibidi bidhaa hafifu zirudishwe zilikotoka au ziharibiwe.
- hakuna njia za uhakiki wa ubora wa kaguzi zinazofanyika.

Hakuna kipaumbele katika ukaguzi unaozingatia vitu hatarishi: ukaguzi uligundua kuwa Shirika la Viwango Tanzania halina njia nzuri ya kufahamu aina ya bidhaa zinazoingizwa nchini. Vilevile, ilibainika ya kuwa hakuna nyaraka yoyote inayoonyesha vitu gani vipewe kipaumbele.

Sababu za kutokuwa na vipaumbele katika ukaguzi bidhaa kutoka nje ni pamoja na:

- Ukosefu wa mipangilio inayozingatia viashiria vya msingi ambavyo vitasaidia kutambua bidhaa zenye vihatarishi vya uwepo wa bidhaa hafifu;

- Kushindwa kutumia takwimu za kielektroniki za bidhaa zinazoingia nchini kabla ya kuwasili. TBS haikutafuta takwimu hizo kutoka TRA na kuzitumia wakati wa kuandaa mipango na vipaumbele vya ukaguzi wa ubora wa bidhaa zinazoingia nchini; na

- Kukosa ufahamu kuhusu ukaguzi unaozingatia viashiria/vihatarishi vya uwepo wa bidhaa zenye ubora hafifu wakati wa ukaguzi.

Sababu za kuwa na mipango dhaifu katika ukaguzi wa ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini

Aidha, ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iligundua sababu kuu mbili za kuwa na mipango dhaifu ya ukaguzi wa ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini:

- kukosa maarifa ya kutosha juu ya mipango inayozingatia viashiria/vihatarishi vya uwepo wa bidhaa zenye ubora hafifu katika kaguzi zake

- Kutopata taarifa mapema za bidhaa zinazoingizwa nchini na hivyo kushindwa kuandaa mipango madhubuti ya kaguzi hizo.
  Ukosefu wa miongozo ya mipango ya ukaguzi wa ubora bidhaa zinazoingia nchini.

3.4.2 Mapungufu ya kaguzi za ubora wa bidhaa zinazoingia kutoka nje

Ukaguzi wa ubora wa bidhaa unaofanyika uligundulika kuwa na mapungufu kadhaa. Mapungufu hayo ni pamoja na;

- Hakukuwa na njia zilizozingatia viashiria/vihatarishi vya uwepo wa bidhaa zenye ubora hafifu kwa ajili ya kufanya ukaguzi;
- Tofauti kubwa kati ya kaguzi lengwa na zile zilizofanyika;
- Upungufu wa mgawanyo wa rasilimali watu ikilinganishwa na kiwango cha bidhaa zinazoingia nchini; na
- Uingizaji wa bidhaa nchini kupitia mipaka isiyo rasmi.

Ukosefu wa njia madhubuti za kuchagua bidhaa za kukagua kwa kuzingatia viashiria mbalimbali

Ukaguzi umegundua ya kwamba, TBS haikuwa na njia yoyote ya kutambua viashiria vya msingi katika kuchagua bidhaa za kukagua kutoka miongoni mwa zile zinazoingia nchini.

Pia, ilibainishwa kwamba ukaguzi wa ubora wa bidhaa haukuzingatia mazingira ya viashiria vya uhatarishi wa baadhi ya bidhaa yanayohusiana na maeneo husika.

Tofauti kati ya ukaguzi lengwa na halisi

Kupitia mapitio ya ripoti za mwaka za utendaji wa TBS kwa kipindi kutoka mwaka 2010/11 hadi 2012/13, ilibainika kuwepo kwa tofauti kubwa kati ya makadirio na idadi halisi ya kaguzi zilizofanywa na TBS. Tofauti ilibainishwa katika aina zote za ukaguzi yaani, ukaguzi kabla ya bidhaa kuingia nchini (PvoC), na ukaguzi baada ya bidhaa kuingia nchini (Destination Inspection - DI).

Ukaguzi wa ubora wa bidhaa kabla kuingia nchini (PvoC): ukaguzi huu ulianza kufanyika hapa nchini mwaka wa fedha 2011/12, katika ukaguzi huu, tofauti kati ya malengo na ukaguzi halisi kwa miaka miwili ni asilimia 241 kwa mwaka 2012 na asilimia 718 kwa mwaka 2012/2013. Hata hivyo kwa mwaka 2012/2013, tofauti ya makadirion bado iliendelea kuwa kubwa na imezidi asilimia 100. Hii inaonyesha ya kwamba idadi ya bidhaa zilizotegemewa kukaguliwa hazikuakisi hali halisi.

Ukaguzi baada ya bidhaa kuingia nchini: kwa wastani tofauti kati ya makadirio na ukaguzi halisi ilikuwa wastani wa asilimia 30 kwa mwaka 2012/13. Hii ni kwa sababu kaguzi hii ilipungua baada ya ukaguzi wa bidhaa kabla ya kuingia nchini kufanyika zaidi.

Sababu ya kuwepo kwa tofauti kubwa kati ya makadirio ya ukaguzi na ukaguzi halisi ni:

- Kushindwa kutumia takwimu za uhakika zinazoweza kupatikana kutoka Mamlaka ya Mapato (TRA). Taarifa hizi zingeweza kutumika kwa ajili ya kufanyia makadirio ya kaguzi zinazokuja, aina ya ukaguzi kwa kulinganisha na bidhaa zinazotegemewa kuingia nchini.
- Kushindwa kutumia uzoefu wa nyuma katika kufanya maamuzi na kuandaa mipango ya kaguzi mpya. Pamoja na kufahamu kuwa makadirio yalikuwa chini katika mwaka uliopita, TBS iliendelea kuwa na makadirio ya chini kwa mwaka unaofuata.

Upungufu wamgawanyo wa rasilimali watu ikilinganishwa na kiwango cha bidhaa zinazoingia nchini

Moja ya mamboambayo yamechangia kuwepo kwa mapungufu katika ukaguzi wabidhaa zinazoingia nchini ni uhaba wa wakaguzi katika bandari na baadhi ya mipaka.

Jedwali Na. 3.1 linaoneshauwiano wawastaniwa bidhaa (katika tani) kwa mwaka ikilinganishwa na idadi yawakaguzi.

Jedwali Na. 3.1:Uwiano wa Wastani wa Idadi ya Bidhaa kwa Mkaguzi

Bandari na Mipaka	Wastani wa Bidhaa kwa mwaka (Tani)	Idadi ya wakaguzi	Uwiano wa wastani wa Bidhaa kwa mkaguzi mmoja
Bandari ya Dar es salaam	7,380,000	5	1,476,000
Bandari ya Tanga	301,573	1	301,573
Namanga	123,166	1	123,166
Sirari	125,053	2	62,527
Holili	44,062	2	22,031
Horohoro	85,862	0[4]	-

Chanzo: Takwimu za Mizigo iliyoingizwa nchini (TRA) na Orodha ya Wakaguzi wa bidhaa

Uchambuzi wa uwiano wa wastani wa bidhaa kwa idadi ya wakaguzi katika Jedwali Na. 3.1 unaonyesha ya ukosefu wa rasilimali watu katika mgao wa kazi za ukaguzi katika bandari na mipaka inayosimamiwa na TBS.

Kwa mfano, kwa wastani bidhaa kwa mwaka katika Bandari ya Tanga ni mara saba zaidi ya zile zinazoingizwa kupitia mpaka wa Holili.

Kwa bandari ya Dar es Salaam, kwa wastani mkaguzi mmoja anatakiwa kukagua tani 1,476,000 za mizigo kwa mwaka. Hii ina maanisha kwamba mkaguzi mmoja katika bandari ya Dar es salaam anahudumia mizigo mara 67 zaidi ya ile inayohudumiwa na mkaguzi mmoja katika mpaka wa Holili.

3.4.3. Ubora usioridhishawa ukaguzi wabidhaa zinazoingia nchini

Kwa mujibu waShirika la Kimataifa la viwango (ISO /IEC 9001:1998 kifungu 0.2), ubora wa ukaguzi wa bidhaa zinazoingia nchinini

[4]Kwa miaka 2 iliyopita, mpaka wa Horohoro ulikuwa unafanya kazi bila ya kuwepo na mkaguzi wa TBS wa kukagua bidhaa zinazoingia nchini.

muhimu kuboreshwa na kuimarishwa kwa ajili ya kazi nyingine zinazofanana.

Ubora wa ukaguzi wa bidhaa zinazoingia nchini unaofanywa na TBS ulifanyiwa tathmini kwa kuzingatia mambo yafuatayo (1) idadi ya bidhaa hafifu nchini (2) idadi ya malalamiko kutoka kwa umma/watumiaji kuhusu ubora wa bidhaa zinazoingia nchini(3) idadi ya mapendekezo ya wakaguzi yaliyotekelezwa na yasiyotekelezwa na (4) utaratibu wa ufuatiliaji bidhaa zilizoruhusiwa kutoka kwa masharti ya kutouzwa mpaka ukaguzi ukamilike.

Katika mambo manne yaliyotajwa hapo juu katika kutathmini ubora wa ukaguzi, ilionekana kuwa tathmini ya ubora waukaguzi uliofanywa na TBS haukuwa wa kuridhisha kulingana na mambo yafuatayo;

Idadi ya bidhaa hafifu zilizoingizwa nchini : Imeonekana kuwa idadi ya bidhaa hafifu nchini imekuwa ikiongezeka kwa miaka mitatu kwa asilimia kati ya 30 na 40 kutoka mwaka 2010/11. Bidhaa hizo nyingi hupita katika bandari na mipaka ya Tanzania ambapo wakaguzi wa TBS walitakiwa kukagua bidhaa hizo.

Idadi ya malalamiko kutoka kwa umma/ watumiaji kuhusu ubora wa bidhaa zinazoingia nchini: idadi ya malalamiko yameendelea kuwa juu. Katika mwaka wa fedha 2010/11, TBS ilipokea malalamiko 18 kupitia vyanzo mbalimbali yanayohusu bidhaa hafifu kutoka nje, idadi iliongezeka hadi 44 katika mwaka uliofuata na mwaka 2012/13 idadi ya malalamiko imepungua hadi kufikia 33.

Kiwango cha utekelezaji wa mapendekezo ya wakaguzi: kiwango cha utekelezaji wa mapendekezo yaukaguzi kimepungua kutoka mwaka hadi mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu ya fedha, kutoka asilimia 57, 2010/11hadi asilimia 392012/13.

Hii inamaanisha ya kuwa, idadi ya bidhaa ambazo zinatakiwa kuharibiwa au kurudishwa katika nchi zilizotoka bado zinaingia nchini. Vilevile, ukaguzi ulibaini ya kwamba;

- Mosi, ukaguzi uliokuwa ukifanyika haukuwa yakinifu na hivyo kutoa mianya ya kuingiza bidhaa hafifu sokoni;
- Pili, utaratibu uliowekwa ili kuhakikisha ya kwamba mapendekezo yaliyotolewa na wakaguzi wa bidhaa yanatekelezwa hauko imara hivyo bidhaa mbalimbali kuweza kuingia nchini bila ya kugundulika; na
- Tatu, taasisi mbalimbali za serikali ambazo zilitakiwa kushirikiana na Shirika la Viwango katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na na wakaguzi wa viwango vya bidhaa hazitoi ushirikiano ulionuiwa. Hii ni kwa sababu ya udhaifu wa uratibu uliopo katika kuhakikisha kuwa taasisi hizo zinashirikiana kikamilifu ili kuweza kutekeleza mapendekezo hayo.

Ufuatiliaji dhaifu wa bidhaa zilizoruhusiwa kuingia nchini kwa masharti: Muongozo wa ukaguzi wa bidhaa zinazoingia nchini uliotolewa na Shirika la Viwango nchini una mapungufu mbalimbali ambayo yanatoa mianya ya kuingiza bidhaa zenye ubora hafifu na kukwepa adhabu husika pale waagizaji wa bidhaa wanapokosea.

Mojawapo ya utaratibu ambao Shirika la Viwango nchini limejiwekea ni kutoa matokeo ya vipimo vya maabara ya bidhaa zilizokaguliwa kuhakiki ubora wake ndani ya muda wa kati ya siku tatu mpaka tano. Shirika limeshindwa kutoa matokeo hayo ndani ya kipindi ilichojipangia na hivyo kuliweka Shirika la Viwango nchini katika shinikizo kubwa kutoka kwa wateja wanaoingiza bidhaa nchini na hivyo kuruhusu baadhi ya bidhaa hizo kabla ya matokeo hayo.

Pili, Shirika la Viwango nchini halifanyi ufuatiliaji yakinifu wa bidhaa zilizoruhusiwa kutoka bandarini na mipakani kwa masharti.

Tatu, Shirika la Viwango nchini halina mfumo madhubuti wa kuthibitisha kama bidhaa iliyopimwa ni ileile iliyoruhusiwa kutoka kwa masharti. Hii ni kwa sababu bidhaa husika huachwa mikononi mwa mwenye bidhaa wakati uchunguzi zaidi juu ya ubora wa bidhaa hiyo ukiendelea.

Yafuatayo ni mambo yaliyosababisha ukaguzi wa bidhaa zinazoingia nchini usiwe na ubora unaotakiwa:

- Ukosefu wa mipango inayohusisha vihatarishi wakati wa kufanya ukaguzi;
- Ukaguzi haufanyiki katika maeneo mengi ya mipaka inayotumika kuingiza bidhaa nchini kwa sababu ya uhaba wa wakaguzi wa ubora wa bidhaa;
- Kutokuwa na mifumo madhubuti za kudhibiti wanaokiuka Sheria Na. 2 ya Viwango ya mwaka 2009.
- Uratibu na ushirikiano usioridhisha baina ya taasisi mbalimbali za kiserikali kama vile Mamlaka ya Mapato nchini, Mamlaka ya Chakula na Madawa nchini n.k.

3.4.5 Utoaji wa Taarifa Usioridhisha katika masuala ya Ukaguzi wa bidhaa zinazoingia nchini

Kuna utoaji wa taarifa usioridhisha kutoka Shirika la Viwango nchini na Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusiana na ufanisi wa kaguzi za ubora wa bidhaa zinazoingia nchini. Changamoto na matatizo ambayo wakaguzi hao walikumbana nayo hayakuainishwa hivyo hakuna hatua zilizochukuliwa katika kuboresha ufanisi wa utendaji kazi wa Wakaguzi wa ubora wa bidhaa nchini.

Ukaguzi uligundua kuwa, kwa TBS, haikuwa na aina moja inayofanana ya kuandaa ripoti ya ukaguzi. Hali hii imepelekea wakaguzi wa ubora wa bidhaa kutokuwa na mfumo mmoja wa taarifa wenye vigezo vinavyofanana.

Ukosefu wa miongozo kwa ajili ya maandalizi na kuandaa ripoti ya ukaguzi wa kila mwezi

Hakukuwa na miongozo kwa ajili ya kuandaa ripoti ya ukaguzi za kila mwezi. Ripoti za mwezi ziliandaliwa na wakaguzi kwa kutoa muhtasari wa nyaraka zote za ukaguzi. Mihtasari hiyo ilipelekwa makao makuu kwa ajili ya kutengeneza muhtasari wa ujumla.

Ripoti nyingi za ukaguzi za mwezi zilionekana kuwa na matatizo yafuatayo: hazikuwa sahihi, hazikukamilika, na hazikuwa za uhakika. Tofauti ilijionesha katika nyaraka za uthibitisho, rejesta,

na taarifa zilizopatikana kutoka nyaraka hizo na zile za ukaguzi wa mwezi ambapo hazikuoana.

Kwa hiyo, maamuzi mbalimbali ya kiutendaji juu ya ukaguzi wa ubora wa bidhaa yalifanywa kwa kutegemea taarifa hizo zilizokuwa na mapungufu hayo na hivyo kushindwa kuleta ufanisi katika udhibidi bidhaa hafifu zisiingie nchini.

3.4.6 Ufuatiliaji hafifu na tathmini duni ya utendaji kazi wa kaguzi wa bidhaa

TBS inavyofuatilia na kutathmini shughuli za ukaguzi

Kurugenzi ya Ubora wa bidhaa haikuandaa mwongozo wa ufuatiliaji wa utendaji kazi wa kaguzi za ubora wa bidhaa unaofanywa na wakaguzi wa TBS. Taratibu za ufuatiliaji zilitakiwa kutoa mwongozo wa jinsi gani ufanisi wa kaguzi za ubora wa bidhaa utafuatiliwa.

Kwa upande mwingine, mapitio ya rekodi za ufuatiliaji za Kurugenzi na kwa kumbukumbu za kwenye mafaili kuhusu hatua zilizochukuliwa ilionyesha kwamba, ufuatiliaji wa ndani unafanyika bila kuwepo kwa viashiria vya ufanisi.

Ukaguzi ulibainisha ya kuwa Shirika la Viwango nchini halikuwa linafanya ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara juu ya ukaguzi wa ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini. Kwahiyo, Shirika lilishindwa kupata picha nzima ya utendaji katika eneo hili la ukaguzi wa ubora wa bidhaa na hivyo hakukuwa na mikakati iliyowekwa ili kuboresha ukaguzi wa bidhaa kutoka nje ya nchi.

Sababu kuu mbili zilizoainishwa na timu ya ukaguzi ambazo zilichangia kukosekana kwa umakini wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa kaguzi za ubora wa bidhaa nchini ni pamoja na:

- Mosi, ukosefu wa viashiria vya ufuatiliaji wa utendaji kazi ambavyo vingelenga kutathmini ni kwa kiasi gani malengo ya kaguzi za ubora wa bidhaa yanafikiwa; na
- Pili, ukosefu wa mwongozo na utaratibu wa ufuatiliaji wa shughuli za ukaguzi wa ubora wa bidhaa ambao ungetoa mwongozo wa namna ya ufuatiliaji wa shughuli hizo.

Ufuatiliaji na tathmini ya Kaguzi za Ubora wa Bidhaa

Mapitio ya Mpango Mkakati wa mwaka (2011/12 mpaka 2015/16) wa Wizara ya Viwanda na Biashara yalionyesha ya kwamba Wizara hiyo haijaweka viashiria vitakavyotumika kwa ajili ya kutathmini utendaji kazi wa Shirika la Viwango Tanzania juu ya ukaguzi wa ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini.

Kupitia mahojiano yaliyofanywa na watendaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara, ilibainika ya kuwa, Wizara haikufanya vya kutosha kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa kaguzi za ubora wa bidhaa zinazofanywa na Shirika la Viwango Tanzania.

Sababu zilizotajwa na watendaji wa Wizara kuhusu kutokufanyika kwa ufuatiliaji na tathmini wa kazi hizo za Shirika la Viwango Tanzania ni pamoja na Wizara ilikuwa haijaandaa mwongozo wowote wa kuongoza watendaji wake kufanya kazi hiyo ya kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa kaguzi za ubora wa bidhaa. Vilevile, ilibainika ya kwamba kwa sasa Wizara imeanza kuandaa vigezo hivyo.

Timu ya ukaguzi ilibaini athari kubwa mbili za Wizara kushindwa kufuatilia na kutathmini ubora wa utekelezaji wa kaguzi za bidhaa zinazofanywa na Shirika la Viwango nchini ambayo ni pamoja na:

(1) Wizara ilikosa uwezo wa kujua na kuelewa changamoto zilizoonekana na matatizo yanayowakabili watendaji wa TBS na waagizaji wa bidhaa nchini; na

(2) Wizara ilikosa takwimu za uhakika na taarifa za ufanisi ambazo zingeweza kutumika kama msingi wa kuboresha utendaji wa Shirika la Viwango nchini (TBS).

3.5 Hitimisho

Kwa ujumla, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inahitimisha kuwa kaguzi za ubora wa bidhaa zinazoingia nchini hazikufanyika vizuri na vya kutosha kwa sababu hazikupangwa vizuri, hazikuwa na malengo yanayoeleweka, hakukuwa na mikakati madhubuti ya ufanyaji wa

kaguzi hizo ambazo zingesaidia lengo kuu la kupunguza bidhaa hafifu zinazoingia nchini. Kutokuwa na vigezo vilivyotajwa hapo juu ambavyo ni vya muhimu kama sehemu ya mwongozo wa utendaji wa shughuli za ukaguzi wa ubora wa bidhaa nchini ilifanya kazi hiyo ya ukaguzi kuwa ngumu kwa Shirika la Viwango Tanzania na hivyo kushindwa kufikia lengo tajwa hapo juu.

Usimamizi wa ukaguzi wa bidhaa kutoka nje ya nchi haukufanywa kwa kuzingatia viashiria hatarishi. Bidhaa zote zilipewa kipaumbele sawawakati wa ukaguzi licha ya ukweli kwamba baadhi ya bidhaa zinajulikana kuwa na athari kubwa kwa afya na mazingira ya walaji nchini.

Kutokuzingatia vigezo/viashiria hatarishi wakati wa kaguzi za bidhaa (hasawakati wa kupanga shughuli za ukaguzi) kumeathiri ufanisi wa Shirika la Viwango Tanzania katika kaguzi zake. Hii ni pamoja na rasilimali chache zilizotengwa kwa ajili ya shughuli zaukaguzi wa bidhaa kutumika katika kaguzi hizo na zaidi katika bidhaa ambazo zingeweza kupewa kipaumbele cha chini.

Kwa upande mwingine, ufuatiliaji na tathmini ya mfumo wa ndani ya Shirika la Viwango Tanzaniapia haufanyi kazi. Hakuna ushahidi unao onyesha ya kuwa matokeo ya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za ukaguzi wa ubora wa bidhaa zimetumika ili kuboresha utendaji wake.

3.6 Mapendekezo ya Ukaguzi

3.5.1 Mapendekezo kwa Shirika la Viwango nchini

Shirika la Viwango Tanzania linashauriwa kufanya yafuatayo:

a) lihakikishe lina kuwa na mfumo imara wa kutunza taarifa na takwimu zenye maelezo kuhusu aina ya bidhaa zinazotarajia kuingizwa nchini kwa kuzingatia vihatarishi, ili kurahisisha ukaguzi wa bidhaa hizo;
b) kuandaa mkakati kwa ajili ya bidhaa zinazoingizwa nchini kwa kuzingatia vihatarishi husika. Mkakati huo uweze kutoa kipaumbele katika kaguzi za bidhaa hizo ambazo zinaonekana kama zitakuwa ni hafifu na athari yake kwa afya na mazingira itakuwa ni kubwa;
c) kuhakikisha ya kwamba inapata taarifa ya bidhaa zinazotarajiwa kuingizwa nchini kutoka Mamlaka ya Mapato nchini na kutumia taarifa hizo ili kuweza kuboresha kaguzi zake za bidhaa zinazoingia nchini;

d) lianzishe mfumo madhubuti wa ufuatiliaji wa kaguzi zake ili kuhakikisha ya kuwa kaguzi zinafanyika kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa; na

e) lihakikishe ya kuwa kuna sera na miongozo ya ubora ya kutumia wakati wa kuandaa ripoti za ukaguzi wa ubora wa bidhaa.

3.5.2 Mapendekezo kwa Wizara ya Viwanda na Biashara

Wizara ya Viwanda na Biashara inashauriwa kufanya yafuatayo:

a) kuandaa mfumo madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini ambao utaruhusu ufuatiliaji wa utekelezaji wa kaguzi za ubora wa bidhaa ili kuweza kufikia malengo yaliyowekwa katika ukaguzi wa bidhaa zinazoingia Tanzania;

b) kuandaa viashiria vya ufanisi katika masuala ya ukaguzi wa bidhaa zinazoingia nchini ambavyo vitatumika kupima utekelezaji wa mipango muda mfupi na mrefu ya ukaguzi wa ubora wa bidhaa zinazoingia nchini;

c) kuandaa njia madhubuti za kusimamia taarifa/takwimu zinazohusiana na ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini na kuwa na mfumo mzuri wa kupeana taarifa baina ya taasisi

mbalimbali za serikali ambazo zina mamlaka ya kuidhinisha uingiaji wa bidhaa mbalimbali nchini; na

d) **kuandaa mfumo wa ushirikiano kati ya Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Polisi na Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Shirika la Viwango nchini katika kudhibiti uingizaji wa bidhaa katika mipaka isiyo rasmi.**

SURA YA NNE

UKAGUZI WA UFANISI KATIKA USIMAMISI WA UKAGUZI WA CHAKULA

4.1 Utangulizi

Sekta imara na yenye ubora wa chakula inatarajiwa kutoa nafasi kwa walaji kuweza kupata lishe bora na yenye virutubisho vyote vya msingi kwa taifa zima. Vilevile, kama sekta haisimamiwi kwa ufanisi unaotakiwa basi inaweza kuwa chanzo kikubwa cha magonjwa mbalimbali kwa wananchi na hivyo kuleta hasara kubwa haswa kutokana na vifo na upotevu wa muda kwa wale watakao shindwa kuzalisha na kuwabidi waende hospitali.

Mamlaka ya Chakula na Dawa nchini (TFDA) ilianzishwa baada ya kuunganishwa kwa iliyokuwa Bodi ya Famasi na Kamisheni ya Chakula Tanzania. Hii ilikuwa baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003. Mamlaka hii inafanya kazi zake chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na inajukumu la kusimamia ubora wa Madawa, Vipodozi, Chakula na vifaa tiba.

Vilevile, jukumu la kuhakikisha ya kwamba chakula kinachoingia na kutoka nje na kile kinachozalishwa nchini ni salama kwa watumiaji ni la Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA). Kutekeleza jukumu hilo, Mamlaka ya Chakula na Dawa hufanya kaguzi za ubora wa chakula kinachoingizwa nchini kupitia mipaka yetu na pia kile kinachozalishwa au kusindikwa na viwanda vilivyopo nchini.

4.2 Tulichokichunguza katika ukaguzi wa chakula

Ukaguzi ulitaka kujua kama Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) inatimiza dhamira yake ya kulinda ubora wa chakula nchini. Ukaguzi ulijikita katika mipango, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa ubora wa chakula katika viwanda vinavyosindika chakula na katika mipaka inayotumika kuingiza chakula nchini.

Malengo makuu ya ukaguzi yalikuwa ni kuangalia kama:

- **TFDA ina mipango inayozingatia vihatarishi kwa ajili ya ukaguzi wa viwanda vinavyosindika chakula na bandari zinazotumika kuingiza chakula nchini; na kama rasilimali zinatengwa katika maeneo yenye umuhimu mkubwa zaidi;**
- **TFDA inafanya ukaguzi na ufuatiliaji wa viwanda vinavyosindika chakula na bandari zinazotumika kuingiza chakula nchinikwa kuzingatia vihatarishi juu ya usalama wa chakula hicho na afya ya mlaji; na**
- **TFDA inafanya ufuatiliaji na tathmini ya zoezi la ukaguzi wa viwanda vinavyosindika chakula na kuingiza chakula nchini na kutumia taarifa hizo kuboresha ukaguzi huo.**

Ukaguzi ulihusisha ofisi tano za kanda ambazo ni kanda ya Kaskazini, Mashariki, Nyanda za Juu-Kusini, Kati na Ziwa. Ambapo ukaguzi wa ubora wa chakula hufanywa na wakaguzi waliopo katika kanda hizo. Wakaguzi waliopo katika kanda hizo ndio ambao wanahusika na kufanyika katika viwanda vya kusindika chakula na mipakani. TFDA inafanya aina mbalimbali za kaguzi za ubora wa chakula ikiwa ni pamoja na: ukaguzi wa kiuchunguzi, ukaguzi fuatilizi, ukaguzi maalum, ukaguzi wa mara kwa mara. Lakini ukaguzi huu ulijikita zaidi katika ukaguzi wa mara kwa mara ambao ni mkubwa kuliko kaguzi zingine ndani ya TFDA.

Ili kupata mwenendo wa utendaji kazi wa TFDA na kuwa na hitimisho imara, ukaguzi ulijikita hasa katika mwaka wa fedha wa 2009/10 hadi 2012/13.

4.3 Sababu zilizopelekea kuchunguza ukaguzi chakula

Kumekuwa na kilio kwa umma juu ya uwepo wa bidhaa za chakula ambazo si salama kwa matumizi ya binadamu. Baadhi ya mifano na matukio ya maziwa ya watoto wachanga yasiyo salama, uwepo wa nyama isiyo salama kutokana na kuwa na machinjio yasiyo salama, na ukamatwaji na kutolewa sokoni kwa samaki aina ya vibua walioingizwa nchini kutoka nje ya nchi wakiwa tayari wameharibika.

Shirika la Afya Duniani (WHO) katika kanuni zake kumi kuhusu usalama wa chakula linathibitisha kwamba magonjwa zaidi ya 200 duniani yanaenezwa kwa njia ya matumizi ya chakula kisicho salama. Asilimia 75 magonjwa mapya yaliyoathiri binadamu katika kipindi cha miaka 10 yalisababishwa na bakteria, virusi na vimelea wengine ambao walianzia katika wanyama na bidhaa za wanyama. Inakadiriwa kuwa theluthi moja ya wakazi wa nchi zilizoendelea wanaathiriwa na magonjwa yatokanayo na chakula kila mwaka, na kuna uwezekano kuwa tatizo ni kubwa na limeenea zaidi katika nchi zinazoendelea.

Utafiti wa majaribio juu ya tathmini ya magonjwa yanayo sababishwa na chakula uliofanywa na Mamlaka ya Chakula na Dawa nchini katika mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara ulibaini ya kuwa kumekuwa na matukio ya vifo vinavyotokana na kula chakula kisicho salama ambacho kiliathiri watu zaidi ya 1,000 katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Ilibainika kuwa magonjwa yatokanayo na chakula huathiri uwezekano wa watanzania kutekeleza shughuli zao za kila siku za kiuchumi. Pia unaathiri uwezo wa Serikali kufikia malengo yake ya kimkakati ya maendeleo, kwa jamii na nchi kwa ujumla.

Ukaguzi wa ubora wa chakula ni muhimu kwa Serikali katika kuhakikisha kuwa chakula kinachoingizwa na kuzalishwa nchini kina ubora na ni salama kwa matumizi ya walaji. Hii inapelekea Mamlaka ya Chakula na Dawa kutimiza majukumu yake kwa ufanisi na tija.

4.4 Matokeo ya Ukaguzi

4.4.1 Mipango ya Ukaguzi wa Chakula Isiyojitosheleza

Kwa mujibu wa Mwongozo wa ukaguzi wa Shirika la Chakula duniani (FAO) mamlaka kama TFDA zinatakiwa kuwa na mipango ya ukaguzi wa chakula. Pia mamlaka zinatakiwa kuwa na mipango ya kudhibiti ubora wa kaguzi, kuamua juu ya aina ya ukaguzi, ratiba ya kaguzi hizo na kusimamia wakaguzi ili kuongeza tija na ufanisi na kupunguza uwezekano wa kujihusisha na tabia zinazokiuka maadili ya kazi.

Tuligundua kuwa mipango ya TFDA ya ukaguzi wa chakula:

Haikuwa na sifa za msingi za ukaguzi unaozingatia viashiria vya udhaifu katika usalama wa chakula

Ukaguzi umegundua kwamba mipango ya ukaguzi wa chakula wa TFDA haikuwa na vipengele muhimu ambavyo ni pamoja na idadi ya kaguzi zilizokuwa zimepangwa kufanyika, idadi ya wakaguzi, utaratibu wa usimamizi na ufuatiliaji na usimamizi wa utendaji kazi za ukaguzi wa ubora wa chakula.

Kwa mfano, TFDA hawakuwa na idadi ya kaguzi ambazo zilitakiwa kufanyika katika kipindi fulani cha mwaka, mara ngapi ukaguzi ufanyike, kiasi cha ukaguzi na sababu nyingine kama vile ukaguzi fuatilizi wa viwanda vinavyo sindika chakula ambavyo vina ukiukwaji mkubwa wa matakwa na kanuni za uzalishaji chakula salama, ratiba ya ukaguzi huo na jinsi ya kushugulikia malalamiko ya wananchi.

Mipango ya utendaji kazi katika ofisi za TFDA kanda haikuweka malengo ya ukaguzi kwa vipindi vifupi vifupi na wala haikuonesha ni wakati gani ukaguzi huo ulitarajiwa kufanyika. Aidha ukaguzi ulibaini kuwa mipango ya kaguzi ilikuwa kimya juu ya suala la kusimamia na kufuatilia matokeo ya kaguzi za usalama wa chakula. Ukaguzi ulibaini kwamba TFDA haikua na mipango kwa ajili ya utendaji (katika suala la matokeo na ukaguzi wenye tija), kuwa na viashiria vya kupima utendaji kazi, kuwa na ratiba ya ukaguzi, kufuatilia utendaji ili kuona kama malengo yanafikiwa, na kuboresha iwapo utendaji haukufikia malengo yaliyowekwa kwa mwaka.

Kutokua na vipaumbele vya ukaguzi wa usalama wa chakula

Wkaguzi walifanya uchambuzi wa kiwango cha kipaumbele cha ukaguzi kwa viwanda vya kusindika chakula na bandari zinazotumika kuingiza chakula nchini ambayo ni hatarishi. Jedwali 4.1 linatoa uchambuzi wa uhusiano wa bidhaa hatarishi za chakula, viwanda hatarishi vya kusindika chakula na mzunguko wa ukaguzi uliofanywa katika viwanda hivyo vya kusindika chakula kwa mwaka wa fedha 2012/13.

Jedwali 4.1: Kipaumbele cha ukaguzi wa usalama wa chakula katika viwanda vya kusindika chakula (2012/13)

Orodha ya bidhaa hatarishi za chakula	Idadi ya viwanda hatarishi vya usindikaji wa chakula	Kiasi (idadi) ya ukaguzi (kubwa, kiasi, ndogo)
Nyama	1	Haijatajwa
Nyama na bidhaa za nyama	11	Haijatajwa
Usindikaji nyama	1	Haijatajwa
Maziwa na bidhaa za maziwa	11	Haijatajwa
Samaki na Bidhaa za samaki	10	Haijatajwa

Chanzo: Mwongozo wa maombi na usajili wa chakula na takwimu ya TFD juu ya viwanda hatarishi vya kusindika chakula

Kwa ujumla, ilibainika kuwa kwa sababu TFDA imeshindwa kuwa na rekodi (takwimu) za utekelezaji na ukiukwaji wa kanuni na matakwa ya usalama wa chakula unaofanywa na viwanda vya kusindikaji chakula ilipelekea kwa wakaguzi wa TFDA kujaribu kufanya ukaguzi katika viwanda vyote vinavyosindika chakula katika ofisi zake za kanda. Hii ilipelekea TFDA kuwa katika hatari ya kushindwa kutoa kipaumbele kwa ukaguzi wake katika viwanda hatarishi vya usindikaji wa chakula.

Mambo yanayochangia kuwa na mipango isiyofaa ya ukaguzi wa usalama wa chakula

Zifuatazo zilikuwa ni sababu kubwa zilizopelekea kuwa na mipango isiyofaa ya ukaguzi wa usalama wa chakula katika viwanda vya kusindika chakula na mipakani:

- Kutokufanyika kwa uchambuzi wa vihatarishi na kushindwa kuanzisha rekodi (takwimu) ya utekelezaji na ukiukwaji wa kanuni na matakwa ya usalama wa chakula unaofanywa na viwanda vya kusindika chakulana waagizaji wa chakula nchini;

- **Kutotumika kwa mwongozo wa ukaguzi unaozingatia vihatarishiwakati kanda zikipanga ukaguzi wa chakula;**
- **Uongozi wa TFDA haukutoa mwongozo wowote/maelekezo ya kuwaongoza wakaguzi wake juu ya jinsi gani wanaweza kutumia miongozo mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yao;**
- **Mapungufu katika kuratibu kazi za ukaguzi wa usalama wa chakula. Uratibu huu unawahusisha wakaguzi, ofisi za kanda, watathmini wa vihatarishi nakitengo cha mipango kutoka TFDA wakati wa kupanga mipango ya ukaguzi wa chakula; na**
- **Wakaguzi kutokuwa na mafunzo ya jinsi ya kufanya ukaguzi unaozingatia vihatarishi.**

4.4.2 Mapungufu ya kiutendaji katika ukaguzi wa chakula

Katika Viwanda vya Kusindika Chakula

Mapitio ya mipango ya utendaji kazi ya kila mwaka yalionyesha kuwa kulikuwa hakuna hatua za kiutendaji zilizopangwa kufikiwa kwa kipindi kizima cha mwaka, idadi ya viwanda vya kusindika chakula vitakavyokaguliwa kwa kipindi hicho cha mwaka, makadirio ya muda wa ukaguzi na hata rasilimali ambazo zingetumika katika ukaguzi huo. Mahojiano yetu na ofisi za TFDA-kanda yalibainisha kuwa walijaribu kukagua viwanda vyote vya usindikaji wa chakula angalau mara moja kila mwaka.

Jedwali 4.2 chini linatoa uchambuzi wa idadi ya kaguzi zilizofanywa kwa mwaka dhidi ya idadi ya kaguzi zilizopangwa (hii ni sawa na idadi ya viwanda vya usindikaji wa chakula vilivyosajiliwa katika eneo husika.

Jedwali 4.2: Asilimia ya viwanda vya usindikaji chakula vilivyokaguliwa kwa mwaka (2012/13)

Kanda	Idadi ya viwanda vya kusindika chakula vilivyopangwa kukaguliwa	Idadi ya viwanda vilivyokaguliwa	Asilimia ya viwanda vilivyokukaguliwa (%)
Kasikazini	100	90	90
Mashariki	200	285	143
Nyanda za Juu Kusini	40	77	193
Kati	50	26	52
Ziwa	80	38	48

Chanzo: *TASA na ripoti za kila mwaka za ofisi za kanda*

Jedwali 4.2 linaonyesha kwamba kanda mbili zilizidi idadi ya kaguzi ilizojipangia wakati kanda nyingine tatu zilishindwa kukagua viwanda vyote vya usindikaji wa chakula katika maeneo yao. Pia takwimu zinaonyesha kuwa katika Kanda ya Ziwa, ukaguzi ulikua chini ya asilimia hamsini. Hii ina maana kwamba karibu nusu ya viwanda vya kusindika chakula katika eneo hilo havikukaguliwa licha ya ukweli kwamba TFDA ilikua na nia ya kuvikagua viwanda hivyo.

Ukaguzi kutokufanyika katika viwanda hatarishi vya kusindika chakula

Ukaguzi umegundua kwamba TFDA haikutoa kipaumbele cha kukagua maeneo hatarishi katika viwanda vya usindikaji wa chakula. Msingi wa kuamua idadi na aina gani ya viwanda vya usindikaji yapewe kipaumbele haukuanishwa popote bali lengo lilikua kutembelea viwanda vyote bila kujali kiwango

cha hatari ya usalama wa chakula inayoweza kusababababishwa na baadhi ya viwanda.

Vilevile, mahojiano baina ya Ofisi ya Ukaguzi wa Hesabu na wakaguzi wa usalama wa chakula yalithibitisha kuwa TFDA haikufanikiwa kufanya ukaguzi wa chakula katika viwanda vyote vya usindikaji wa chakula na pia haikuweza kujua kama viwanda vya kusindika chakula ambavyo havikukaguliwa vilikua vile vinavyohatarisha usalama wa chakula kwa kiasi kikubwa. Hii ni licha ya ukweli kwamba Mwongozo wa maombi na usajili wa chakula umeorodhesha aina ya chakula ambavyo kwa uasilia wake ni hatari kwa usalama wa afya ya binadamu.

Ukaguzi uliweza kubaini kwamba licha ya ukweli kwamba ukaguzi katika ofisi za TFDA za kanda hufanyika katika viwanda vyote viwe vile vyenye uhatarishi wa juu, kiasi au chini, ukaguzi huo haukuwa na uwezo wa kuvifikia viwanda vyote vya usindikaji wa chakula, na hili lilionekana katika ofisi zote tano za kanda. Taswira hii inaelezwa vizuri katika jedwali 4.3.

Jedwali 4.3: Idadi ya viwanda hatarishi vya usikaji wa chakula vilivyofikiwa na wakaguzi (2012/13)

Kanda	Idadi ya Viwanda vilivyokaguliwa	Idadi ya viwanda hatarishi vilivyopo	Idadi ya viwanda hatarishi vilivyokaguliwa
Kasikazini	90	8	TFDA Haikuwa na rekodi yake
Mashariki	285	12	TFDA Haikuwa na rekodi yake
Nyanda za Juu Kusini	77	2	TFDA Haikuwa na rekodi yake
Kati	26	2	TFDA Haikuwa na rekodi yake
Ziwa	38	10	TFDA Haikuwa na rekodi yake

***Chanzo:** Ripoti za Kila mwaka za ofisi za TFDA Kanda*

Jedwali 4.3 hapo juu linaonyesha kwamba ukaguzi uliofanywa na TFDA kwa viwanda vya kusindika chakula haukuweza kuvifikia viwanda hatarishi vinavyozalisha chakula visivyofaa kwa matumizi ya binadamu.

Ukaguzi wetu ulitaka kujua sababu zilizopelekea kutoanishwa kwa viwanda vilivyoko katika hatari ya kuzalisha chakula kisichofaa

kwa matumizi ya binadamu na kuvikagua kwa misingi ya kiasi cha vihatarishi na kubaini sababu zifuatazo:

- Kutotumika kwa mwongozo wa ukaguzi unaofuata misingi ya vihatarishi wakati wa ukaguzi;
- Kushindwa kufanya marejeo ya ukaguzi uliopita ambapo kungesaidia wakaguzikutambua maeneo hatarishi; na
- Kushindwa kuandaa rekodi (takwimu) ya utekelezaji na ukiukwaji wa kanuni na matakwa ya usalama wa chakula unaofanywa na viwanda vya kusindikaji chakula

Sababu zilizochangia kuwa na mapungufu katika ukaguzi wa chakula

Zifuatazo ni sababu kuu zilizochangia kuwa na mapungufu katika ukaguzi wa viwanda vinavyosindika chakula:

- Ufahamu juu ya aina ya ukaguzi unaotakiwa kufanyika;
- Mapungufu katika mipango ya ukaguzi wa usalama wa chakula;
- Mapungufu katika matumizi ya rasilimali katika ukaguzi wa usalama wa chakula (watu, fedha na zana ukaguzi); na
- Orodha ya ukaguzi kutokua na masuala muhimu kuhusu ukaguzi wa chakula.

4.4.3 Mapungufu katika Ukaguzi wa Usalama wa Chakula Katika Mipaka rasmi ya kuingiza na kusafirisha chakula nje ya nchi

Ukaguzi haukufanyika kwa bidhaa za chakula ambazo kiasili zinaweza kuwa ni hatarishi

Mapitio ya ripoti za ukaguzi zinazoandaliwa na wakaguzi wa chakula mipakani zilionyesha kuwa TFDA ilikuwa ikijaribu kukagua kila mzigo wa chakula ulioingia nchini. Hii ina maana kwamba mizigo yote ya chakula ilipewa kipaumbele sawa wakati wa ukaguzi bila kujali kama chakula hicho kiasili ni hatari au si hatari.

Matokeo yake TFDA ilishindwa kukagua mizigo yote kwa ufanisi na hivyo kupelekea baadhi ya mizigo ya chakula kuingia nchini bila kukaguliwa. Hali hii wakaguzi walikutana nayo katika bandari ya Dar es Salaam ambapo wakaguzi waligundua kwamba si kila mzigo wa chakula uingiao nchini hukaguliwa kabla ya kuondolewa katika eneo la forodha.

Aidha, wakaguzi walipitia takwimu ya uingizaji chakula kutoka bandari ya Dar es Salaam katika kituo cha ukaguzi wa pamoja "One Stop Centre" na kukuta kwamba kulikuwa na mizigo ya chakula iliyoondolewa bandarini bila kukaguliwa. Hii ilikuwa ni kinyume na matakwa ya lazima ya kukagua kila chakula kiingiacho nchini kabla ya kuondolewa bandari.

Aidha, takwimu ya uingizaji chakula za mwaka 2012 zilionyesha ya kwamba asilimia 90 ya mizigo 311 ya chakula ilikuwa bado haijakaguliwa kwa zaidi ya mwaka mmoja licha yakuondolewa bandarini kwa masharti ya kukaguliwa hapo baadaye. Hii inaoneshwa kwenye kielelezo 4.1.



Kielelezo 4.1: Kiasi cha mizigo ya chakula iliyokaguliwa na ambayo haikukaguliwa katika bandari ya Dar es Salaam.

Chanzo: Takwimu za uingizaji chakula nchini kituo cha ukaguzi wa pamoja "One Stop Centre" bandari ya Dar es Salaam.

Aidha, mambo mengine mawili makubwa yaliyochangia kutokaguliwa kwa chakula kiingiacho nchini kupitia mipakani ni pamoja na:

a) "Mizigo midogo" kupita mipakani bila kukaguliwa; na

b) Kuruhusiwa kwa bidhaa ambazo hasijasajiliwa na TFDA kuingia nchini.

Sababu zilizopelekea kuwa na mapungufu ya ukaguzi wa bidhaa za chakula kutoka nje ya nchi

Ukaguzi umegundua sababu ambazo zilichangia ukaguzi wa bidhaa za chakula kutokuwa wa kuridhisha zilisababishwa na:

- Mapungufu katika mipango ya ukaguzi wa usalama wa chakula mipakani;
- Ukosefu wa kumbukumbu au taarifa ya bidhaa za chakula kutoka nje ya nchi;
- Ufuatiliaji mdogo na usiojitosheleza wa shughuli za ukaguzi wa usalama wa chakula uliofanywa mipakani; na
- Kutokua na vipaumbele katika ukaguzi wa usalama wa chakula kutoka nje.

4.4.4 Kiwango cha chini cha matumizi ya sheria na matakwa ya uzalishaji na uingizaji chakula nchini

TFDA kushindwa kutumia matakwa ya sheria juu ya viwanda vilivyokuwa havifuati matakwa hayo

Utekelezaji wa sheria wa TFDA kwa njia ya ukaguzi na ufuatiliaji ulishindwa kuzuia viwanda vya usindikaji wa chakula kuvunja sheria mara kwa mara. Katika mwaka wa fedha wa 2009/10 hadi 2012/13, asilimia 80 ya viwanda vilivyokuwa vimekiuka sheria, matakwa na kanuni za uzalishaji wa chakula havikuchukuliwa hatua zilizoainishwa kwenye sheria ingawa baadhi ya viwanda hivyo vilikiuka matakwa hayo zaidi ya mara moja.

Hii ilitokea kwa sababu TFDA haikuwa:

(1) ikichukua hatua kali za utekelezaji dhidi ya wakiukaji wanaojirudia rudia;

(2) ikitofautisha kati ya ukiukwaji mkubwa na mdogo kwenye rekodi zake; na

(3) ikitoa miongozo ya kutosha juu ya hatua gani za kuchukua iwapo kuna ukiukwaji fulani. Matokeo yake, viwanda vimekuwa vikirudia rudia kukiuka kanuni bila kuchukuliwa hatua kali zaidi.

Aidha, ilibainika kuwa licha ya ukweli kwamba kuna kutofuatwa na ukiukwaji mkubwa wa kanuni unaofanywa na viwanda vya usindikaji wa chakula na waagizaji wa chakula nchini, TFDA bado imendelea kutokuweka kumbukumbu za ukiukwaji huo vizuri na kuzitumia kuboresha utendaji wake wa kazi.

Maofisa wa TFDA walieleza kuwa kumbukumbu za ukiukwaji wa kanuni ziligusa sana viwanda vya usindikaji wa chakula mbavyo vimekua mara mara vikikiuka kanuni hizo. Bila kuwa na motisha zaidi ya kutekeleza na kufuata kanuni viwanda vya usindikaji chakula vipo katika hatari kubwa ya kuzalisha na kusambaza chakula kisichofaa kwa matumizi ya binadamu.

4.4.5 Ripoti juu ya matokeo ya ukaguzi wa usalama wa chakula

Ukaguzi ulipitia ripoti za utendaji kazi ili kutathmini kiasi na aina ya mapungufu yaliyoelezwa na wakaguzi wa usalama wa chakula na kama ripoti hizo ziliwasilishwa kwa wakati.

Ripoti za ukaguzi wa usalama wa chakula kutotumika vya kutosha

Ukaguzi ulibainisha kuwa wakaguzi wa TFDA hutayarisha ripoti za ukaguzi kupitia fomu za ukaguzi "memorandum of inspection" na baadaye mapendekezo na maelekezo yaliyotelewa katika ukaguzi huo kuwekwa katika rejista ya ukaguzi.

Uchambuzi zaidi wa ripoti za ukaguzi zilizopo kwenye fomu ya ukaguzi na zile zilizopo kwenye rejista ulionyesha kuwa na mapungufu yafuatayo:

- fomu ya ukaguzi kutoruhusu wakaguzi kutoa maoni juu ya ukaguzi uliopita na maelekezo aliyopewa mmiliki wa kiwanda cha usindikaji wa chakula
- rejista ya ukaguzi kutokuonyesha idadi ya maelekezo ya awali yaliyotekelezwa kwa kiasi gani na hatua gani zilihitajika kuchukuliwa kwa ajili ya kaguzi fuatilizi

Kutochunguzwa kwa ripoti za ukaguzi wa chakula unaofanywa na Serikali za Mitaa

Ukaguzi uligundua kwamba ofisi za kanda za TFDA zilikuwa hazichambui ripoti za ukaguzi wa usalama wa chakula zilizowasilishwa na Serikali za Mitaa ili kuona mapungufu yaliyoainishwa katika kaguzi hizo. Hii ni kinyume na matakwa yaliyowekwa na Mwongozo wa ufanisi na uendeshaji wenye tija wa ofisi za TFDA kanda.

Mapitio ya ripoti za mwaka kutoka ofisi tano za TFDA kanda ilionyesha kuwa ofisi za kanda ya kati na nyanda za juu kusini ndizo zilijaribu kujumuisha ripoti za ukaguzi wa chakula kutoka Serikali za Mitaa pekee.

Kuratibu ukaguzi wa chakula na idara nyingine za serikali

Kwa mujibu wa kifungu cha 5 (2) (f) cha sheria ya TFDA, TFDA inatakiwa kufanya kazi na idara nyingine za serikali ili kufikia malengo yake katika ukaguzi wa usalama wa chakula viwandani na bandari za kuingiza bidhaa nchini.

Idara hizi nyingine za serikali ni pamoja na; Mamlaka ya Mapato Tanzania, Shirika la Viwango Tanzania, Shirika la Ushindani Sawa wa Kibiashara, Serikali za Mitaa, Bodi ya Maziwa, Bodi ya Nyama, Bodi ya Sukari, Wizara ya Mifugo na Uvuvi n.k.

Mapitio ya ripoti za mwaka za utendaji kazi pamoja na mahojiano na maofisa kutoka TFDA ulibainisha kuwa ingawa TFDA inaratibu ukaguzi wa chakula ikishirikiana na idara za serikali zilizotajwa hapo juu bado uratibu huo unaonyesha kuwa na mapugufu kadhaa kwa kuto kusimamiwa vya kutosha. Hii inathibitishwa kwa kuzingatia mambo makuu yafuatayo:

- TFDA na idara tajwa kushindwa kubadilishana takwimu zinazohusu ukaguzi wa usalama wa chakula;
- Ukosefu wa utaratibu wa wazi wa kupeana taarifa zinazohusu ukaguzi wa usalama wa chakula;
- Kutobadilishana matokeo ya ukaguzi wa usalama wa chakula; na
- Kutoainishwa kwa shughuli za ukaguzi katika bandari za kuingizia bidhaa za chakula

4.4.6 Udhaifu katika ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa chakula

Ukosefu wa viashiria vya ufuatiliaji na tathmini kwa ajili ukaguzi wa chakula

Kwa mujibu wa Shirika la Kimataifa la Viwango (ISO) 9001:2008 taasisi kama TFDA inatakiwa kuwa na malengo ya utendaji, kuwa na viashiria vya kupima utendaji kazi wake, kuandaa mpango kazi wa mwaka, na ratiba ya ukaguzi, kufuatilia utendaji dhidi ya malengo iliyojiwekea, na kurekebisha iwapo utendaji utagundulika kutofikiwa kwa malengo yaliyowekwa kwa mwaka husika.

Mahojiano na Maofisa Kitengo cha Usimamizi wa Ubora na kile cha Mipango ulibaini kuwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010 hadi 2010/2011, TFDA haikuwa ikifuatilia wala kutathmini shughuli za ukaguzi wa usalama wa chakula viwandani na bandari za kuingiza bidhaa nchini. Pia hakukuwa na viashiria vya ufuatiliaji na tathmini mahsusi kwa ajili ya ukaguzi wa chakula unaofanywa na wakaguzi wa TFDA. Hali hii ilibainika pia wakati wa kupitia mpango mkakati wa TFDA wa miaka mitano 2008/2009 hadi 20012/2013 na mwongozo wa ukaguzi unaozingatia misingi ya vitu hatarishi.

Hata hivyo mipango ya utendaji kazi ya mwaka 2012/13 imeonyesha kujumuisha viashiria vya ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa chakula. Japo haviwezi kupimwa vyenyewe mpaka vikilinganishwa na vipengele vingine vya matokeo tarajari. Mpango mkakati wa miaka mitatu wa TFDA unaoanzia mwaka 2012/13 pia umegundua mapungufu yaliyokuwepo katika mpango mkakati uliopita na kujumuisha viashiria hivyo.

4.5 Hitimisho la ukaguzi

Ilihitimishwa kuwa ukaguzi wa usalama wa chakula katika viwanda vya kusindika chakula na bandari za kuingiza bidhaa nchini haukujitosheleza. Hali hii ilisababishwa na kutokuwa na mipango madhubuti ya ukaguzi, malengo ya wazi, mikakati kwa ajili ya ukaguzi ili kufikia lengo kuu, na hatimaye lengo la kulinda ubora wa chakula katika nchini halikuweza kutimia. Kushindwa kuwa na mipango kazi na kuifuata wakati wa ukaguzi wa usalama wa chakula kwa kiasi kikubwa umechangia madhaifu yaliyoainishwa hapo juu.

Kaguzi za chakula zote mbili katika viwanda na bandari za kuingiza bidhaa nchini haukufanywa kwa kuzingatia vihatarishi mbali mbali vya uzalishaji wa chakula. Viwanda vyote vilipewa kipaumbele sawa wakati wa ukaguzi licha ya ukweli kwamba baadhi ya chakula au taratibu za uzalishaji wa chakula hicho unakifanya kuwa na viatarishi vingi zaidi kwa afya za watumiaji.

Kutokuzingatiwa kwa vihatarishi wakati wa ukaguzi, haswa wakati wa kuandaa mipango ya ukaguzi wa usalama wa chakula, kunaathiri ufanisi wa TFDA katika kutekeleza jukumu lake la kulinda usalama wa chakula nchini. Hii inathibitishwa na rasilimali chache zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za ukaguzi kupelekwa kwenye viwanda na bandari za kuingiza chakula nchini ambazo zingeweza kupewa uzito mdogo.

Kwa kuhitimisha, wakati mifumo ya kufuatilia utekelezaji wa matakwa ya sheria na kanuni inaruhusu kuchukua hatua kali dhidi ya wakiukaji wanao rurudiarudia, ni mara chache sana mamlaka imechukua hatua kali dhidi ya vitendo hivyo. Kwa kuwa hakuna hatua kali zilizochukuliwa dhidi ya viwanda vya kusindika chakula ambavyo mara kwa mara vimekiuka kanuni za usalama wa chakula, viwanda hivyo vimekosa motisha wa kuboresha utendaji kazi wao. Ukiukwaji mkubwa unaweza kuwa na madhara makubwa kwaafya ya mtumiaji. Kwa kuvisaidia viwanda vya kusindika chakula kutimizalengo hili, TFDA italihakikishia taifa kuwa biashara na usambazaji wa chakula nchini ni salama na safi. Kwa upande mwingine, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya utendaji kazi ndani ya TFDA unahitaji kufanyiwa marekebisho makubwa.

4.6 Mapendekezo ya Ukaguzi

4.6.1 Mapendekezo kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA)

Yafuatayo ni Mapendekezo kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania:

1. **TFDA ianzishe utaratibu wa kuweka takwimu za ukiukwaji na utekelezaji wa sheria na kanuni za viwanda vya kusindika chakula na waagizaji chakula ili kujua ni yupi anatekeleza na kwa kiasi gani ili kusaidia katika mipango ya ukaguzi na ukaguzi fuatilizi;**
2. **TFDA inapaswa kuhakikisha kuwa ofisi zote za kanda na bandari za kuingiza bidhaa nchini zinakuwa na mipango ya ukaguzi na itumike kama msingi wa kuwaongoza katika kaguzi zao. Vile vile, mipango hiyo lazima izingatie vihatarishi mbali mbali vya usalama wa chakula;**
3. **TFDA inapaswa kuanzisha vipimo vya hatua za utendaji kazi kwa ajili ya shughuli za ukaguzi wa chakula, ikiwa ni pamoja sera inyoongoza ukaguzi huo, na mambo mengine kama vile tathmini ya vihatarishi, muda, kazi ratiba n.k;**
4. **Mamlaka inapaswa kuanzisha taratibu za utoaji kipaumbele na kuhakikisha ukamilikaji kwa wakati, kaguzi zote za viwanda vya usindikaji wa chakula na bidhaa kutoka nje ya nchi;**
5. **TFDA inatakiwa kuratibu upatikanaji wa takwimu kati ya idara za serikali na kupata mafunzo ya jinsi ya kutumia takwimu hizo, kufanya uchambuzi wa ufuatilia utendaji kazi, ikiwa ni pamoja na shughuli kama vile ukaguzi na majibu ya malalamiko;**
6. **Kuanzisha mkakati wa kuchukua hatua kali na endelevu dhidi ya viwanda vya usindikaji wa chakula vinavyokutwa na ukiukwaji mkubwa au wa mara kwa mara, na kuanzisha vigezo na taratibu za kufuatwa wakati wa ukiukwaji mkubwa wa sheria na kanuni za usalama wa chakula;**
7. **TFDA ihakikishe kuwa viashiria vya ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa chakula mipakani na katika viwanda vya kusindika chakula vina andaliwa na kukubaliwa; na mara kwa mara ifanye tathmini na ufuatiliaji wa ukaguzi ili matokeo yake yatumike kama msingi wa kuboresha ukaguzi wa chakula, na**

8. Mamlaka ihakikishe kuwa mtaarifa zote za ukaguzi kutoka serikali za Mitaa zinachunguzwa nakupitiwa kwa kina ili kubaini mapungufu yoyote na kutoa mrejesho kwa walengwa ili waboreshe mapungufu hayo;

4.6.2 Mapendekezo kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ina paswa kuhakikisha kuwa:

1. Ukaguzi wa usalama wa Chakula nchi unaratibiwa na kuwianishwa vizuri, na wadau wote wafanye kazi kwa karibu na kwa pamoja;
2. Ripoti ya jumla juu ya ukaguzi wa chakula unaofanywa na idara mbalimbali za serikali inaandaliwa kila mwaka na kutumika kama msingi wa kuboresha shughuli za ukaguzi wa chakula na hatimaye usalama wa chakula nchini;
3. Takwimu na taarifa kuhusu usalama wa chakula zinasambazwa katika idara mbalimbali za serikali zinazo husika na ukaguzi wa chakula na hutumiwa kama msingi wa mipango ya ukaguzi wa chakula nchini; na
4. Kuanzisha mazungumzo na Wizara ya Viwanda na Biashara ya kuangalia uwezekano wakuchanganya wajibuna majukumu ya Shirika la Viwango (TBS) na Mamlaka ya chakula na dawa (TFDA) kwa sababu mamlaka hizi kimsingi zinajihusisha na majukumuyanayohusiana au yanayofanana.

SURA YA TANO

UKAGUZI WA USIMAMIZI WA WANYAMA PORI

5.1 Utangulizi

Uwindaji wa wanyamapori nchini Tanzania unasimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii (WMU) kupitia Idara yake ya Wanyamapori. Wizara ina wajibu wa:

- Kutengeneza Sera, mikakati na mipango kwa ajili ya utekelezaji wa sera;
- Kutoa na kuendesha haki za watumiaji na leseni za biashara zinazohusu rasilimali ya wanyamapori;
- Kukuza kubadilishana habari na kubadilishana utaalamu kitaifa, kikanda, na kimataifa;
- Kulinda wanyamapori dhidi ya matumizi yaliyo kinyume cha sheria zinazohusiana na uwindaji, ukamataji , na upigaji picha wa wanyamapori na upatikanaji wa nyara
- Kufanya tathmini ya utendaji wa kila mwaka wa utendaji wa makampuni yote ya uwindaji; na
- Kuhakikisha kwamba makampuni yote ya uwindaji yanatoa ripoti juu ya wanyama wote waliouawa, kujeruhiwa, au kukamatwa na wawindaji.

Uwindaji wa wanyamapori nchini unaongozwa na Sheria ya Uhifadhi ya 2009, kanuni zake za mwaka 2010 na Sera ya Wanyamapori ya mwaka 2007. Lengo la sheria hii ni kuongeza ulinzi na uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori na makazi yao.

Tanzania imeridhia mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa na itifaki kwa ajili ya rasilimali za wanyamapori hifadhi na ulinzi. Makubaliano ya kimataifa yanayohusu usimamizi wa uwindaji wanyamapori ni:

- Mkataba wa Biashara ya Kimataifa kuhusu wanyama na mimea iliyo hatarini kutoweka duniani (CITES);
- Mkataba wa Bioanuai (CBD) wa mwaka 1992; na
- Makubaliano ya Lusaka juu ya shughuli za ushirikiano zinazolenga kupambana na biashara haramu ya wanyamapori na mimea.

5.2 Kilichokaguliwa katika uwindaji wa wanyamapori

Ukaguzi ulichunguza kama Wizara ya Maliasili na Utalii inasimamia na kufuatitilia ipasavyo shughuli za uwindaji wa wanyamapori na

ukusanyaji wa mapato yatokanayo na wanyamapori katika mapori ya akiba na mapori tengefu.

Yafuatayo ni maeneo yaliyochunguzwa:

- Kiwango cha mamlaka husika katika kutekeleza kanuni zinazohusu uwindaji wa wanyamapori
- Ufanisi wa wizara katika kufuatilia uwindaji wa wanyama pori katika mapori ya akiba na mapori tengefu.
- Usimamizi wa ukusanyaji na mgawanyo wa mapato unaofanywa na Wizara katika halmashauri za wilaya zenye rasilimali za wanyamapori.

Ukaguzi uliangalia kipindi cha miaka mitatu kuanzia Julai 1, 2009 hadi Machi 31, 2012. Taarifa zilikusanywa katika mapori ya akiba sita (6) kati ya 27 na mapori tengefu manne(4) kati ya 39 yaliyopo Tanzania[5]. Pia, katika vikosi dhidi ujangili vya kanda, vitatu kati ya nane vilitembelewa. Vikosi hivyo ni:- Dar es Salaam, Arusha, and Tabora.

5.3 Sababu za kukagua usimamizi wa uwindaji wanyamapori

Tanzania ni maarufu ulimwenguni kote kwa urithi wa aina mbalimbali za wanyamapori pamoja na mtandao mzuri wa maeneo ya hifadhi. Aina mbalimbali za wanyama pori inatokanana na aina mbalimbali ya mazingira ya asili yapatikanayo nchini ambayo yameifanya nchi kuwekwa katika kundi la ya mataifa yenye aina mbalimbali ya mazingira ya asili. Tanzania inatambua matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori kama sehemu muhimu ya uhifadhi.

Aina kuu ya matumizi ya wanyamapori kwaTanzania ni kutazama wanyama, utalii wa picha,uwindaji wa wakazi na wageni wakazi, ranchi na ufugaji wa wanyamapori. Aina hizi zamatumizini msingi wamaendeleo ya nchikijamii na kiuchumi katika utoaji waajira, upatikanaji wa fedha za kigeni na soko kwa bidhaa za ndani, kwa hiyo mchango wa sekta ya wanyamapori kwa uchumi wa nchini

[1] Mapori ya akiba yaliyotembelewa ni Selous, Rungwa, Kigosi, Moyowosi Ugalla na Rukwa-Lukwati na mapori tengefu yalikuwa ni Kilombero, Lake Natron, Loliondo, na Simanjiro.

mkubwa. Sekta hii inakadiriwa kuchangia asilimia mbili katika pato la taifa. Kwa mfano, uwindaji wa kitalii ulizalisha zaidi ya Shilingi za Kitanzania bilioni 91katika kipindi cha miaka mitatu kati ya mwaka 2009 hadi 2012.

Licha ya mchango huu muhimu, ujangili wa wanyamapori umekuwa changamoto, hasa kwa uchumi wa nchi na jamii zinazopakana na maeneo ya hifadhi. Hivi karibuni, kumekuwa na ongezeko la ujangili nchini. Kwa bahati mbaya jitihada za Idara ya Wanyamapori hazikuzaa matunda katika kukabiliana na wimbi kubwa la mauaji ya wanyamapori yanayotokea, hivyo basi taarifa hii inafika masikioni mwa umma katika kipindi ambacho pembe za ndovu zilikamatwa zikiwa zinasafirishwa nje ya nchi.

Kwa mfano Novemba2010wanyama hai wa aina mbalimbali wapatao 120 na ndege hai 16 walisafirishwa nje ya nchikinyume cha sheria.Pia, kulikuwa na matukio ambapo pembe za ndovu zenye jumla ya uzitowa tani 17.7 zilikamatwa nchini. Ni dhahiri kumekuwa na ongezeko la ukamatwaji wa pembe za ndovu kutoka kilogramu 264mwaka 2008 hadi kilogramu 8,255mwaka 2013.Hiini dhahiri kwamba tembo wengi zaidiwamekuwa wakiuawamwakabaada yamwaka. Hii ni hali ya kushtua.

Kutokana na umuhimu wa wanyamapori kiuchumi kwa nchi na matatizo yaliooneshwa, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iliamua kufanyaukaguzi wa ufanisi wa usimamizi washughuli za uwindaji wanyamapori katika Wizara ya Maliasili na Utalii.

5.4 Matokeo

5.4.1. Utekelezaji wa sheria ya uhifadhi wa wanyamapori

Doria hazikufanywa kwa ufanisi

Doria hazikufanyika kwa ufanisi katika maeneo yanayodhaniwa kuwa na uwezekano mkubwa wa kutokea kwa ujangili. Sababu kuu ni kwamba maeneo ambayo ni korofi kwa ujangili yapo ndani sana ambapo ni vigumu kwa maafisa wanyamapori kufika hasa nyakati za mvua.Wakati wa masika,hali ya barabara katika maeneo hayoni mbaya hivyo magari ya doriakushindwa kupitakatika matope. Idara ya Wanyamapori haijakusanya takwimu kwa lengo la kuzichambua ili kuyaainishamaeneo korofi ya ujangili.

Jumla yatembo 721waliripotiwakuuawa namajangilikatika mapori ya akibamatano2009-2012. Hata hivyo,kutokana na ukosefu watakwimu, jumla ya tembo waliouawa inakadiriwa kuwa ni zaidi ya idadi iliyotolewa hapo juu. Idadi ya tembo waliouawa kutoka na ujangili ni kubwa kuliko idadi ya vifo vya tembo vilivyotokana na sababu nyingine katika mapori hayo matano ya akiba. (angalia Kielelezo namba 1). Katika kipindi cha miaka mitatu hiyo ujangili unaonekana kuongezeka katika mapori ya akiba. Ongezeko hili limetokana nakuongezeka kwa shinikizo la soko la uhitaji wa pembe za ndovu.

Kielelezo namba 1: Vifo vya tembo vilivyotokana na ujangili 2009-2012



Source: Wizara ya Maliasili na Utalii-Kikosi Dhidi Ujangili (KDU)

Takwimu za vifo vya tembo katika mapori tengefu hazikuweza kupatikana. Kwa mujibu wa maafisa wanyamapori takwimu za vifo vya tembo zinakusanywa kwa kufuata mfumo wa ikolojia "ecosystem". Takwimu kwa kufuata mfumo wa kiikolojia zinaonesha vifo vya tembo katika kipindi cha mwaka 2009 hadi 2012 vilifikia 597. Kwa msingi huu, Loliondo na Ziwa Natron – Longido ni sehemu ya mfumo wa ikolojia wa Serengeti-Ngorongoro; Simanjiro ni sehemu ya mfumo wa ikolojia wa Tarangire – Lake Manyara na Kilombero ni sehemu ya mfumo wa ikilojia ya Selous-Mikumi. Kwa hivyo basi haikuwezekana kupata takwimu kwa pori tengefu moja moja.

Tathmini ya doria zilizofanyika

Ukaguziulibaini kuwahakuna mwongozowakufuatwawakati wa kupangadoria, hivyo basi kusababisha maafisa wanyamapori katika mapori ya akiba kukosa uhakika katika utekelezaji wamajukumu yao. Utaratibu unaotumika katika mapori mengi ya akiba ni kwamba timu za doria hukaa porini kwa wastani wa siku10 hadi 15 kwa mwezi. Timu hufuata nyayo kama viashiria vya matukio ya ujangili. Pia ukaguzi ulibaini kuwa, takwimu zilizokusanyawa wakati wa doria hazikuchambuliwa ili kuweza kutathmini mwenendo waujangili na mikakati kutumika katika maeneo husika.

Rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya kupambana na ujangili

Kuna ufinyu wa bajeti kwa ajili ya shughuli za kupambana na ujangili. Wizara ilijipangia lengo la mwaka la doria "surveillance coverage" kuwa asilimia 60 ya jumla ya ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 68,076. Katika kipindi cha mwaka 2010/11 na 2011/12, bajeti ya shilingi za kitanzania bilioni 10 na bilioni 14.9 katika miaka hiyo kwa mfuatano (angalia jedwali namba 1), haikutosha kufanya doria na kufikia lengo la asilimia 60% kama ilivyopangwa.

Jedwali namba 1: Makadirio na matumizi kwa ajili ya shughuli dhidi ujangili

Mwaka	Makadirio (Shilingi Billioni)	Matumizi (Shilingi Billioni)
2010/11	10.0	8.0[6]
2011/12	14.9	10.2[7]

Chanzo: TWPF na taarifa ya utekelezaji kwa mwaka 2010/11 and 2011/12

Kama inavyoonekana katika jedwali hapo juu, fedha zilizotolewa zilikuwa chini ya bajeti iliyopangwa. Hata hivyo, Idara ya Wanyamapori ilifanikiwa kufanya doria katika eneo lenye ukubwa wa 25,135 km² kwa mwaka 2010/11 na 31,825 km² kwa mwaka 2011/12. Hii ni sawa na 37% na 47% kwa miaka hiyo ambayo ni chini ya lengo lililoweka la asilimia 60. Inakadiriwa kuwa, ili kulinda maeneo yaliyohifadhiwa katika ukanda wa kusini na mashariki mwa Afrika zinahitajika kiasi cha dola za Kimarekani 200 kwa kilometa moja ya mraba sawa na makadirio ya shilingi za kitazania 320,000 kwa kilometa moja ya mraba. Hii ina maanisha kwamba kiasi cha bajeti ya shilingi za kitanzania bilioni 21.8 ilitakiwa kupangwa ili iweze kutosha kufanya doria kufikia lengo la asilimia 60 ya jumla ya eneo lilipangwa . Aidha, kulikuwa na upungufu mkubwa wa wafanyakazi wa kufanya doria, zana hasa za simu za upepo "radio call" na kamera katika mapori sita ya akiba na mapori tengefu manne yaliyotembelewa. Kulikuwa na upungufu mkubwa wa "Global Positioning System (GPS)" na mahema katika maeneo manne ya mapori tengefu yaliyotembelewa.

Ushiriki wa wadau muhimu katika utekelezaji wa sheria ya uhifadhi wanyamapori

Ilibainika kuwa Wizara haikuhusisha Mamlaka ya Bandari Tanzania na Mamlaka ya Mapato Tanzania kushiriki kikamilifu katika udhibiti wa ujangili katika bandari na mipakani. Wizara haikufanya ukaguzi katika bandari ingawa kanuni za wanyamapori zimetaja bandari kama sehemu mojawapo ambapo nyara zinaweza kusafirishwa nje ya nchi[8]

6 TWPF MTEF 2011/12
7 TWPF MTEF 2011/12+ Annual implementation Progress Report 2011/12
8 The wildlife conservation (dealing with trophies) regulation of 2010 sixth schedule

Mfumo wa taarifa za siri na usimamizi wa kesi mahakamani

Mfumo wa kuwazawadia watoa taarifa hauna ufanisi wa kutosha kwani malipo ya kuwazawadia watoa taarifa yanafanyika baada ya kesi mahakamani kukamilika na maamuzi kufikiwa. Hakuna mfumo wa kuwezesha uongozi wa mapori ya akiba na wa vikosi dhidi ujangili kuwa na bajeti kwa ajili ya kuwazawadia watoa taarifa wa kufichua ujangili. Mchakato wa kuwalipa watoa taarifa unafanyika moja kwa moja katika idara ya wanyamapori makao makuu. Kwa wastani mchakato huu unachukua muda usiopungua siku 30.

Hata hivyo,hakuna kiwango cha muda kilichowekwa na wizara cha mchakato wa kuwazawadia watoa taarifa. Kwa mujibu wamahojiano na maafisa wanyamapori katika maeneo yaliyotembelewa, ucheleweshwaji wa malipo umesababisha watoa taarifa kutotoa tena taarifamuhimu zinazohusiana na ujangili. Katika mahojiano na maafisa wanyamapori katika maeneo yaliyotembelewa wamebainisha kuwa mahakimu wana mapungufu ya uelewa wa thamani iliyopo katika maliasili. Hii inadhihirishwa kwa adhabu ndogo zinazotolewa kwa wahalifu hivyo kutotumika kama fundisho katika kutokomeza kabisa ujangili.

5.4.2. Ufuatiliaji wa shughuli za uwindaji

5.4.2.1. Tathmini ya mwaka kwa makampuni ya uwindaji

Tathmini ya idadi ya wanyamapori na upangaji wa mgao kwa wawindaji

Sensa kwa kutumia ndege zinazofanywa na Taasisi ya Utafiti wa wanyamapori, pekee hazitoshi katika kutathmini idadi ya wanyamapori na upangaji wa mgao.

Ilibainika kuwa, taarifa za wingi wa wanyama, mafanikio ya uwindaji, ubora wa nyara na mgao hazikuweza kukusanywa ipasavyo na kuchambuliwa ili kupata taarifa kwa ajili ya usimamizi endelevu wa mgao na wanyamapori. Hivyo basi, ilikuwa vigumu kutambua endapo kumekuwa na kupungua au kuongezeka kwa

ubora wa nyara na wingi wa wanyama kwa kutumia taarifa chache zilizokusanywa pasipo kuchambuliwa na idara ya wanyamapori.

Ubora wa Nyara

Katika sampuli ya karatasi153 za ukaguzi wa nyara "trophy inspection sheets" kwa mwaka 2010 na 2011 (karatasi za ukaguzi 83kwamwaka2010 na70kwa mwaka 2011)ilibainika kuwaseti23 za pembe za ndovu, hazikuzingatia viwango. Zote zilikuwa na uzito chini ya kilogram 18 na urefu chini ya sentimita 160. Seti 35 zapembe za ndovu ziliweza kukidhi kiwango kimojawapo ama uzito au urefu. Pia, mwaka 2011seti tatu za pembe za ndovu hazikuwa na kipimo. Hakukuwa na rekodi za kuonyesha vipimo vya ngozi za simba 16 katika makampuni ya matatu hivyo kusababisha ugumu katika kuhakiki kama vigezo vilivyowekwa vilizingatiwa. Hakukuwa narekodi kuonyesha hatua zilizochukuliwa na Wizara dhidi ya makampuni ya uwindaji ambayo hayakukidhi viwango vya nyara vilivyowekwa.

Ubora na Upatikanaji wa makazi ya wanyamapori

Ukaguzi umegundua kwamba, kati ya vibali108 vya uwindaji vilivyopitiwa, asilimia 1 vilijazwa kuonyesha ikolojia ya wanyama waliowindwa, 50% ya vibali vilijazwa kwa sehemutu na49% havikujazwa kabisa hivyo kutoonesha ikolojia ambapo mnyama amewindwa. Zifuatazo ni sababu za vibali kutojazwa ipasavyo:

- Kutokuwa na uelewa wa namna ya kujaza fomu hizo,
- Maafisa wanyama pori kutilia mkazo na kuhakikisha mnyama aliyepo kwenye kibali ndiye anayewindwa bila ya kuzingatia amewindwa katika mazingira yapi.

Kwa sababu hiyo,wanyama huwa wanawindwa katika maeneo yasiyoruhusiwa kama vile katika vyanzo vya maji.

Hali ya Kitalu cha uwindaji

Ilibainika kuwa taarifa zinazowasilishwa zilikuwa hazifanyiwi tathmini ya kina na taarifa ya tathmini hiyo kutumika kama kipimo cha ugawaji wa vitalu katika msimu wa uwindaji utakaofuata.

Uwezo wa wawindaji katika matumizi ya mgao

Si makampuni yote ya uwindaji yalitumia 40% ya wanyama muhimu katika vitalu vya uwindaji walivyopewa. Katika msimu wa uwindaji wa mwaka 2009, jumla ya vitalu vya uwindaji 49 vilitumia 40% ya wanyama na zaidi, katika vitalu 11 matumizi ya wanyama yalikuwa chini ya 40% na vitalu 7 vilikuwa havijatumia kabisa mgao wa wanyama walioruhusiwa. Zifuatazo ni sababu za matumizi ya mgao chini ya asilimia 40:

- Mdororo wa uchumi duniani ambao uliathiri vibaya sekta ya uwindaji wa kitalii
- Kushindwa kulipa madeni ya nyuma.
- Ukosefu wa wanyama wa kuwindwa

Pia katika mwaka huo huo wa 2009, kati ya vitalu vya uwindaji 28 katika mapori ya akiba na mapori tengefu yaliyochaguliwa, vitalu 17 vilikuwa na mgao kwa ajili ya uwindaji wakati vitalu 11 havikuwa na mgao ingawa uwindaji ulifanyika na jumla ya wanyama 151 waliwindwa bila kuwa na mgao. Mwaka 2010, kati ya vitalu vya uwindaji 26, vitalu 10 vilikuwa na mgao na vitalu 16 havikuwa na mgao. Wakati huohuo wanyama 204 wa aina mbalimbali waliwindwa bila kuwa na mgao uliotengwa kwa makampuni ya uwindaji katika vitalu vyao uwindaji. Vile vile, mwaka 2011, vitalu vya uwindaji 25 vilikuwa na mgao kwa ajili ya wanyama kuwindwa. Hata hivyo, tembo 9 na nyati 2 waliwindwa zaidi ya idadi ya mgao uliopangwa.

Tathmini ya Utendaji kazi wa Makampuni ya uwindaji

Ilibainika kuwa, Wizara ya Maliasili haijawahi kufanya uchambuzi wa kina kwa makampuni ya uwindaji kwa kipindi cha 2009-2012. Hakukuwa na ushahidi kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii iliwahi kuandaa taarifa juu ya utendaji makampuni ya uwindaji katika kuchangia maendeleo ya jamii pamoja na kuchangia ulinzi wa maliasili na uhifadhi wa mazingira. Hakuna kampuni uwindaji huu ambayo ilitoa dola za Marekani 5000 kwa mwaka katika kipindi cha mpito[9]. Idara ya Wanyamapori hawana taarifa muhimu za kufanya uchambuzi wa kina wa makampuni ya uwindaji.

---

[9]Kawaida kipindi mkataba kwa ajili ya uwindaji ilikuwa miaka mitano ambayo ilimalizika mwaka 2009. Mwaka 2009 Wizara haikuingia makubaliano mpya na makampuni ya uwindaji kama ilivyotarajiwa. Badala yake, mikataba ya iliyokuwepo

Mfumo wa kusimamia taarifa za Uwindaji

Ukaguzi ulibaini uwepo wa orodha tofauti, moja kwa ajili ya wanyama waharibifu na nyingine ya pembe za ndovu. Zaidi ya hayo ilionekana kuwa, katika kipindi cha msimu wa uwindaji cha 2009-2011 hakukuwa na takwimu zilizohusiana na wanyama waharibifu wala takwimu za pembe za ndovu. Vile vile, Wizara haina mfumo wa kukusanya taarifa za safari za uwindaji. Hii imesababisha Wizara kutokuwa na taarifa ya mienendo ya idadi ya wanyamapori kwa kila kitalu cha uwindaji.

5.4.3. Ukusanyaji wa mapato na Mgawanyo wake

Makadirio ya Mapato

Ilibainika kuwa, Wizara haikuwa na takwimu za mapato ambazo zingetumika kama msingi wakukadiria thamani ya vitalu husika. Makadirio ya mapato yalifanyika kwa kutumia mgao wa wanyama uliotolewa kwa vitalu vya uwindaji kuzidisha kwa bei ya kila mnyama katika eneo husika. Pia Wizara ilifanya makadirio mapato yatokanayo na utalii wa picha kwa Pori la Akiba la Selous tu na kuacha mapori mengine ya akiba na mapori tengefu. Makadirio yanategemea uzoefu wa makusanyo yaliyopita.

Udhibiti wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na Utalii wa Picha

Ilibainika kuwa, katika utalii wa picha, malipo kwa utalii wa picha yalifanyika wakati wateja walipomaliza ziara zao. Makampuni 36 yalibainika kutolipa bili kwa ajili ya utalii wa picha kwa wakati hivyo kuisababibishia wizara hasara ya mapato ya shilingi za kitanzania bilioni 2.7 hadi ilipofikia 2012/11/12. Hii ni ilitokana na kutokuwa na utaratibu sahihi katika kusimamia utalii wa picha.

---

iliongezewa muda wa miaka 3 (2009-2012) kabla ya matangazo ya makubaliano mpya. Kipindi hicho cha miaka 3 ndicho kipindi kama mpito.

Mgawanyo wa mapato kwa wahusika

Katika kipindi cha ukaguzi, ilikuwa ni vigumu kujua mgawanyo wa mapato yatokanayo na rasilimali ya wanyamapori hasa kiasi cha fedha kinachopelekwa Hazina, Idara ya Wanyamapori na kiasi kinachobakia katika mfuko wa uhifadhi wanyamapori (TWPF). Ingawa mgawanyo umekuwa ukifanyika, nyaraka zautoaji fedha hazikuweza kupatikana kwa kipindi kati ya 2009hadi 2012. Hivyo basi Wizara haikuweza kuonyesha kama mgao wa mapato ulifanyika kwa kila mdau sawasawa na asilimia zinazotakiwa.

Matumizi ya Fedha zilizogawiwa kwa Serikali za Mitaa

Wilaya zenye mapori tengefu zinatakiwa kupata mgao wa asilimia 25 ya ada ya wanyamapori waliowinda katika wilaya husika. Halmashauri hutakiwa kupeleka makusanyo yote wizarani na kisha wizara kutuma asilimia 25 ya makusanyo kwa halmashauri husika. Hakuna halmashauri iliyowasilisha taarifa wizarani kuhusu matumizi au mpango kazi juu ya matumizi ya asilimia 25 walizopewa na wizara . Katika wilaya zote zilizotembelewa 40% ya 25% ya fedha ambazo serikali za mitaa hupokea kutoka wizarani hazikutengwa kwa ajili ya kutimiza wajibu wa msingi wa shughuli za uhifadhi wanyamapori. Zifuatazo ni sababu zilizotolewa za fedha kutotumika kwa kusudi la msingi:

- Fedha kutumwa moja kwa moja kwenye akaunti ya pamoja ya wilaya inayosimamiwa na mkurugenzi ambapo matumizi ya fedha yatategemea kipaumbele cha Mkurugenzi.
- Wizara kutochukua hatua kwa wilaya zisizotoa taarifa za matumizi ya mapato kwa ajili ya uhifahi wa maliasili zilizopo wilayani humo. Hivyo basi ni vigumu kwa wizara kuweza kutoa tathmini ya ufanisi wa 25% ya mgao wanayoitoa katika halmashauri za wilaya husika.

Jedwali 5.1: Pesa zilizopokelewa (milioni TZS) na sehemu (%) iliyotumika kwa usimamizi wa wanyamapori katika baadhi ya Serikali za Mitaa

Mwak	KILOMBERO	LONGIDO	SIMANJIRO	LOLIONDO

	Pesa zilizopokelewa(TZS millioni)	Sehemu (%) iliyotumika kwa shughuli za wanyama pori	Pesa zilizopokelewa (TZS millioni)	Sehemu (%) iliyotumika kwa shughuli za wanyama pori	Pesa zilizopokelewa (TZS millioni)	Sehemu (%) iliyotumika kwa shughuli za wanyama pori	Pesa zilizopokelewa (TZS millioni)	Sehemu (%) iliyotumika kwa shughuli za wanyama pori
2010	41.6	40%	59.6	0.0	96.7	0.0	232.3	3.2
2011	30.0	40%	66.1	0.0	70.9	0.0	245.4	3.9
2012	44.6	40%	87.3	6.2	90.8	0.0	184.9	12.0

Chanzo: Halmashuri zilizotembelewa

5.5 Hitimisho

Wizara ya Maliasili na Utalii haijahakikisha sheria ya wanyamapori inatekelezwa ipasavyo kwa lengo la kupunguza matumizi haramu yawanyamapori.Hiiimechangiwa na kugawanya rasilimali zake bila kulenga maeneo korofi kwa ajili ya kupambana na ujangili; Pia si wadau wote walio husishwa kikamilifu katika utekelezaji wa sheria ya uhifadhi wanyamapori; kutofuatilia kwa ukaribu shughuli zauwindaji; nautata wa asilimia katika ugawanywaji wa mapato yatokanayo na maliasili kwa wadau husika.

5.6 Mapendekezo

5.6.2 Utekelezaji wa sheria na kanuni za uhifadhi wanyamapori

Wizara ya Maliasili na Utalii inapaswa kuhakikisha kuwa:

- Inafanya uchambuzi wa viashiria vya ujangili na kuweka malengo yanayotekelezeka pamoja na uchambuzi wa mgawanyo wa rasilimali.
- Inaweka mikakati madhubuti katika kupambana na ujangili nyakati za masika.
- Vifaa muhimu vinapatikana kwa ajili ya doria katika mapori ya akiba na kanda za vikosi dhidi ujangili.
- Ifanye uchambuzi wa wadau muhimu na kuwashirikisha katika kupambana na ujangili na kupambana na mauzo haramu ya nyara nje ya nchi.
- inashirikiana na Mahakama kuhakikisha kwamba adhabu zitolewazo zinaleta matokeo chanya katika kuzuia ujangili.

- Inaweka vituo katika maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa wanyamapori.

5.6.3 Ufuatiliaji wa shughuli za uwindaji

Wizara ya Maliasili na Utalii inapaswa kuhakikisha kuwa:

- Inafanya tathmini ya ubora wa nyara
- Inafanya mapitio ya malipo ya dola za kimarekani 5000 ya kila mwaka kutoka kwa makampuni ya uwindaji na kuhakikisha inafanya kazi iliyokusudiwa.
- Inasimamia ukusanyaji, uchambuzi, utunzaji wa kumbukumbu na matumizi ya takwimu za uwindaji na doria zinazokusanywa katika kupanga na kufanya maamuzi.
- Inaandaa na kutumia fomu ambazo zitatumika kujazwa na maafisa wanyamapori au ''game scout'' ambao wanaambatana na wateja wa uwindaji.
- Inaratibu ipasavyo michango itolewayo na wadau kwa ajili ya kutokomeza ujangili na maendeleo ya jamii.
- Inawapa mafunzo maafisa wanyama pori katika kujaza sehemu husika katika vibali vya uwindaji.

5.6.4 Ukusanyaji wa mapato na Mgawanyo

Wizara ya Maliasili na Utalii inapaswa kuhakikisha kuwa:

- Inafanya tathmini ya mapato yatokanayo na wanyamapori ili kupata "benchmark" kama msingi wa makadirio ya mapato
- Kuna mfumo wa kukusanya mapato yatokanayo na utalii wa picha kwa wakati
- Mfumo wa udhibiti wa ukusanyaji wa mapato na unafuatwa
- Kuna mfumo wa mgawanyo wa mapato kwa kuzingatia ukubwa wa majukumu na viashiria mbalimbali vilivyoainishwa.
- Inawataka Serikali za Mitaa kutoa taarifa za fedha zilizopangwa kwa ajili wa uhifadhi wa mazingira na ulinzi wa rasilimali za wanyamapori katika maeneo yao husika.
- Inashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kuhakikisha serikali za mitaa zinatumia rasilimali zilizopangiwa kwa ajili ya shughuli za ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na maeneo yao kama ilivyoelekezwa.

SURA YA SITA

USIMAMIZI WA TAKA ZINAZOTOKANA NA HUDUMA YA AFYA

6.1 Utangulizi

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) ndio waangalizi na wasimamzi wakuu kwenye masuala yanayohusu usimamizi na udhibiti wa taka zinazotokana na huduma ya afya hapa nchini. Wizara hizi mbili ndio zenye wajibu wa kutunga sera na kuandaa miongozo ya namna ya kutekeleza sera hizo.

Usimamzi wa taka hatarishi zitokanazo na huduma ya afya unasimamiwa na: Sheria ya Afya ya umma ya mwaka 2009, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, ya mwaka 2004, Sheria ya Afya na Usalama Kazini ya 2003, Sera ya Taifa Miongozo ya Udhibiti wa taka zitokanazo na huduma ya afya, Mpango wa ufuatiliaji wa taka zitokanazo na huduma ya afya, na viwango va kitaifa na taratibu kwa ajili ya usimamizi wa taka zinazotakana na huduma ya afya.

6.2 Tulichochunguza katika usimamizi wa taka

Ukaguzi umeangalia kama Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zina hakikisha kwamba taka zinazotokana na huduma ya afya zinasimamiwa ipasavyo ili kulinda afya ya umma na mazingira. Ukaguzi huu uliangalia kama:

- **Vituo vinavyotoa huduma za Afya vinadhibiti taka zinazotokana na huduma ya afya kuanzia pale zinapozalishwa mpaka zinapotupwa au kuteketezwa**

- **Serikali za Mitaa na Sekretaret za Mikoa zinafanya ufuatiliaji shirikishi (supportive supervision) na ukaguzi wa jinsi Vituo vinavyotoa huduma za Afya vinavyosimamia au kudhibiti taka zinatzotokanana na huduma ya afya, na**

- **Wizara ya Afya na Ofisi ya Waziri mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa jinsi wanavyo dhibiti na kutathmini kiwango cha usimamizi wa taka zinazotokana na huduma ya afya nchini.**

Ukaguzi ulichunguza utaratibu mzima wa usimamizi wa taka zinazotokana na huduma ya afya, kuanzia pale zinapozalishwa mpaka pale zinapotupwa au kuteketezwa. Pia, mambo mengine kama vile usimamizi shirikishi, ukaguzi, ufuatiliaji na tathmini ya usimamzi wa taka viliangaliwa.

Ukaguzi ulichunguza taarifa za miaka mitatu ya fedha kutoka 2010/2011 mpaka 2012/2013 ni kufuatia kutungwa kwa mpango wa Taifa wa kusimamia taka zinazotokana na huduma ya afya wa mwaka 2007 ambao ulitoa mwanya wa kipindi cha miaka mitatu kuutekeleza kabla ya kufanyiwa tathmini ya kiwango cha utendaji.

6.3 Sababu za kuchunguza taka zinazotokana na huduma ya afya

Tanzania kama zilivyo nchi nyingine zinazoendelea inakabiliwa na tatizo la usimamizi wa taka zinazotokana na huduma ya afya. Hakuna takwimu za uhakika juu ya kiwango cha taka zinazozalishwa hapa nchini. Hata hivyo, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (mwaka 2007) ilikadiria kuwa, wastani wa uzalishaji kwa mwaka kuwa ni tani 4,745. Taka nyingi zinazozalishwa hazisimamiwi vizuri, kuanzia utekelezaji wa utenganishaji, ukusanyaji, uhifadhi na utupaji.

Uzalishaji wa taka zinazotokana na huduma ya afya umekua ukiongezeka zaidi katika miaka ya hivi karibuni, kwa sababu ya kuongezeka na upanuzi wa huduma za afya hasa katika maeneo ya mijini, hii pia inatokana na ongezeko la watu, kuongezeka kwa kampeni na mahuduma ya afyabu ya magonjwa mbalimbali kama surua, kifua kikuu na pepopunda, ongezeko la matumizi ya mabomba ya sindano na sindano zinazotumika mara moja tu ili kuepusha maambukizi ya virusi vya ukimwi. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na vituo vya huduma ya afya bado hazija chukua hatua za kutosha kukabiliana na ongezeko la taka zinazotokana

na huduma ya afya. Iwapo taka zinazotokana na huduma ya afya hazisimamiwa vizuri, zinanaweza kusababisha athari kubwa kwa afya ya binadamu na mazingira kwa ujumla. Katika miaka ya karibuni kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wataalam wa afya na watu mbalimbli wakitoa wito kwamba hatua za haraka zinahitajika kuchukuliwa juu ya marekisho ya namma ya kudhibiti na kutunza taka katika hospitali na taasisi nyingine za afya.

6.4 Matokeo ya ukaguzi

6.4.1 Wizara ya Afya na OWM - TAMISEMI hawaja fuatilia vya kutosha shughuli zinazohusiana na usimamizi wa taka zinazotokana na huduma ya afya nchini

Utaratibu wa uwasilishaji taarifa hauna tija

Masuala yanahusu usimamizi wa taka zinazotokana na huduma ya afya hayatolewi taarifa kama inavyotakiwa katika ngazi zote. Utaratibu wa kutoa taarifa uliopo yaani kumia MTUHA hautoi taarifa sahihi za namna taka zinavyosimamiwa, hivyo taarifa sahihi haziwasilishwi kama inavyotakiwa kwenda kwenye ngazi za juu. Yaani kutoka vituo vya afya, serikali za mitaa na Sekretarieti za Mikoa. Matokeo yake, masuala muhimu kuhusiana na usimamizi wa taka hayafiki kwa usahihi katika ngazi ya serikali kuu. Pia, Wizara ya Afya haikuweza kuandaa ripoti kuhusu hali ya taka zinazotokana na huduma ya afya hapa nchini.

Wizara ya Afya, ambayo ilitakiwa kuwa taswira na taarifa zote zinazohusu usimamizi wa taka nchini ili iweze kutoa taarifa za kuaminika kwa wadau. Bila kuwepo kwa taarifa sahihi za usimamizi wa taka zinazozalishwa wakati wa huduma ya afya nchini, ni vigumu kwa serikali kupima maendeleo na kutambua maeneo dhaifu yanayohitaji kuboreshwa zaidi.

Wizara muhimu katika swala hili, Wizara ya Afya na OWM - TAMISEMI, hawajaandaa mkakati wa kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za taka katika ngazi zote (yaani Mikoa, Serikali za Mitaa na vituo vya huduma ya afya).

Wizara imekuwa ikiandaa mipango, kwa dharura, pale tu wanapopata fedha. Mipango hii ya dharura inakuwa haina malengo wala mikakati ya muda mrefu ya usimamizi shirikishi na ukaguzi wa shughuli za taka katika vituo vya huduma ya afya. Kwa sababu ya hiyo, wizara ya haiwezi kutathimini utendaji wake katika kusimamia taka zinazotokana na huduma ya afya nchini.

Ukosefu wa takwimu za taka zinazotokana na huduma ya afya ili kufanya maamuzi

Wizara ya Afya haina taarifa na takwimu za kutosha zinazohusiana na hali ya usimamizi wa taka zinazotokana na huduma ya afya ili kuwawezesha kufanya maamuzi na kutathmini utendaji wao. Kuna matatizo katika upatikanaji wa takwimu zenye ubora kwa wakati mwafaka.

Wizara haikuweza kutunza takwimu za kuaminika na zinazokwenda na wakati kutoka Serikali za Mitaa na vituo vya huduma ya afya. Mara nyingi taarifa na takwimu zilizopatikana zilikuwa ama hazina uhakika au zilichelewa. Ukosefu wa mfumo mzuri wa kuripoti masuala ya usimamizi wa takahuduma ya afya kutoka Serikali za Mitaa na vituo vya huduma ya afya umechangia kuleta changamoto inayowakabili watoa huduma katika kukusanya taka zinazotokana na huduma za afya.

Wizara haitumii MTUHA kukusanya taarifa za taka zinazotokana na huduma ya afya kutoka vituo vya huduma ya afya. Mfumo wa MTUHA hautoi nafasi kwa ajili ya ukusanyaji wa taka zitokanazo na huduma ya afya kama invyotakiwa. Kwa sababu hii, Wizara ya Afya na OWM - TAMISEMI wamekuwa wanakosa taarifa muhimu za usimamizi wa taka zinazotokana na huduma ya afya kutoka Serikali za Mitaa na vituo vya huduma ya afya katika ngazi mbalimbali.

Uratibu usiotosheleza kati ya serikali kuu, Serikali za Mitaa na vituo vya huduma ya afya

Shughuli za usimamizi wa taka nchini, katika ngazi zote, haziratibiwi vizuri. Watendaji wengi amabao walitakiwa kusimamia au kudhibiti taka zinazotokana na huduma ya afya katika Serikali za Mitaa, vituo vya huduma ya afya na Sekretarieti ya mkoa hawatambui majukumu na wajibu wao kuhusu usimamizi wa taka hizi. Kwa sababu hiyo, shughuli muhimu za udhibiti wa taka hazifanyiki kama ilivyo ainishwa katika miongozo mbalimbali. Aidha, miongozo muhimu kuhusu udhibiti wa taka haijawafikia walengwa.

Ukosefu wa Mipango katika Ngazi za Mkoa, Halmashauri na Vituo vya huduma ya afya

Wizara ya Afya iliandaa mpango mkakati wa kitaifa wa kudhibiti taka zinazotokana na huduma ya afya mwaka 2008. Hata hivyo, mpango huu haukutumika katika kuandaa mipango ya utelezaji katika ngazi za chini, yaani Sekretarieti za Mikoa (RSs), Serikali za Mitaa na vituo vya huduma ya afya. Kwa sababu hiyo, mkakati wa kitaifa wa kudhibiti taka zinazotokana na huduma ya afya hautaweza kufikia malengo yaliyokusudiwa na kuleta matokeo ya kitaifa.

Pia imeonekana kwamba, Wizara ya Afya haina mikakati kabambe ya kusambaza elimu ya namna ya kudhibiti taka zinazotokana na huduma ya afya wadau. Programu za kuhamasisha na

kufundisha hazifanywi mara kwa mara. Usambazaji wa taarifa/elimu ya masuala ya taka zinazotokana na huduma ya afya umekua ukifayika wakati wataalamu mbalimbali wanapokutana katika warsha, semina, mikutano na matukio mengine ambayo huvutia idadi kubwa ya wadau.

Shughuli za usimamizi wa taka za huduma ya afya hazifadhiliwi ipasavyo

Masuala ya usimamizi wa taka za huduma ya afya hutengewa fedha kidogo za uendeshaji. Hii inatokana na kipaumbele kidogo kilichowekwa katika mgawanyo wa rasilimali kwenye shughuli zinazohusiana na usimamizi au udhibiti wa taka zinazotokana na huduma ya afya.

6.4.2 Sekretariati ya mkoa na Serikali za Mitaa hazifuatilii ipasavyo usimamizi wa taka za huduma ya afya

Serikali za Mitaa hazisimamii na kufuatilia vya kutosha utendaji wa shughuli za usimamizi wa taka zinazotokana na huduma ya afya katika vituo vya huduma ya afya kama Hospitali na Vituo vya afya vilivyopo katika maeneo yao. Hii, pamoja na mambo mengine, inasababishwa na mfumo uliopo wa kupeleka taarifa kutoka ngazi za chini hadi wizarani. Mfumo huu wa mawasiliano hautoi nafasi kwa habari za taka za huduma ya afya kutoka kwenye vituo vya huduma kwenda Serikali za Mitaa.

Ziara za usimamizi zinazofanywa na Halmashauri kwenye vituo mbalimbali vya huduma ya afya hazigusii sana masuala ya yanayohusu usimamizi wa taka zinazotokana na huduma ya afya. Wakati wa ziara hizo, watalaam wa afya hawatumii miongozo yenye orodha ya vitu muhimu vinavyo takiwa kuangaliwa katika kutuo husika cha huduma ya afya. Wakati mwingine, maafisa afya wa halmashauri wanashindwa kufika katika vituo vyote vya huduma ya afya, Matokeo yake, kuna ongezeko la watu kuchanganya taka hatarishi pamoja na taka zisizo hatarishi.

Katika halmashauri nyingi, mgawanyo wa rasilimali (yaani watu, vifaa, na fedha) hautoi kipaumbele kwa shughuli taka. Hapakuwa na Halmashauri yoyote ambayo iliandaa bajeti mahsusi kwa ajili ya usimamizi masuala ya taka hatarishi zinazotokana na huduma ya afya. Halmashauri nyingi ziliweka kipaumbele kwenye ununuzi wa dawa na shughuli nyingine za huduma ya afya.

6.4.3 Vituo vinavyotoa huduma ya afya havifuati kanuni za kudhibiti taka wanazozalisha

Utenganishaji wa taka haufanyiki kama inavyotakiwa katika vituo vingi vya huduma ya afya, ikiwemo hospitali, zahanati na vituo vya afya. Kiasi kikubwa cha taka zinazozalishwa hazitenganishwi kama inavyotakiwa. Taka zisizo hatarishi, taka hatarishi, taka hatarishi zaidi pamaja na vifaa vyenye ncha kali kama sindano na nyembe huwa zinachanganywa pamoja. Ukiukwaji wa taratibu za utenganishaji taka unaofanywa na vituo vya huduma ya afya unachangiwa na kutokuwa na ufuatiliaji wa karibu, usambazaji hafifu wa vifaa vya kudhibiti taka, ukosefu wa mafundisho sahihi na uhamasishaji kwa watoa huduma za taka. **Jedwali 6.1** linaonyesha kiwango cha kufuata taratibu kama ilivyochambuliwa kutoka katika majibu yaliyopatikana kupitia madodoso yaliyojazwa na maofisa wa huduma za afya katika vituo mbalimbali vilivyo tembelewa.

Jedwali 6.1: Kiwango cha kufuata kanuni za utenganishaji wa taka zinazotokana na huduma ya afya

Aina ya kituo cha huduma ya afya	Asilimia
Hosptitali za rufaa	65% - 80%
Hospitali za mikoa	60% - 80%
Hospitali za wilaya	30% - 60%
Vituo vya afya	40% - 60%

Chanzo: Majibu kutoka madodoso yaliyojazwa na maafisa kutoka katika vituo vya huduma ya afya

Taka hatarishi kutoka katika vituo vya huduma ya afya, hazitunzwi vizuri kabla ya kwenda kutupwa. Katika hospitali nyingi za Wilaya na katika baadhi hospitali za mikoa, mitambo ya kuchomea taka hizo ni aina ya De Montfort na imechakaa sana. Hivyo taka huwa hazichomwi vizuri mpaka kuwa majivu kama inavyotakiwa, ili kweza kuua vijidudu vyote na kuepuka watu kuchomwa na kujeruhiwa na vitu vyenye ncha kali. Kutochomwa vizuri kwa taka hizi hatarishi kunaweza kupelekea uchafuzi mkubwa wa mazingira na kuathiri afya za watu.

Hapakua na kituo hata kimoja ambacho kiliweza kuunganisha shughuli za usimamizi wa taka katika mpango wake wa shughuli

za kila siku. Vituo vya huduma ya afya havikuweza kutoa malelezo ya kina kuhusu malengo, shughuli na rasilimali zitakazotumika kwa ajili ya usimamizi wa taka za huduma ya afya kuanzia hatua ya kuzalisha taka hadi tupa au kuchoma.

Wakati huohuo, Bohari ya Madawa nchini (MSD) haikuweza kusambaza vifaa vinavyohitajika kwa matumizi ya usimamizi wa taka kwenye vituo vya huduma ya afya. Hii ni kwa sababu Wizara ya Afya haijajumuisha vifaa hivi katika orodha ya vitu muhimu ambavyo MSD wanapaswa kununua ili kukidhi mahitaji ya vituo vya huduma ya afya.

6.5 Hitimisho

Pamoja na uwepo wa miongozo na kanuni mbalimbali zinazohusu usimamizi wa taka hatarishi zinazotokanana huduma ya afya hapa nchini, udhibiti wa taka hizo kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati bado si mzuri. Hii ni kwa sababu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na OWM –TAMISEMI, kama waangalizi wakuu, hawajaweka mfumo na utaratibu mzuri wa ufuatiliaji na udhibiti katika usimamizi wa taka hizo.

Kwa upande mwingine, sekretarieti za mikoa na Serikali za Mitaa hazikufanya vizuri kwenye kusimamia na kufuatilia namna vituo vya huduma ya afya vinavyodhibiti taka hatarishi. Matokeo yake, Hospitali na Vituo vya Afya havikuweza kufanya vizuri katika kusimamia udhibiti wa taka kuanzia pale zinapozalishwa, zinapotenganishwa, zinapokusanywa, zinaposafirishwa na zinapoharibiwa au kuchomwa.

6.6 Mapendekezo

Mapendekezo haya yanaelekezwa kwa Wizara ya Afya na OWM - TAMISEMI, ambao ni waangalizi wa wakuu katika usimamizi wa jumla wa udhibiti wa taka kutoka vituo vya huduma ya afya. Mapendekezo yamegawanyika katika makundi mawili, la kwanza mapendekezo ambayo yanaelekzwa moja kwa moja kwa wizara, ambapo yale ya kundi la pili ni yale ya kutekelezwa na vituo vya

huduma ya afya, serikali za mitaa chini ya usimamizi wa Taasisi zote mbili kwa ushirikiano.

6.6.1 Mapendekezo yanayoelekezwa kwa Wizara ya Afya na OWM - TAMISEMI

Inapendekezwa kwa Wizara ya Afya kufanya yafuatayo:

- Kuandaa na kutekeleza mpango wa ufuatiliaji namna mambo ya udhibiti wa taka zinazotokana na huduma ya afya inavyosimiwa katika ngazi zote (yaani Mikoa, Serikali za Mitaa na vituo vya huduma ya afya). Mpango huo unatakiwa uwe na malengo na mikakati ya kufanya ziara ya usimamizi (supportive supervision) na ukaguzi kwenye vituo vya huduma ya afya kwenye masula ya taka.

- Kuanzisha utaratibu ama mfumo wa namna wa kugharamia mambo ya usimamizi wa taka hapa nchini, ili shughuli hizi ziwe zinaingia kwenye mipango na zina tengewa bajeti.

- Iongeze wigo katika MTUHA, ili mfumo huo wa ukushanyaji taarifa uweze pia kukusanya taarifa za usimamzi wa taka hatarishi zinazotokana na huduma ya afya. Hii itaboresha ufuatiliaji wa karibu.

- Wizara iingize mambo ya udhibiti na usimimazi wa taka katika mitaala ya vyuo vya utabibu na masuala ya afya ili wahitimu waweze kuwa na uelelwa mapema wa mambo ya takahuduma ya afya kabla ya kuanza kazi ya utabibu.

- Wizara ya Afya ijumuishe vifaa muhumu katika usimamizi wa taka hatarishi zinazotokana huduma ya afya kwenye orodha ya vitu muhimu ili MSD waweze kununua vifaa vitakavyokidhi mahitaji ya vituo vya huduma ya afya.

6.6.2 Mapendekezo yanayoelekezwa kwa Sekretariet ya mikoa na Serikali za Mitaa

Ili kuboresha hali ya udhibiti wa taka katika vituo vya huduma za huduma ya afya na Serikali za Mitaa, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI inatakiwa kuhakikisha kwamba:

- **Serikali za mitaa zinaweka taarifa za udhibiti wa taka hatarishi zinazotokana na huduma ya afya katika taarifa zao zinazopelekwa katika ngazi ya mkoa. Hii itarahisisha kazi ya ufuatiliaji inayofanywa na Sekretarieti za mikoa.**

- **Watalaam wa Afya kutoka katika halmashauri wanatakiwa kuandaa mpango wa kufanya usimamizi na ukaguzi. Ukaguzi lazima uwe na orodha ya vitu muhimu vya kuagalia kuhusiana na usimamizi wa taka hatarishi kutoka katika vituo vya huduma ya afya kama ilivyoainishwa kwenye miongozo ya Wizara ya Afya.**

- **Serikali za Mitaa zitoe kipaumbele cha kutosha kwa shughuli za usimamizi wa taka hatarishi zinazotokana na huduma ya afya katika mgawanyo wa rasilimali fedha, watu na vitendea kazi.**

6.6.3 Mapendekezo yanaelekezwa kwa vituo vya huduma ya afya

Ili kuboresha usimamizi mzima wa taka hatarishi zinazotokana na huduma ya afya (yaani kuanzia uzalishaji wa taka hizo hadi utupaji au uchomaji) katika vituo vya huduma za huduma ya afya, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI inatakiwa kuhakikisha kwamba:

- **Vituo vinavyotoa huduma za huduma ya afya vinawekeza katika njia za kupunguza, kutumia tena na kusaga vifaa vinavyo tumika katika mahuduma ya afyabu na kusababisha kuwa taka ili kupunguza uzalishaji taka.**

- **Vituo vinavyotoa huduma za afya vinasimamia na kufuatilia kwa karibu utoaji wa huduma za afya ili kuhakikisha kwamba, miongozo iliyotolewa ya namna nzuri ya kudhibiti taka hatarishi inafuatiliwa. Halikadhalika, kila kituo cha**

huduma ya afya kinatakiwa kuwa na Afisa Afya mahsusi atakaye simamia shughuli zote za udhibiti wa taka katika kituo husika.

- Vituo vinavyotoa huduma za afya, vinatakiwa kuunganisha shughuli za udhibiti wa taka hatarishi zinazotokana na huduma ya afya katika mipango mkakati yao. Mipango hiyo inapaswa kutoa maelezo ya kina juu ya malengo mahsusi, shughuli na rasilimali zinazotakiwa kutumika, aina ya taka zinazozalishwa na namma ya kuzitenganisha.

SURA YA SABA
USIMAMIZI NA UDHIBITI WA GHARAMA KATIKA MANUNUZI YA UMMA

7.1 Utangulizi

Manunuzi katika Sekta ya Umma yalikuwa yakisimamiwa na sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na Miongozo ya 2005. Kuanzia Desemba 2013, manunuzi katika Sekta ya Umma yalianza kusimamiwa na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Miongozo ya mwaka 2013. Sheria hii inahusu manunuzi yote yanayotokana na fedha za Umma; hata hivyo, manunuzi katika Serikali za Mitaa yanasimamiwa na sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 pamoja na mabadiliko yaliyofanyiwa katika nyakati tofauti. Sheria hizi zimeweka mfumo wa manunuzi ya umma ambao una malengo yafuatayo:

- Kuhakikisha kuwa manunuzi yanafanyika kwa haki, uwazi, uwajibikaji na kwa namna ya ushindani;
- Kuchangia katika kuleta mazingira bora ya kiuchumi nchini; na
- Kuongeza ushiriki wa Sekta Binafsi katika kuleta maendeleo nchini.

Wizara ya Fedha ina wajibu wa jumla wa kusimamia masuala ya manunuzi nchini. Hii ni pamoja na uundaji wa sera, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa sera.

7.2 Tulichochunguza kwenye udhibiti wa gharama katika manunuzi ya umma

Ukaguzi ulichunguza endapo Taasisi za Serikali Kuu na zile za Serikali za Mitaa zina utaratibu unaofaa na unaofanya kazi katika kudhibiti ongezeko la gharama katika manunuzi ya umma. Ukaguzi ulijikita katika manunuzi ya tiketi za ndege kwa ajili ya usafiri wa anga kwa watumishi wa umma katika baadhi ya wizara zilizoainishwa, na kwa upande mwingine, ujenzi wa majengo ya umma ambapo ukaguzi uliangalia miradi iliyoainishwa kutoka mamlaka ya serikali za mitaa.

Ukaguzi ulidhamiria kutathmini haya yafuatayo:

- endapo Taasisi za Manunuzi zinafanya mipango na matayarisho kwa ajili ya manunuzi mbalimbali kwa utoshelevu;
- endapo watoa huduma na wakandarasi wanachaguliwa kwa kuzingatia udhibiti wa gharama za kupata huduma husika;
- endapo Taasisi za Manunuzi zinawasimamia vema watoa hudima kwa lengo la kudhibiti gharama za huduma husika; na
- hatua zilizochukuliwa na taasisi za manunuzi na vyombo vya udhibiti katika kushughulika na masuala ya udhibiti wa gharama.

Kwa upande wa tiketi za ndege, wizara nne[10] zilichaguliwa kwa msingi wa matumizi yake katika manunuzi ya tiketi kwa ajili ya usafiri wa anga. Kwa upande wa ujenzi wa majengo ya umma, Mamlaka saba za Serikali za Mitaa[11] zilichaguliwa. Ukaguzi ulichunguza taarifa zinazohusu shughuli zilizofanyika katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka Julai 2010 hadi Juni 2013.

Ukaguzi huu unafanya marejeo kutoka sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005. Ukaguzi unatambua pia uwepo wa sheria mpya ya manunuzi ya mwaka 2011 pamoja na kanuni zake za mwaka 2013 ambazo zimeanza kutumika kuanzia Januari 2014.

7.3 Sababu za kuchunguza udhibiti wa gharama katika manunuzi ya umma

Manunuzi katika sekta ya umma ni moja ya mambo muhimu katika shughuli za kila siku za kwenye serikali yoyote ile katika utekelezaji wa majukumu yake. Hata hivyo, kumekuwa na wasiwasi kutoka kwa wadau mbalimbali kuhusu mfumo wa manunuzi ya umma uliopo serikalini na utekelezaji wake endapo unaleta manufaa

[10] Wizara ya Mambo ya Nje na ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Mali asili na Utalii, Ofisi ya Rais-Menejiment ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Fedha.
[11] Manispaa ya Kinondoni, Ilala, Morogoro, Mji wa Kibaha, Wilaya za Bahi na Kilombero.

kupitia vifaa na huduma zinazonunuliwa. “Thamani ya fedha” ndiyo kanuni ya msingi inayoongoza manunuzi ya serikali. Haipimi tu gharama za manunuzi ya vifaa ama huduma bali inazingatia pia mchanganyiko wa ubora, gharama na matumizi ya rasilimali, madhumuni, wakati na uwezekano wa kufikia maamuzi endapo, kwa pamoja, itathibitika kuna thamani bora. Katika mchakato wa manunuzi, kanuni hii inahitaji uchambuzi wa undani wa gharama zote halali na faida ya kila pendekezo katika mzunguko wote wa mchakato wa wa manunuzi.

Kwa mwaka 2012/2013, taarifa[12] zinaonesha kuwa kiasi cha Shilingi 37 bilioni zilitumika kwa ajili ya manunuzi ya tiketi kwa ajili ya usafiri wa anga kwa watumishi wa umma katika wizara zote serikalini. Hiki ni kiwango kikubwa cha fedha ambacho kimeleta motisha wa kufanya utafiti huu. Kwa upande mwingine, ujenzi wa majengo katika halmashauri za serikali za mitaa ni eneo jingine ambalo wadau wameonesha wasiwasi juu ya ukubwa wa gharama zake. Inakadiriwa kuwa kiasi cha Shilingi 88[13] bilioni zimetumika kwa ajili ya manunuzi ya kazi za ujenzi wa majengo ya umma kwa mwaka unaoishia Juni 2013.

7.4 Matokeo ya ukaguzi

7.4.1 Manunuzi ya tiketi za ndege

Kuanzishwa na kuboreshwa kwa bei elekezi (benchmark price)

Taasisi za manunuzi hazina mipango iliyo toshelevu na makadirio sahihi kwa ajili ya usafiri wa ndege kwa watumishi wa umma. Bei elekezi pekee zilizotumika na zilizobainishwa zilikua ni makadirio yaliyoko kwenye mipango ya manunuzi ya mwaka na bajeti ambazo hata hivyo hazikuandaliwa na kukadiriwa kwa usahihi. Makadirio

[12] Taarifa kutoka EPICOR, 2012/2013
[13] Taarifa kutoka EPICOR, 2012/2013

ya matumizi kwa mujibu wa mipango ya manunuzi hayakutoa picha halisi ya safari ambazo zinafanyika katika miaka husika. Taasisi za serikali hazikujumuisha idadi ya safari za maofisa na muda wao wa safari katika mipango yao ya manunuzi kwa miaka husika.

Hapakuwa na ushahidi uliooonesha kuwepo kwa mapitio ya makadirio na maoteo kabla ya kuwaalika wazabuni kwa ajili ya kutoa huduma hiyo. Pia, hapakuwa na kumbukumbu, taarifa za utafiti wa bei za soko ambao ulifanywa wala kuhusisha taasisi nyingine ili kupata bei zinazosadifu soko kwa wakati husika.

Uhalisi wa bei elekezi

Wakala wa Huduma za Manunuzi (GPSA), kwa kutumia mamlaka[14] yake kisheria, huweka bei elekezi. Bei hizi ni kwa ajili gharama za huduma ambazo Taasisi za Manunuzi zingewalipa mawakala wa kutoa huduma za usafiri wa anga walioidhinishwa kwa muda wa wote wa miaka mitatu iliyokaguliwa. Hii ilifanyika kwa njia ya zabuni ya wazi ambapo wazabuni waliwasilisha zabuni zao na bei ambazo zilifanyiwa uchambuzi na kisha bei elekezi ziliwekwa na kuidhinishwa kwa ajili ya kutumika na wazabuni wote.

Mapitio ya taarifa na nyaraka hayakuonesha kuwepo kwa utafiti wa kina wa bei za soko uliofanyika ili kufikia bei elekezi zilizoidhinishwa. Mapitio Zaidi yalibainisha kutokuwepo kwa mchanganuo wa mahesabu uliopelekea kupatika kwa viwango vilivyoidhinishwa. Mapitio ya bei zilizowekwa na GPSA kwa miaka mitatu ya ukaguzi pia yalionesha mkinzano/kutokushabihiana kwa kuwa kila mwaka GPSA waliweka viwango vinavyotofautiana kwa kiasi kikubwa bila ya maelezo ya kuhalalisha tofauti hizo.

[14] Executive Agencies (Government Procurement Services Agency Establishment) (amendment) Order, 2012; Para 2.3.3

Tofauti ya bei zinazolipwa na bei zilizoko kwennye mikataba

Mawakala wa usafiri wa anga walitakiwa kutoza gharama ya huduma kama ilivyo katika Mikataba iliyoandaliwa na GPSA[15]. Hata hivyo, mawakala wamekuwa wakitoza gharama za huduma kwa viwango ambavyo ni zaidi ya vile vilivyoko kwenye mikataba na GPSA. Sampuli ya tiketi 22 iliyochukuliwa ikiwakilisha safari 239 za maofisa wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ilibainisha kuwa bei ya gharama ya huduma ilitozwa zaidi ya kiwango kilichokubaliwa. Matokeo yake taasisi za manunuzi zililipa TZS 44 milioni badala ya TZS 23.5 milioni hivyo kupelekea malipo ya ziada ya TZS 20.5 milioni ambayo ni karibu ya mara mbili ya gharama zilizotakiwa kulipwa.

Vile vile, uchunguzi wa sampuli ya safari 229 (ikiwa ni tiketi 20) kutoka kwa wakala mwingine kwenye wizara hiyo hiyo[16] ulibaini kuwa tiketi zote zilitozwa zaidi ya kiwango kilichokubaliwa. Baadhi ya tiketi zilitozwa zaidi ya mara kumi na sita (16) ikilinganishwa na bei iliyowekwa kwenye mkataba na wa GPSA. Nusu ya tiketi ilitozwa zaidi ya mara tatu (3) bei iliyokubaliwa. Matokeo yake, wizara ililipa TZS 70.8 milioni badala ya TZS 18.4 milioni ikipelekea ongezeko la TZS 52.3 milioni ambayo ni mara tatu zaidi ya kiwango kilichokuwa kwenye mkataba.

Mawakala wanachagua bei za juu zaidi

Mawakala walioidhinishwa na GPSA wamekuwa wakiwasiliana moja kwa moja na taasisi za manunuzi endapo kuna uhitaji wa usafiri wa anga. Mapitio ya mikataba ya manunuzi yalionesha hapakuwa na kipengele ambacho kingeweza kumfanya wakala kuchagua bei za chini. Matokeo yake, mawakala wamekuwa wakitoza bei za juu kwa zaidi ya asilimia hamsini (50%) ya kima cha

[15] Instructions to Bidders (ITB);Clause 15.5.

[16] Wizara ya mambo ya nje

chini japokuwa kulikuwa na fursa ya kupata tiketi zilezile kwa bei za chini zaidi.

Kwenye sampuli ya tiketi 32 za usafiri wa ndani, kulikuwepo na fursa za mawakala kuchagua bei kati ya TZS 60,000 na TZS 470,000. Hata hivyo bei halisi zilizochukuliwa zilikuwa kati ya TZS 109,000 mpaka 360,000. Matokeo yake taasisi ililipa TZS 7.5 milioni ambapo kulikuwa na uwezekano wa kulipa chini zaidi kufikia TZS 4.1 milioni na kuokoa kiasi cha TZS 3.4 milioni. Kwa wastani, nusu ya tiketi za safari za ndani ziligharimu kiasi ch TZS 100,000 zaidi ya kiwango cha chini cha nauli wakati wa kufanya manunuzi (booking).

Vilevile, kwenye sampuli ya tiketi 45 za safari za nje, kulikuwepo fursa ambayo ingemwezesha wakala kuchagua bei kati ya TZS 488,250 hadi 46,379,100. Hata hivyo bei iliyochukuliwa ilikuwa kati ya TZS 919,150 hadi 40,351,150. Matokeo yake wizara ililipa kiasi cha TZS 611.9 milioni ingawa wangeweza kulipa kiasi cha chini kufikia TZS 366.6 milioni na kuokoa ongezeko la kiasi cha TZS 162.3 milioni. Kwa wastani, nusu ya tiketi zilizonunuliwa kwa safari za nje ziligharimu TZS 2 milioni kila moja zaidi ya kiwango cha chini kilichokuwepo wakati wa kufanya manunuzi.

Sampuli ya tiketi 72 kwa safari za nje ilichukuliwa kutoka Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Malisasili na Utalii. Baadhi ya tiketi hizi hazikuonesha kiasi cha nauli pamoja na mnyumbuliko wake. Kwa sababu hiyo, nauli zilizalishwa kutoka kwenye mtandao wa usambazaji taarifa za nauli za ndege (GDS) na ilibainika kwamba tiketi 56 kati ya 72 zilitozwa zaidi. Hii ni sawa na asilimia 78 ya sampuli iliyochukuliwa. Ukaguzi ulibaini pia kiasi ambacho kilitakiwa kutozwa kilifikia TZS 700.9 milioni lakini kiasi halisi ambacho kililipwa kilikuwa TZS 974.5 milioni ambayo ni TZS 273.6 zaidi ya kiasi kilichotakiwa kulipwa.

Kutowekwa wazi kwa taarifa muhimu kwenye tiketi za ndege

Mapitio ya tiketi yalionesha kuwa asilimia 12.5 ya sampuli ya tiketi 32 kwa safari za ndani zilionesha kiasi cha nauli. Sampuli ya tiketi 72 kwa safari za kimataifa ilionesha kuwa ni asilimia 11 tu ya tiketi zilizokuwa na taarifa muhimu ikiwemo nauli na mchanganuo wa kodi. Tiketi zilizobaki hazikuonesha taarifa muhimu kama vile gharama za huduma, kodi, kiasi cha nauli na mahesabu ya kukokotoa nauli. Taarifa hizi ni muhimu na hutakiwa kuwepo kwenye tiketi kwani ni sehemu ya mkataba kati ya mnunuzi na mnunuaji wa huduma na zinatakiwa kuwekwa bayana.

Uchaguzi wa namna ya kukokotoa nauli

Ili kufikia kiasi cha nauli kinachofaa, mawakala wanaweza kuamua namna bora ya kufanya mahesabu pale ambapo nauli tofauti zinahusika kwa safari moja. Ukaguzi ulibaini mchanganyiko wa mahesabu ya nauli kwa tiketi No. 1763275774603/4 (daraja la kwanza) ambazo zilileta matokeo ya nauli ya juu kwa kiasi cha Dola za Marekani 30,520 (sawa na Shilingi 40.8 milioni). Aidha viwango vya juu sana vilitumika kwenye kukokotoa nauli. Endapo kungekuwa na uchaguzi mzuri wa namna ya kukokotoa nauli kwa kutumia viwango hivyohivyo vya juu, taasisi ingeweza kugharimu kiasi cha Dola za Marekani 6,000 (Shilingi 9.6 milioni).

Taasisi za manunuzi hazihakiki Ankara za malipo dhidi ya tiketi

Ilibainika kuwa taasisi za manunuzi hazihakiki uhalisi wa ankara kutoka kwa mawakala. Isipokuwa Ofisi ya Rais menejimenti ya Utumishi wa Umma, taasisi zingine zote zimekuwa zikiwalipa mawakala bila kuhakiki uhalali wa malipo yanayodaiwa na mawakala. Mawakala wa usafiri wa anga wamekuwa wakidai malipo kutoka kwa taasisi hizo bila kuonesha mchanganuo wa tozo zote kama vile nauli, kaodi, ukokotozi wa nauli pamoja na alama zinazoonesha kiasi cha nauli (codes). Hii ilipelekea uwezekano wa taasisi hizo kulipa zaidi ya wanachodaiwa au kulipia huduma ambayo haikutolewa.

Kutokuwepo kwa ushindani wakati wa kuagiza tiketi

Ilionekana kwamba kwa baadhi ya taasisi za manunuzi, mawakala walewale wamekuwa wakitoa huduma kwa kipindi kirefu bila kubadilika. Kulikosekana ushindani wakati wa kuchagua wakala wa kutoa huduma ya usafiri. Taasisi zilitegemewa kuwasilisha mahitaji yao kwa wakala zaidi ya mmoja ili kupata bei zao. Hii ni kwa sababu gharama za huduma zilikuwa tayari zimewekwa japo za gharama za nauli zingeweza kutofautiana kwa kutegemea na shirika la ndege, namna ya kukokotoa nauli, n.k. Mahojiano na maofisa mbalimbali wa GPSA na wizara husika yaliashiria kuwa GPSA na taasisi za manunuzi hazikuwa na uelewa juu ya uwezekano wa kuokoa fedha endapo mawakala wangeshindanishwa.

Taasisi za manunuzi hazizingatii utaratibu wa manunuzi

Kwa kuzingatia kanuni na miongozo, taasisi za manunuzi zilitarajiwa kupata huduma ya usafiri kutoka kwa mawakala walioidhinishwa na GPSA. Hata hivyo mapitio ya nyaraka kutoka wizara ya maliasili na utalii yalibaini kutokuzingatia matakwa hayo kwa wakati wote wa manunuzi kwani walitumia mawakala wawili[17] ambao hawakuidhinishwa na GPSA kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Kuagiza tiketi kwa dharura

Taarifa kuhusu tiketi za ndege na muda wa kuagiza ilichukuliwa kutoka sampuli ya tiketi 36 kutoka wizara ya mambo ya nje ilionesha kwamba, kwa wastani, wizara ilipata taarifa za safari siku 9 kabla. Hata hivyo uagizaji wa tiketi ulifanyika kwa mtindo wa dharura. Karibu nusu ya uagizaji wa tiketi ulifanyika siku 3 kabla ya safari. Ilichukua hadi siku 33 kwa wizara kuagiza tiketi kutoka kwa mawakala.

---

[17] Sunshine Travel and Tours Ltd na Omongwe Travel and Tours Ltd

7.4.2 Ujenzi wa majengo ya Umma katika Halmashauri

Kutokuwepo kwa bei elekezi na makadirio yasiyo sahihi

Asilimia 47 ya miradi iliyokaguliwa haikuwemo mipango wa manunuzi ya mwaka. Asilimia 16 ya miradi haikuwa na makadirio ya mhandisi. Asilimia 45 ya miradi yote haikuwa na bajeti ingawa ilitekelezwa. Baadhi ya Halmashauri ziliweka fungu kwenye bajeti kwa ajili ya ujenzi wa madarasa bila kuonesha/kuorodhesha shule zilizohusika na idadi ya madarasa yaliyotarajiwa kujengwa.

Tofauti kati ya bei katika mikataba na makadirio ya wahandisi

Mapitio ya nyaraka kutoka LGAs zilizobainishwa zilionesha kulikuwepo na utofauti mkubwa kati ya bei zilizotolewa na wakandarasi dhidi ya makadirio ya wahandisi. Bei ya zabuni ilikuwa kati ya asilimia 18 chini ya makadirio ya wahandisi hadi kufikia asilimia 55 juu ya makadirio ya mhandisi. Kwa wastani bei za wazabuni zilikuwa juu kwa zaidi ya asilimia 11. Kwa ujumla wastani wa bei zilizosomwa katika Halmashauri zote wakati wa ufunguzi wa zabuni zilizokuwa juu ya makadirio ya wahandisi isipokuwa katika halmashauri ya mji wa Kibaha.

Tofauti kati ya bei iliyolipwa dhidi ya bei za kwenye mikataba

Ukaguzi ulibaini kuwa miradi 45 kati ya miradi 64 iliyokaguliwa ilikuwa imekamilika na kiasi cha pesa kilicholipwa kilikuwa sawa kwa mujibu wa mikataba japo kulikuwepo na tofauti ndogondogo. Tofauti zilizobainishwa zilitokana na fedha za dharura ambazo hazikutumika pamoja na fedha ziliyoshikiliwa kwa mujibu wa mkataba ambayo ilikuwa haijarejeshwa kwa mkandarasi. Pia baadhi ya malipo yalifanyika kwa kazi ambazo hazikutekelezwa kama ilivyooneshwa kwenye mkataba. Miradi 15 ilikuwa haijakamilika wakatimiradi mingine 4 ilikamilika japokuwa gharama iliyolipwa ilitofautiana kwa kiasi kikubwa na gharama iliyoainishwa kwenye mikataba ya awali.

Matumizi ya bei elekezi wakati wa kutoa tuzo kwa mzabuni

Ilibainika kwamba wakati wa kutoa tuzo kwa mkandarasi, kipaumbele kilitolewa kwa kuzingatia bajeti pamoja na makadirio ya mhandisi. Mapitio ya mkadirio hayo pamoja na mahojiano na maofisa[18] katika Halmashauri zilizochaguliwa yalionesha kwamba makadirio hayakuandaliwa kitaalamu kwani maofisa wote walishindwa kuonesha namna walivyokokotoa viwango vya bei zilizotumika kuandaa makadirio hayo. Kwenye mazingira ambayo makadirio hayakuwepo, bajeti zilitumika kama moja ya iigezo cha tathimini ya zabuni.

Upendeleo wa kutumia nukuu (quotations) wakati wa manunuzi

Idadi kubwa ya zabuni zilitolewa kwa njia ya nukuu na kutangazwa kwenye mbao za matangazo jambo lililofanya zabuni kukosa ushindani kwa sababu ya wigo mdogo wa matangazo na idadi ndogo ya wazabuni katika mchakato wa zabuni. 'Quotations' mara nyingi ni rahisi kuathiriwa na upangaji bei na hivyo kuongeza gharama. Vile vile Halmashauri hazikufuata utaratibu 'pre-qualification' kuwapata wazabuni kama sheria ilivyoagiza[19] pale ambapo utaratibu wa 'quotation' ulitumika.

Mipango ya manunuzi kutoheshimiwa

Mahojiano yaliyofanyika kwenye kitengo cha kusimamia manunuzi (PMU) katika Halmashauri yaliashiria kwamba mipango ya mwaka ya manunuzi hujumuisha miradi yote ambayo inatekelewa na Halmashauri. Hata hivyo mapitio ya nyaraka yalibainisha kuwa asilimia 58 ya miradi yote iliyokaguliwa haikuwemo kwenye mpango wa manunuzi wa miaka husika.

Kuondolewa kwa mzabuni mwenye bei ya chini

[18] Wakadiriaji majengo na wahandisi kwenye Ofsisi ya mhandisi

[19] Kanuni Sheria ya Manunuzi ya Umma, kifungu 67(1) (TS No. 90/2005)

Halmashauri zinatakiwa kufanya tathmini ili kubaini mzabuni mwenye bei ya chini ambaye pia ametimiza vigezo vilivyowekwa katika nyaraka za zabuni.[20] Mapitio ya taarifa za tathimini za zabuni yalibainisha baadhi ya wazabuni walikuwa na bei za chini ambao hata hivyo waliondolewa katika hatua mbalimbali za mchakao wa uchambuzi kwa sababu ya kutofikia vigezo vilivyowekwa. Asilimia 27 (ambayo ni miradi 17 kati ya 64) ya zabuni zilizokuwa na bei ya chini ziliondolewa kwenye mchakato wa tathimini. Ilionekana pia asilimia 31 ya zabuni zilizotuzwa zilikuwa juu ya makadirio ya mhandisi, asilimia 56 chini ya makadirio ya mhandisi na asilimia 13 zilikuwa sawa na makadirio ya mhandisi.

Mapungufu wakati wa mchakato wa manunuzi

Wajumbe wa kamati za tathmini za zabuni kwenye Halmashauri hawakuwa na sifa na walichaguliwa bila kuzingatiwa mahitaji halisi. Taarifa za tathmini zilionesha maamuzi dhaifu na yasioridhisha kwa upande wa kamati za tathmini. Kasoro ndogo ndogo kwenye nyaraka za wazabuni zilionekana kuwa kasoro kubwa zilizosababisha kuondolewa mara moja kwa mzabuni.

Marekebisho ya kimahesabu kwenye bili ya makadirio ya bei (BOQ) na makosa ya kujumlisha yalikuwa bayana muda mwingi na ama yalizingatiwa kwenye tathimini ama kutupiliwa mbali wakati wa tathimini ya mwisho na ukokotoaji wa gharama mikataba husika. Vitengo vya kusimamia manunuzi katika Halmashauri husika havikukagua taarifa za tathimini ili kuhakiki usahihi wake kama miongozo inavyoelekeza.

Kufuata vipengele vilivyokubaliwa wakati wa kutekeleza masharti ya mkataba

(i) Kuchelewa kwa kukamilika kwa miradi

[20] Kanuni ya Manunuzi ya Umma, kifungu No. 18(a) (TS No. 90/2005)

Miradi iliyochaguliwa haikukamilika kwa wakati. Hata hivyo Halmashauri nyingi hazikutoza fidia[21] kwa wakandarasi. Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero pekee ilitumia kipengele hiki cha mkataba kwa miradi yote iliyocheleweshwa na wakandarasi pasipo sababu za msingi. Wilaya ya Bahi na Manispaa ya Morogoro zilitoza fidia kwa miradi kadhaa iliyochelewa kukamilishwa. Kwenye Halmashauri zilizobaki fidia ya uchelewaji haikutozwa ingawa kulikua na uchelewaji ulianzia miezi miezi 3 hadi 33.

(ii) Uchelewashwaji wa malipo kwa wakandarasi

Kwa mujibu wa mapitio ya mikataba, malipo kwa wakandarasi yalitakiwa kufanyika ndani ya siku 28 baada ya mkandarasi husika kuwasilisha hati ya madai. Hata hivyo palikuwepo na uchelewaji mkubwa ambao ulifikia siku 160 kuanzia siku ya madai. Hali hii ilisababisha uwezekano wa Halmashauri kulipa faini inayofikia asilimia 17 ya gharama za mradi.

(iii)Malipo kufanyika kwa kazi zilizo chini ya kiwango

Ilibainika kuwa miradi 19 kati ya 51 iliyotembelewa ilikuwa na hali isiyoridhisha ikilinganishwa na kile kilichotakiwa kufanywa na mkandarasi. Hii ilitokana na wakandarasi kufanya kazi bila usimamizi wa kutosha. Ni miradi 3 tu ambayo ilikuwa na rejesta za wageni na vitabu vya maelekezo ambavyo vingeweza kuonesha kumbukumbu za maofisa kutoka ofisi za wahandisi wa halmashauri waliotembelea maeneo ya ujenzi kwa ajili ya usimamizi. Rejesta hizi tatu hata hivyo hazikuonesha endapo maofisa kutoka ofisi za wahandisi walitembelea miradi hiyo.

7.4.3 Majukumu ya Tasisi za Usimamizi na Udhibiti

[21] Kiasi cha fedha kinachotozwa endapo mkandarasi amechelewa kukamilisha mradi kama fidia kwa mteja (Halmashauri)

Majukumu ya GPSA katika kusimamia bei

Wakala wa Ununuzi (GPSA) haikufanya utafiti na mchanganuo wa kutosha wa bei za bidhaa na huduma na matokeo yake, ilishindwa kuwa na njia bora ya kudhibiti bei na gharama ya huduma zinazotolewa na mawakala pamoja na wakandarasi. Kwa mfano, kwenye mikataba inayoandaliwa na GPSA, GPSA ilijikita katika gharama ya huduma. Mambo mengine yaliyoathiri bei za tiketi kama uchaguzi wa shirika la ndege, njia na ukokotozi wa bei yaliachwa kwa mawakala wa huduma za usafiri kwa ajili ya kuamua.

Ufuatiliaji na tathmini ya mikataba

GPSA inatakiwa kufanya tathimini utendaji wa taasisi za manunuzi juu ya matumizi ya mikataba ya msingi na kuandaa taarifa[22] ya tathimini hizo. Ilibainika kwamba GPSA hawafanyi tathimini na ufuatiliaji juu ya matumizi ya mikataba ya msingi ili kubaini inavyoandaliwa na kutumiwa na taasisi za manunuzi.

Wajibu wa TCAA katika kusimamia gharama za usafiri wa anga

Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCCA) haikuwa ikitimiza wajibu wake wa kisheria[23] wa kusimamia viwango vya nauli za usafiri wa anga. Mahojiano na maofisa wa TCAA yalibainisha kuwa majukumu ya mamlaka hayakuwa sehemu ya kazi ya mamlaka na kwamba bei ya nauli ilitegemea zaidi nguvu na mabadiliko ya soko. Mamlaka ilichukua jukumu la kuongeza ushindani pale ambapo kulionekana hali ya kuwepo kwa hali ya ukiritimba. TCAA hawakutambua majukumu yao ya kusimamia viwango vya nauli za ndege na hivyo kusababisha mawakala wa usafiri wa anga kukosa msimamizi na hivyo kutoza kadiri walivyoona inafaa.

---

[22] GPSA establishment order 2007 no. 3.1, 9.6; GPSA establishment order 2007 GN 111 from 13/4/2012 – the executive agencies act – no. 2.3.1.5 (d), 2.3.3 (a) is required to Formulate, monitor and evaluate the implementation of Procurement of Common Use Items through framework contracts.

[23] The Tanzania Civil Aviation (Economic regulation) Regulation 9(1) of 2006

7.5 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya ukaguzi, inahitimishwa kuwa wadau wanaohusika na ununuzi wa umma hawakushughulikia masuala yanayohusu udhibiti wa gharama katika ununuzi, ingawa sheria na taratibu zinawapa nafasi ya kulinda rasilimali za umma na kuepuka matumizi makubwa yanayoepukika. Kwa ujumla ununuzi wa umma unaathiriwa na vitu vifuatavyo:

- **Ni kawaida kwa taasisi za ununuzi kuwa na mipango, bajeti na makadirio ya gharama yasiyofanana na hali halisi;**
- **Kukosekana kwa ushindani wakati ya uteuzi wa watoa huduma na wakandarasi;**
- **Watoa huduma/wakandarasi hawasimamiwi ipasavyo na wakati mwingine malipo hufanyika bila ya kuhakiki kazi zilizofanyika au huduma iliyotolewa; na**
- **Mamlaka zinazoshughulikia ununuzi wa umma, hazishughulikii kikamilifu masuala yanayohusu udhibiti wa gharama katika ununuzi wa umma.**

Sehemu ya mapungufu hayo yanasababishwa na mambo yafuatayo:

- **Mamlaka zinazoshughulikia ununuzi wa umma, hazipati taarifa za kutosha kutoka kwa taasisi za manunuzi;**
- **Ni vigumu kugundua mianya ya rushwa kutokana na njia na zana zinazotumiwa na mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa umma;**
- **Taasisi za ununuzi wa umma hazifanyi majadiliano (negotiation) na watoa huduma au wakandarasi ili kuingia mikataba yenye manufaa kwa umma;**
- **Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa haijawezeshwa vya kutosha kuweza kuchunguza rushwa katika maeneo ya ununuzi wa umma; na**
- **Kuna ukosefu wa miongozo ya kuweza kushughulikia masuala ya serikali yanayofanana.**

7.6 Mapendekezo

Mapendekezo yanaelekezwa katika masuala ya kimkakati (sera na utawala) katika usimamizi wa ununuzi wa umma kitaifa kama ifuatavyo:

1) **Divisheni ya Sera ya Ununuzi wa Umma iliyoko Wizara ya Fedha, kiangalie upya miongozo inayotumika katika ununuzi wa ujenzi, bidhaa na huduma kwa lengo la kupunguza gharama zinazoepukika. Hii ni pamoja na sera na kanuni zinazohusu mafuta,nauli ya usafiri wa anga,huduma za kiutaalamu na ujenzi wa majengo ya serikali. Hii itasaidia katika kuepuka mambo kama yafuatayo:**
    i. **Kulipia daraja la juu katika usafiri wa anga pale maafisa wanaposafiri ndani na nje ya nchi kwa ndege zisizo na daraja hilo;**
    ii. **Kusafiri kwa daraja la juu bila ya kujali urefu wa safari;**
    iii. **Kuweka lita 10 ya mafuta katika kila gari la serikali linalotumiwa na afisa kila siku bila ya kujali matumizi ya mafuta ya gari husika wala umbali linaotembea kila siku;**
    iv. **Kurudia rudia kugharamia usanifu wa majengo ya serikali kwa kukosa miongozo juu ya aina za majengo kulingana na matumizi yaliyokusudiwa;**
2) **Mlipaji mkuu wa serikali anapaswa kuhakikisha kuwa Kitengo cha Sera za Ununuzi wa Umma (PPD) kinatekeleza majukumu yake ipasavyo, ya kuratibu na kuandaa miongozo itakayotumiwa na Taasisi za Manunuzi ili kulinda masilahi ya Taifa.**
3) **Kitengo cha sera ya ununuzi wa umma kifikirie juu ya uwezekano wa kufanya majadiliano ya moja kwa moja na wakandarasi na watoa huduma yatakayolenga kupunguza gharama za huduma husika au kuongeza ubora wa huduma bila kuongeza gharama.**

4) Serikali inahitaji kuimarisha uwezo wa taasisi kama TAKUKURU na Mamlaka ya Udhibiti wa manunuziwa Umma, ili ziweze kufanya uchunguzi unaolenga kubaini vitendo vya rushwa katika ununuzi wa umma. Sambamba na hilo:
    i. TAKUKURU wafikirie kufanya uchunguzi zaidi kwenye masuala ya ununuzi;
    ii. TAKUKURU wafikirie kutambua maeneo hatarishi na yenye viashiria vya rushwa katika taasisi za ununuzi wa umma. Hi inaweza ikafanyika kwa kukusanya taarifa za ununuzi katika taasisi za umma kwa lengo la kuzuia, kugundua na kuchunguza masuala ya rushwa katika ununuzi.
5) Wakala wa Ununuzi wa Serikali (GPSA) inatakiwa kuzitambua bidhaa na huduma muhimu zinazoigharimu sana serikali na kuandaa utaratibu wa kuzifuatilia ununuzi wake, kwa mfano nauli ya usafiri wa anga.
6) Serikali iangalie uwezekano wa kufanya ununuzi kwa njia ya mtandao wa kompyuta kupitia mfumo jumuishi wa usimamizi wa ununuzi (*Integrated Procurement Management System (IPMS))* kwalengo la kupunguza muda wa unaotumika katika kushughulikia manunuzi, kupunguza gharama za ununuzi na kuimarisha huduma.
7) Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuziwa Umma na wakaguzi wa ndani waandae njia zitakazoweza kugundua na kukagua viashiria vya rushwa.

8) Ukaguzi unaofanywa na Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi (PPRA) isiishie kuangalia taratibu tu. Mapitio yajikite pia kwenye utekelezaji ili kujiridhisha endapo

9) unalingana na hali iliyotakiwa kuwapo, kuanzia kwenye mipango, mchakato wa manunuzi na hatua ya utekelezaji.

10)Kitengo cha Sera ya Ununuzi katika ngazi ya kitaifa kinatakiwa kibuni teknologia ya kupambana na udanganyifu na rushwa katika masuala ya ununuzi na kiboreshe usimamizi, utambuzi, uchambuzi na kuzitaarifu Taasisi ya ununuzi.

11)Kuna haja wa kupeana habari zinazohusu ununuzi katika sekta ya umma katika ngazi ya kitaifa baina ya taasisi za ununuzi na taasisi za udhibiti kama vile TAKUKURU, Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi wa Umma (PPRA), na Wakala wa Ununuzi wa Umma (GPSA). Hii itaimarisha usimamizi katika ununuzi wa umma.

12)Taasisi za udhibiti ziweke mifumo mizuri ya kupata habari kutoka kwa raia wema na kuhakikisha kuwa wapasha habari wanalindwa ili waweze kuendelea kutoa habari zitakazopelekea kubainika kwa vitendo vya rushwa.

13)Serikali inapaswa kurekebisha sheria ili kuiwezesha kitengo cha Sera za Ununuzi (PPD) kusimamia shughuliza manunuzikatika ngazi zote zaserikali, yaaniSerikali KuunaSerikali za Mitaa.

SURA YA NANE

MADHAIFU YALIYOTAMBULIWA KUWA YA KAWAIDA KUONEKANA KWENYE SHUGHULI ZA SERKALI KATIKA KAGUZI ZA UFANISI ZILIZOFANYIKA

8.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia muhtasari wa madhaifu yaliyoonekana katika kaguzi nyingi za ufanisi na maalumu zilizofanyika kwa kipindi kilichoishia Machi 2014. Lengo la sura hii ni kuonyesha madhaifu ya kawaida ambayo yanapaswa kuangaliwa na serikali. Kulingana na malengo ya ukaguzi na matokeo yaliyoonekana katika kaguzi sita zilizofanyika kama ilivyoelezwa kwa kifupi katika katika ripoti hii, kuna masuala yanayohitaji kuitaadharisha Serikali ili kuhakikisha kuwa serikali inaendesha na kusimamia shughuli zake kwa ufanisi.

8.2 Madhaifu ya kawaida yaliyobainishwa

Masuala yenye udhaifu yaliyoonekana katika kaguzi nyingi ni kama ifuatavyo:

8.2.1 Mipango isiyotosheleza

Kwa serikali kutekeleza wajibu wake ipasavyo, mipango sahihi ni muhimu sana kama mkakati wa kuweza kufikia malengo yake. Hata hivyo, imekuwa kawaida kama ilivyobainishwa katika kaguzi za ufanisi na maalumu kwamba mipango ambayo ni mkakati mzuri haiandaliwi, haitekelezwi, haifuatiliwi na kutathminiwa kiusahihi. Hii ni kama nilivyoeleza hapa chini:

Imebainika katika Ukaguzi wa bidhaa kutoka nje, TBS ina idadi kubwa ya zana ambazo zinaweza kutumika kama msingi wa mipango ya ukaguzi wa bidhaa kutoka nje. Hizi ni kama vile Mwongozo wa utaratibu wa kukagua bidhaa zinazoingizwa nchini, mwongozo wa cheti cha bidhaa na miongozo iliyowianishwa wa kibali cha kutoa mizigo. Hata hivyo, TBS haijaweza kutumia nyenzo hizo ili kuboresha uwezo wake wa kutambua hatari kubwa au kuzuia kuingia kwa bidhaa zilizochini ya kiwango.

Katika ukaguzi wa Usimamizi wa watoto wanaoishi katika mazingira magumu, imekuwa wazi kwamba jukumu la kutambua halitekelezwi ipasavyo. Hii ni kutokana na udhaifu katika mipango. Si maeneo yote yalipangwa kufikiwa katika hatua ya mipango . Hii ni kutokana na ukweli suala la WWKMH halikuonekana kama sualala maendeleo kutoka ngazi ya kijiji / mtaa hadi ngazi ya halmashauri. Hii pia imesababisha mapungufu yaliyoonekana katika utoaji wa huduma kwa WWKMH.

Ilibainika pia katika ukaguzi kuwa mipango ya maendeleo ilikuwa kimya juu ya vipengele muhimu kama vile kutimiza lengo katika idadi ya WWKMH waliotambuliwa au kupewa huduma; vijiji / mitaa kufikiwa, na jinsi gani utendaji utapimwa. Mipango ya pamoja ni haiandaliwi ipasavyo kati ya Halmashauri / Sekretarieti ya Mkoa na washirika wa utekelezaji katika utoaji wa huduma kwa WWKMH . Washirika wengi wa utekelezaji wanatumia vipaumbele vyao husika mdhamini / mfadhili kama msingi wa kutoa huduma kwa WWKMH .

